ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
3. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
4. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
5.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
6. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
7. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
8. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge

9. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
10. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
11. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
12.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
14. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
15. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
17. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
18. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
20. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
21. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
22. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
23. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
24. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
26. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
27. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
28. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
29. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
30. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
31. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
32. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
33. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
34. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani

35. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
36. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
37. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
39. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
40. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
42. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
43. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
44. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
45. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
46. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
47. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
48. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
49. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
50. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
51. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
52. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
53. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
54. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
55. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
56. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
57. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
58. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Jimbo la Chukwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
66. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tatu - Tarehe 24 Mei, 2016

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 50

Askari Jamii Kukiuka Dhamana Zao

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza**:**

Kwa kuwa lengo la kuanzisha Ulinzi Shirikishi la Polisi Jamii ni kukabiliana na vitendo vya uhalifu. Na kwa kuwa hivi sasa kumekuwepo na malalamiko ya askari wake baadhi yao kutumia vibaya dhamana waliyopewa ikiwemo vitendo vya kupiga watu wanaowakamata na wakati mwengine kuwanyang'anya vitu vya thamani.

a) Serikali imefuatilia vipi utaratibu wa askari jamii baada ya kujitokeza malalamiko ya watu kunyang'anywa mali zao ikiwemo Shehia ya Malindi.

b) Kwa nini Polisi Jamii hawafanyi doria kwa kushirikiana na Polisi ambao wana ujuzi na taaluma ya kukabiliana na uhalifu au mtu yeyote anayetiliwa shaka.

c) Je, kuna tija gani iliyopatikana tangu kuanzishwa utaratibu wa Polisi Jamii katika Shehia mbali mbali hasa katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi makini swali lake Nam. 50 lenye vifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

a) Kwa mujibu wa taarifa za Jeshi la Polisi mpaka sasa hakuna taarifa au lalamiko rasmi lililoripotiwa katika kituo cha Polisi juu ya suala hili la

kunyang'anywa mali za wananchi na Polisi Jamii ikiwemo Shehia ya Malindi.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa taarifa za Jeshi la Polisi mpaka sasa litaendelea kuhakikisha usalama wa wananchi na mali zao inaheshimiwa na haitovumilia kitendo chochote cha uvunjaji wa Sheria ikiwemo kunyang'anywa mali za wananchi.

Mhe. Spika, Serikali imeliagiza Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi zaidi juu ya kadhia hii, na taarifa yake kuwasilishwa Serikalini ili kupata undani wa jambo hili na hatua madhubuti kuchukuliwa.

b) Mhe. Spika, katika utekelezaji wa Sera ya Polisi Jamii, Jeshi la Polisi limepeleka Askari katika kila Shehia hapa Zanzibar, askari huyo pamoja na kazi nyengine za Kiulinzi alizonazo kwenye Shehia husika anatakiwa kushirikiana na Vijana wa Ulinzi Shirikishi katika kufanya doria kwenye Shehia zao. Kama kuna kikundi cha Ulinzi Shirikishi kinafanya doria bila kuambatana na Askari aliyepelekwa katika Shehia yao kikundi hicho kielewe kinafanya kazi kinyume na utaratibu uliopangwa.

c) Mhe. Spika, kwa ujumla uanzishwaji wa Sera ya Polisi Jamii katika Shehia mbali mbali hapa Zanzibar hasa katika Mkoa wa Mjini/Magharibi umeleta tija kubwa kama ifuatavyo:-

Kujenga hali ya kuaminiana baina ya Jeshi la Polisi na Jamii, hali inayopelekea wananchi kujenga mashirikiano ambayo yamewezesha Jeshi la Polisi kupata taarifa nyingi za kihalifu kabla na baada ya uhalifu kutendeka, jambo ambalo linasaidia kupunguza uhalifu nchini hasa katika maeneo ambayo uhalifu huu umekithiri.

Kupitia dhana ya Jeshi la Polisi Jamii, jamii imehamasisha Kamati za Ulinzi na Usalama za Shehia kukaa na kutatua matatizo madogo madogo ya kijamii kabla hayajaleta athari kubwa kwa wananchi na kwa nchi kwa jumla.

Mhe. Spika, Serikali inatoa wito kwa jamii kuitekeleza dhana Polisi Jamii kwani imesaidia kutatua kero zinazojitokeza na kupunguza uhalifu katika maeneo mbali mbali nchini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumsifu Mhe. Waziri; Waziri ambaye kwa muda mrefu alikuwa hana jimbo kwa majibu muafaka kabisa aliyojibu kwa niaba ya serikali, nikushukuru. Naomba kuuliza swali moja dogo sana la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Kwa kuwa malalamiko, naomba Mhe. Naibu Spika, nizungumze kidogo kidogo maana yake Mhe. Mohammed Aboud ana matatizo ya kutokusikia kwa sauti. Kwa kuwa malalamiko ya matumizi mabaya kwa Polisi Jamii hayaleti sura nzuri kwa serikali. Hatua gani zimechukuliwa za kuhakikisha Askari Jamii wanafanya kazi zao bega kwa bega na Askari Polisi wakati wa doria ili wajue jinsi ya kukabiliana na mtu wanayemkamata bila ya kutumia matumizi ya nguvu wanapokuwa kwenye doria.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku utaratibu wa maswali ya nyongeza husomi, liulize kutokana na majibu ambayo umepewa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, mimi si mzoefu, ninashukuru hichi ni kipindi cha pili, sisomi swali. Hii ni kutokana kuwa hasikii ndiyo maana nikainama chini.

Mhe. Naibu Spika: Tumekuona unasoma.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kama utaniruhusu nisome hivyo hivyo. Hata ukiniruhusu nitasimama lakini mimi hanisikii.

Mhe. Naibu Spika: Tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub:

a) Kwa kuwa malalamiko ya matumizi mabaya kwa Polisi Jamii haileti picha nzuri kwa serikali. Je, serikali imechukua hatua gani ya kukubaliana na askari hao kutoa mafunzo kwa askari hao, ili kuhakikisha mtuhumiwa anapokamatwa askari hawa hawatumii nguvu.

b) Kwa kuwa kazi ya kuhakikisha mhalifu anapokamatwa kuleta malalamiko, na malalamiko hayo yapo Mhe. Mohammed. Je, utakuwa tayari kukuletea watu waliopata kadhia hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa kufuatilia kwa karibu kuhusu usalama wa wananchi wetu. Na jukumu la msingi la Polisi ni kulinda raia na mali zao. Inatakiwa dhamira hiyo itekelezeke vizuri haina budi kuwa na mashirikiano makubwa na jamii. Na ndiyo maana tukawa na dhana ya Polisi Jamii ili tushirikiane katika kuondoa uhalifu nchini, siyo kwa namna yoyote nyengine ile, zaidi ya kujenga mahusiano mazuri na kuhakikisha tunaondoa uhalifu.

Pale ambapo dhana hii inatumika vibaya kwa vyovyote Mhe. Mwakilishi atakubaliana na mimi kwamba siyo dhamira ya serikali wala siyo lengo la serikali itumike vibaya, bali itakuwa ni makosa ya mtu mmoja mmoja. Na sisi serikali hatuna njia ya mkato ya kupata taarifa bila ya kupitia Jeshi la Polisi ama raia wema wanapotoa taarifa hizi.

Na kwa sababu Mhe. Mwakilishi ana taarifa nyingi na yupo tayari kushirikiana na sisi ili kupata taarifa za ziada, ili hatua zichukuliwe kwa wale ambao wanaokwenda kinyume na utaratibu na dhana ya Polisi Jamii. Ninafurahi sana Mhe. Naibu Spika, unapopata taarifa hizo za ziada, maana nia na dhamira ni kuwahudumia wananchi na nchi yetu kubaki katika hali ya usalama na amani. (*Makofi*).

Kwa msingi huo, yapo maeneo ambayo Polisi Jamii inafanya vizuri. Kwa hivyo, ninataka niwapongeze sana wale ambao wanaofanya vizuri. Na wale ambao kuna matatizo, tayari tumeagiza Jeshi la Polisi kupitia maeneo yote kuona ni wapi kuna matatizo na kutafuta namna ya kutatua changamoto hizo. Lakini kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, kwamba bado tumeliagiza Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa jambo hili na hatua madhubuti zichukuliwe baada ya kupata taarifa hizi.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Swali la pili la nyongeza. Mhe. Simai Mohamed Said.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Waziri na nimpongeze sana yeye ni mtaalamu.

Lakini niseme Mhe. Naibu Spika, katika jamii kunakuwa kuna watu wenye rika, mawazo, fikra, utamaduni, malezi na mengi mengineyo. Lakini ningependa kujua ni utaratibu gani unaotumika wa serikali kwa kushirikiana pamoja na hivi vyombo vya ulinzi kuweza kuwatambua na kuwatafuta na ili kuwapata vijana wanaoshiriki katika hili suala zima la Polisi Jamii kwa upande wetu wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Simai Mohamed Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kama umesikiliza uzuri jibu langu la msingi, nilisema kuwa katika kila Shehia kuna askari wa Shehia wa Polisi. Msingi wetu na dhamira yetu kuwa washirikiane na vikosi hivi vya ulinzi shirikishi ili kufanya wajibu wao wa kufuata misingi ya sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

Na dhamira ni ile ile kupunguza uhalifu na ikiwezekana kuuondosha nchini. Kwa msingi huo, Jeshi la Polisi linaelewa shughuli za Polisi Jamii katika Shehia kupitia Askari wa Shehia ya Polisi. Na kama nilivyosema kwamba kwa sasa tumewaagiza Jeshi la Polisi kufanya utaratibu wa zaidi na uchunguzi zaidi kuona ni matatizo yepi yanayojitokeza katika suala zima la Polisi Jamii ili tuelewe undani na hatua madhubuti ziweze kuchukuliwa.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Ali Salum (Shihata).

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi ninaitwa Ali Suleiman Ali (Shihata). Lakini madhali Shihata ndiyo ninaeleweka huko na wananchi wangu. *(Makofi/Kicheko).*

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza ninampongeza Mheshimiwa kwa majibu yake mazuri juu ya kuelimisha jamii kuhusu Askari Jamii katika nchi yetu. Lakini jambo zuri lolote Mhe. Naibu Spika, huwa na viongozi. Kwa hivyo Askari Jamii wengi wametoka mitaani hawakupitia JKU wala JKT. Ni mwanzo wa vurugu katika maeneo yetu.

Na kwa kuwa Askari Jamii hawa wana viongozi wao, ambayo hiyo sera niliyosema kama hawakupitia JKT au JKU hawamo. Je, wizara haioni kuwa

kwa sasa wale viongozi wa Askari Jamii kila maeneo wakapelekwa katika Chuo cha Polisi ili kupewa mafunzo kwa usalama wa wengine.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu rafiki yangu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, inaonekana kutokana na maelezo ya Waheshimiwa Wawakilishi yapo matatizo katika baadhi ya maeneo kwenye ulinzi shirikishi. Kwa msingi huo, ni wajibu wa serikali na Jeshi la Polisi kufanya kazi kwa karibu zaidi kuona matatizo gani ya msingi.

Hata hivyo, ushauri wake tunaupokea tuzungumze na Jeshi la Polisi tuone uwezekano huo anaosema. Lakini la msingi zaidi ni lile lililofanyiwa maamuzi kwamba tuwe na Polisi wa Shehia ili aongoze utaratibu. Inaonekana kwa maelezo haya ya Waheshimiwa Wawakilishi hiyo kazi ya Polisi katika Shehia haifanyiki vizuri, ndiyo maana kunajitokeza matatizo haya.

Kwa hivyo, ninataka niupokee ushauri huu, tutakutana na viongozi wa Jeshi la Polisi ili tuweze kulifanyia jambo hilo na liwe na msingi mzuri. (*Makofi*).

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 9

Uboreshaji wa Mitaro

Mhe. Salma Mussa Bilal (Kny: Mhe. Bahati Khamis Kombo – Aliuliza **:-**

Kwa kuwa mazingira tuliyonayo ni hatari wakati wa mvua, sababu mitaro haisafishwi na wananchi wanatupa taka ovyo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mitaro ili kupunguza maafa hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: - Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 9 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Ofisi kupitia Baraza la Manispaa inaendelea na kazi ya kusafisha mitaro katika maeneo mbali mbali ya Mji wa Zanzibar. Maeneo yaliyosafishwa kwa kipindi cha miezi mitatu kabla ya mvua ya masika ni misingi ya maji ya mvua na maji machafu ya Jang'ombe, Kwa Alinato, na Kwa Abass Hussein. Aidha, juhudi za kuelimisha wananchi zinaendelea siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kupitia mradi wa huduma za Jamii Mjini *"Zanzibar Urban Services Project"* (*ZUSP*) inaendelea kuimarisha misingi ya maji ya mvua ili kupunguza maafa yanayojitokeza katika maeneo mbali mbali ya Mji wetu. Maeneo yaliyofaidika na mradi huo ni Sebleni, Mpendae kwa Binti Amrani, Migombani, Karakana, Chumbuni, Sogea, Jang'ombe na Viwanja vya Mnazi Mmoja.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza ninampongeza Mhe. Waziri kwa juhudi zake kubwa za kuhakikisha kwamba hali ya nchi yetu au miji yetu inakuwa vizuri na salama juu ya kuhakikisha kwamba mitaro ni njia mojawapo ya kuokoa maisha siku za mvua kwa wananchi wetu. Swali langu lipo hapa.

Kwa kuwa mitaro aliyoitaja Mhe. Waziri ipo mingi sehemu ya mjini lakini kwa bahati mbaya Wilaya ya Magharibi hakuigusa.

Je, Mhe. Waziri atakuwa tayari na watendaji kuhakikisha kuitembelea na miradi ya mitaro mengine ambayo ipo katika sehemu ya Wilaya ya Magharibi hasa katika Jimbo langu la Kijitoupele.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi.

Nipo tayari kutembelea katika Jimbo lake Wilaya ya Magharibi ili kujua changamoto ziliopo katika suala zima la kutuama kwa maji machafu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ya swali lake mama, lakini naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwamba miongoni mwa maeneo yaliyoathirika na mvua moja ni Welezo, na hii inatokana na kukosa mitaro katika maeneo yale au mitaro kuziba.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba kumuuliza Mhe. Waziri je, ana mkakati gani wa kujenga au kuizibua ile mitaro hasa katika jimbo langu la Welezo kunusuru kipindupindu kisiendelee kutuathiri na kuwaathiri wananchi wetu? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, katika Jimbo la Welezo na Wilaya ya Magharibi A na B kwa jumla, hakuna hasa miundombinu ya mitaro na hiyo ni kutokana na kwamba bado mji wa maeneo hayo ulikuwa haujapangwa rasmi katika mipango miji na vijiji. Kwa sababu tayari serikali imeshatangaza rasmi kuwepo kwa manispaa ya Magharibi A, ni imani yangu kwamba baada ya watendaji kufika kwenye *site* na kufanya kazi zao watashirikiana na mipango miji yaani Idara ya Mipango Miji na Vijiji, ili kupanga mji wa Manispaa ya Magharibi B na suala la mitaro litazingatiwa.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.
Mhe. Naibu Spika, mbali na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, vile vile nichukue fursa hii pia kulipongeza Baraza la Manispaa, kwa kazi nzuri ya ushirikiano na kuweza kufanya usafi, kwa kushirikiana viongozi na wananchi katika Jimbo la Kikwajuni katika kipindi cha nyuma kilichopita cha wakati wa mvua.

Mbali na pongezi hizo. Swali langu ni kwamba je, Manispaa haioni kwamba ipo haja ya kusafisha mitaro kwa kushirikiana na serikali za shehia kila wakati wa siku za Jumamosi na Jumapili za mwisho wa mwezi, ili kuondoa tatizo hili la mitaro kujaa michanga pamoja na takataka ili kuondoa tatizo linalojitokeza katika kipindi cha mvua?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, Baraza la Manispaa liko tayari kushirikiana na mwananchi yeyote katika kutekeleza kazi hii ya kusafisha mitaro ya Zanzibar. *(Makofi)*

Nam. 33

Kuwepo kwa Adhabu ya Kutumikia Huduma za Jamii

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-
Mahakama nyingi duniani ikiwemo Tanzania Bara zimeanza kutekeleza Sheria ya wafungwa kupewa adhabu ya kutumikia maeneo ya huduma za jamii jambo ambalo linazidisha usafi wa mazingira.

a) Je, Serikali ya Zanzibar kupitia Mahakama zake itaanza lini kutoa adhabu za kutumikia huduma za jamii kama ilivyo nchi nyengine.

b) Kwa kuwa mwizi wa kuku anatumia gharama kubwa kwa adhabu ya kutumikia Chuo cha Mafunzo kuliko thamani ya kuku 1 aliyeiba, je Serikali haioni wakati umefika wa kutoa adhabu ya kutumikia huduma za jamii.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b) naomba nitoe maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, maana ya adhabu ya kutumikia jamii ni utaratibu maalum wa kisheria ambao unaruhusu mtu aliyetiwa hatiani kwa kosa dogo la jinai kupewa adhabu ya kufanya kazi ya kutumikia jamii, ikiwemo kusafisha barabara, kufanya usafi katika Skuli, Hospitali n.k, badala ya adhabu ya kutumikia Chuo cha Mafunzo. Mpango huu una faida nyingi ikiwemo kuihusisha jamii katika kurekebisha tabia za wakosaji, mkosaji kupata muda wa kuihudumia familia yake n.k.

Mhe. Naibu Spika, baada ya ufafanuzi huo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua kuweko kwa adhabu hiyo ambayo utekelezaji wake upo katika Mikoa miwili tu ambayo imechaguliwa katika kutekeleza mpango wa adhabu za kutumikia Jamii. Mikoa hiyo ni Mkoa wa Mjini Magharibi na Kusini Pemba. Mpango huo umeanza kutumika rasmi tarehe 1 Februari, 2006.

b) Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na maoni ya Mhe. Mwakilishi kwamba wakati umefika wa kuanza kutumika kwa adhabu hizi hapa Zanzibar, na ndio maana Mahakama zetu zimeanza kutoa adhabu hizi tangu mwezi Februari, 2006.

Miongoni mwa sharti la kutolewa kwa adhabu hiyo ni kwamba, mkosaji awe amefanya kosa ambalo adhabu yake haizidi miaka miwili. Hivyo, hata mwizi wa kuku anaweza kupewa adhabu ya

kutumikia jamii badala ya kutumikia Chuo cha Mafunzo kadri mahakama itakavyoona inafaa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kumshukuru Mhe. Naibu Waziri mpya kwa majibu yake muafaka na sahihi, nikushukuru sana na nakutakia kila la kheri. *(Makofi)*

Nataka nimuulize swali moja dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Tangu kuanza mpango wa kutumikia jamii Februari 1, 2006 ni wanafunzi wangapi wamenufaika, na kosa gani yaliyowapeleka huko gerezani na walitumikia vipi. Hilo swali (a).

(b) Kwa kuwa vituo vyetu vya afya vingi vinakabiliwa na tatizo la usafi na uchafu, ikiwemo Hospitali yetu Kuu ya Mnazi Mmoja. Je, ni lini sheria hii au mpango huu mtauanza ili kutumikia wafungwa wanaoiba kuku na mkungu wa ndizi?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

(a) Mhe. Naibu Spika, idadi halisi ya hao wanafunzi au wakosaji ambao waliopata fursa hii ya kutumikia jamii, kwa hivi sasa ni vigumu kukupa jawabu la moja kwa moja, lakini naomba ujue Mhe. Mjumbe kwamba idadi iliyokuwepo ni chache sana hadi sasa.

(b) Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na masuala ya usafishaji wa hospitali. Suala hili kwa kweli ni suala zuri la kuwatumia hawa wakosaji kwenda kufanya kazi hospitali na sehemu nyengine. Tatizo lililokuwepo zile taasisi husika zinakuwa haziko tayari kuwapokea hawa watu, kwa maana kwamba unapozungumzia masuala ya usafi katika hospitali, unazungumzia kwamba hawa wanaopelekwa kusafisha wanatakiwa wapate vifaa mbali mbali ambavyo wanaweza kutumia katika huo usafi. Kinyume ya hilo unapowapeleka kule kusafisha, basi inawezekana badala ya kutumikia jamii na muda wake ukimalizika arudi nyumbani, lakini inawezekana kumbe ikawa ni njia ya kumpeleka kule kupata maradhi na hatimaye kumsababishia hata kifo. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul- latif Yussuf Alwardy: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Je, wizara yake inadhibiti vipi au inapata ripoti gani za unyanyasaji wa wale wafungwa ndani mule, kama Kiinua Miguu pale wanachunguza vipi kuwakamata wale

wanaowanyanyasa wale wafungwa ndani, wakiwemo labda Askari Magereza pamoja na wenyewe kwa wenyewe. Hili ndio swali langu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri umelisikia vizuri swali?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Naomba arudie kidogo.

Mhe. Nadir Abdul- latif Yussuf Alwardy: Nitarudia tena.

Mhe. Naibu Spika: Naomba Mhe. Nadir Abdul- latif uende kwenye swali la msingi.

Mhe. Nadir Abdul- latif Yussuf Alwardy: Ninalouliza ni swali la msingi. Hapa yamezungumzwa maswali ambayo yanamuhusu yeye wizara yake. Kwenye Kiinua Miguu kuna matatizo makubwa ya wafungwa yanafanyika wananyanyasika. Sasa wana mashine gani za kukamata au kuwaona wale ambao wanawanyanyasa wale wafungwa? Hilo ndio swali langu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, wizara yangu hadi hivi sasa bado hatujapokea lalamiko hilo, lakini kama lalamiko hilo lipo basi tutalifanyia kazi na kuchukua hatua ipasavyo. *(Makofi)*

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa kuhakikisha kwamba sheria hii ilipitishwa na Baraza hili tukufu, kwamba baadhi ya watuhumiwa au washitakiwa watumikie adhabu za kuhudumia jamii. Lakini kwa kuwa hapa katika majibu yake ametwambia kwamba, mwanzo huu umeanzia katika Mikoa miwili, Mkoa wa Mjini na Mkoa wa Kusini Pemba.

Je, kwa kuwa kesi nyingi zinaendelea huko vijijini. Kwa mfano Mkokotoni, Mwera na kadhalika, haoni kwamba kuna haja sasa hivi ya kuongeza wigo kwa washtakiwa kama hapa wakapelekewa hizo adhabu katika maeneo hayo, hasa ukizingatia wengi zaidi ni wezi wa kuku na mambo madogo madogo wako huko?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, nikubaliane na Mhe. Mjumbe kwamba tokea uanze mpango huu ni kipindi kirefu sasa.

Mhe. Naibu Spika, naomba Baraza lako tukufu litambue kwamba mikoa hii miwili, Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkoa wa Kusini Pemba, hii tulianzisha kama ni *pilot*. Lengo la serikali ni kuhakikisha kwamba na mikoa mingine inafaidika na huduma hizi, kwa sababu unapopeleka hawa wakosaji katika huduma za kutumikia jamii, vile vile kwa upande wa serikali ni nafuu. Nafuu kwa maana kwamba kwanza ule msongamano katika magereza yetu, katika yale makosa madogo madogo unapungua. Halafu pili zile gharama za kuwahudumia hao wakosaji wakiwa Chuo cha Mafunzo zinapungua kwa upande wa serikali.

Mhe. Naibu Spika, kubwa zaidi ni kushirikiana zaidi na zile taasisi husika wanazopelekewa hawa wakosaji kutoa mashirikiano na vile vile kutoa huduma vikiwemo vile vifaa. Kwa mfano vifaa vya *mask* na kadhalika ili kuwaepusha wale wakosaji kupata maradhi zaidi au matatizo mengine ya kiafya. *(Makofi)*

Nam. 7

Misaada kwa Timu ya Taifa ya Zanzibar

Mhe. Nassor Salim Ali – Aliuliza:-

Ahsante Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuuliza swali langu, naomba kwa ruhusa yako niipongeze sana *Club* ya Yanga kwa kuwa bingwa wa Tanzania. Mbali na ubingwa, nimpongeze Rais wa *FIFA* Gianni Infantino, kwa kuweza kuthamini mafanikio ya *club* hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo Mheshimiwa kwa ruhusa yako naomba swali langu nambari 7 lipate majibu.

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya SMZ chini ya Dkt. Ali Mohamed Shein inastahiki pongezi kwa kuzisaidia kwa hali na mali timu zetu zilizoshiriki katika mashindano mbali mbali kuwakilisha Zanzibar katika mashindano yanayoandaliwa na *CAF* lakini mbali na pongezi hizo.

a) Je, Serikali imejiandaa vipi kusaidia timu yetu ya Taifa ya *Zanzibar Heroes* katika mashindano wanayoshiriki katika nchi za Afrika Mashariki na Kati *CECAFA*.

b) Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kuajiri kocha kutoka nje kuja kuifundisha timu yetu ya Taifa na Serikali kuchukua dhamana ya kulipa mshahara wa kocha huyo. *(Makofi)*

Mhe.Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hizo meza mkizipiga sana mwisho zitavunjika, mnazipiga sana, taratibuni. Najua mnapandwa na jazba lakini taratibu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo – Alijibu:-
Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 7 lenye vifungu (a), na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo inafuatilia kwa karibu sana mahitaji na muelekeo wa Timu yetu ya Taifa ya *Zanzibar Heroes* wakati wa matayarisho na ushiriki wa mashindano ya *CECAFA*.

a) Mhe. Naibu Spika, kwa kawaida serikali kupitia Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo hutenga bajeti maalum kila mwaka kwa ajili ya kuiwezesha Timu ya Taifa ya *Zanzibar Heroes* na *Karume Boys*, kushiriki katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati yanayoandaliwa na *CECAFA* na *CAF*. Baraza la Taifa la Michezo (*BTMZ*) na Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA*) kwa kushirikiana na wadau wengine hujaza pengo la mapungufu na kuhakikisha ushiriki mzuri wa timu zote.

b) Mhe. Naibu Spika, Kupitia Baraza la Michezo, Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA)* kwa kushirikiana na *TFF* huendesha mafunzo mbali mbali ya makocha. Kwa taarifa Mhe. Naibu Spika, Zanzibar inayo walimu, makocha wazuri ambao wana uwezo wa kufundisha Timu ya Taifa.

Kama nilivyoeleza katika maelezo ya utangulizi kuhusiana na uwezo wa makocha, serikali kwa sasa inaona hakuna haja ya kuajiri kocha kutoka nje na vyema kutumia makocha wetu wa ndani kufundisha timu ya Taifa, kama wanavyofanya wenzetu wa Tanzania Bara kwa kutumia makocha wazalendo. *(Makofi)*

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba fedha zinazotengwa kwa kugharamia timu zetu za taifa hazitoshi. Mbali na wadau kuongeza pengo la mapungufu yanayohitaji timu zetu za taifa.

a) Je, Wizara pamoja na Baraza la Taifa la Michezo lina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wanapata udhamini kwa timu zetu za Taifa?

b) Mbali na kuipongeza *TFF* na *ZFA* kuwapatia mafunzo mbali mbali makocha wetu wazawa hapa Zanzibar. Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kuchukua hatua ya kumlipa kocha wetu wa timu ya Taifa ili hao hao makocha wetu wazalendo waweze kuendeleza vipaji vya wachezaji wa Zanzibar kwa timu yetu kuleta ushindi katika mashindano mbali mbali ambayo yanaandaliwa na *CECAFA*.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo*:*

a) Mhe. Naibu Spika, Tutajitahidi tukishirikiana pamoja na wewe pia kwa mawazo yako kama ulivyoeleza tutafute hawa wadhamini kwa kuendeleza timu zetu za Taifa.

b) Mhe. Naibu Spika, pia naungana na Mheshimiwa Mwakilishi na nakiri kwamba makocha wazalendo kama nilivyoelezea katika jibu mama kwamba tunao makocha wazalendo, kwa hivyo nikuhakikishie au nikuahidi kwamba tutafanya kila mpango au kila inavyowezekana tumlipe huyu kocha wetu kwa kumuimarisha ili kuwaendeleza vijana wetu na kusogeza mbele michezo yetu.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kabla ya kumuuliza swali langu na mimi ningewatakia *Club* ya Yanga leo katika kucheza mchezo wa tarehe 24 waweze kupata taji la *FA CUP* ili waweze kufanikisha kupata mataji matatu *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tukirudi kwenye suala la msingi ni kweli kwamba michezo sio eneo la Muungano lakini sisi na ndugu zetu Tanzania Bara tunafanya kazi kwa kushirikiana kwa karibu kabisa, pamoja na udugu wetu tulikuwa nao wa kihistoria. Hapa Zanzibar tuna *ZFA* na kule kuna *TFF* lakini mara nyingi Zanzibar hushiriki katika michezo inayoandaliwa nje ya dunia au inayofanyika pale panapoweza hasa katika Bara la Afrika.

Mhe. Waziri nikuulize swali langu moja, Je, mwaka huu ukiwa ni mwaka muhimu katika michezo duniani, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia Wizara yako mumejipangaje katika ushiriki wa mashindano ya *Olympic* yatakaofanyika mjini Rio De Janairo, Brazil mwaka huu 2016.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii,Utamaduni na Michezo: Naungana na yeye kwamba Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo tunapenda sana timu zetu zishiriki katika michezo ya kimataifa na mfano wa hayo tumeona timu zetu zinavyoshiriki mashindano mbali mbali ya Kimataifa kwa mfano kama *CECAFA* ndani ya Afrika, lakini pia tumeshawahi kutoa wachezaji wetu kwa mfano kama riadha kushiriki mashindano ya Kimataifa.Hili nikwambie kwamba nakuahidi kwamba tutaweka mpango maalum tukishirikiana na Serikali ili tuandae vijana wetu na timu zetu kushiriki katika michezo ya Kimataifa.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi kukushukuru na niwashukuru ndugu zetu wa Yanga kwa kupata nafasi ya kutuwakilisha, na leo usiku inapangwa *draw* ya makundi tumuombe Mwenyezi Mungu wasije wakawa washindi wa mwisho kwenye kundi lao. Baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa nimuulize Mhe. Waziri swali langu.

Waziri alisema kwamba kama ilivyo kwa Tanzania Bara tunaona na sisi Zanzibar hakuna haja ya kuwa na kocha wa kigeni, lakini kwa hiyo hiyo Tanzania Bara Kocha mkuu wa *Taifa Stars* analipwa mshahara kati ya milioni 18 mpaka 24 kwa mwezi na ana mkataba.

Je, kwa Zanzibar makocha wetu wanao mkataba, na kama wanao kwa hivi sasa wanalipwa kiasi gani ili kuondoa dhana kwamba kwenda Rwanda kocha mkuu anakwenda na champali na mambo mengine. Je, tumejiandaa vipi katika masuala haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ni kweli naungana na yeye na nathibitisha kwamba makocha wa Tanzania Bara wana mikataba, na wanalipwa kwa mujibu wa makubaliano na kile Chama cha Michezo cha Tanzania Bara.

Napenda nimhakikishie kwamba na sisi kwa upande wa Zanzibar pia makocha wetu tumejiandaa kuwafanyia hivyo na tutahakikisha kwamba mikataba yao

itaendelea na kuwalipa hii mishahara kwa ajili ya kuendeleza timu zetu za Taifa za Zanzibar.

Nam. 17

Wananchi wa Bungi Kupatiwa Mashine ya Maji

Mhe. Simai Mohamed Said – Aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wanaoishi maeneo ya Bungi wanategemea maji kutoka mashine ya maji ya Kibele.

Ni lini watakabidhiwa mashine ili wananchi wa Bungi wapate maji ya kutosha.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: - Alijibu:-

Mhe Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 17 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, maeneo ya Bungi ni miongoni mwa vijiji vilivyopata huduma ya maji safi na Salama kupitia kisima cha maji Kibele. Mradi umekuwa ukifanya kazi vizuri kwa muda wote tokea kuanza kazi kwake, hata hivyo kutokana na ongezeko la mahitaji linachochangiwa pia na ongezeko la watu linalopelekea pia ujenzi wa makaazi mapya, baadhi ya maeneo hususan yale ya mbali na vijiji vipya ambavyo havikuweko wakati wa ujenzi wa mradi huduma ya maji safi na salama imekuwa haipatikani vizuri.

Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji tayari inaendelea na juhudi za kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo kwa kuchimba kisima katika eneo la Bungi Pangoni kupitia mradi wa uchimbaji wa visima ambao unafadhiliwa na Mtawala wa Ras-al-Kheimah. Kukamilika kwa mradi huo kutaweza kutatua tatizo linalowakabili wananchi wa maeneo ya Bungi pamoja na maeneo jirani. Hivyo Wizara yangu inamuomba Mhe. Mwakilishi na wananchi wa maeneo hayo na maeneo jirani kuwa wastahamilivu wakati jitihada za kulipatia ufumbuzi wa tatizo hilo zinaendelea.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nimpongeze na yeye muda mchache ameanza kuwa mtaalamu kwa majibu mazuri, lakini naomba niulize swali moja la nyongeza.

Eneo la Bungi ni eneo la kihistoria na makaazi kweli watu wameanza kuongezeka, lakini taarifa nilizokuwa nazo ni kwamba mashine ya pale ni ndogo Mhe. Naibu Waziri, lakini pia hakuna tangi la kutosha la kuweza kuhifadhia maji, lakini tatizo hili ni sugu katika maeneo mengi ya Jimboni kwangu jimbo la Tunguu eneo la Kaebona Unguja Ukuu, pamoja na Dunga.

Mhe. Naibu Waziri utakuweko tayari nikikufuata twende bega kwa bega, mkono kwa mkono kuweza kunitembelea maeneo yote jimboni kwangu ili tuweze kuondoa tatizo hili sugu la maji linalowakabili wananchi wangu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, naomba kumwambia Mhe. Simai kwamba niko tayari.*(Makofi)*

Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Tunatambua kwamba kisima kile kimechimbwa maeneo ya Kibele na tayari kimeshakuwa kinatumika kwa kutoa huduma kwa jamaa zetu wa Bungi, lakini cha kusikitisha Mhe. Naibu Waziri mpaka leo wananchi wa Kibele hawafaidiki na kisima kile hali ya kuwa kisima kile kimechimbwa nyumbani kwao, lakini wanafaidika jamaa zao na jirani zao wa Bungi.

Je, Mhe. Waziri Serikali inatwambia nini au inawaambia nini wakaazi wa Kibele kutokana na fursa ile ambayo inapatikana kwao na kuwa hawafaidiki nayo?.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Kama kafuatilia vizuri katika jibu langu la msingi ni kwamba vijiji ambavyo vimekuja baada ya mradi ama vile vya mbali kutoka kwenye kisima ndio vinavyokabiliwa sasa na upatikanaji mdogo wa maji, katika kulitatua hili tayari kimechimbwa kisima Bungi Pangoni na vyengine viwili vinachimbwa njia ya Dunga kwa ajili ya kupeleka Ndijani na kusaidia Kibele, na kile cha Bungi Pangoni kwa ajili ya kusaidia Bungi, vikimalizika hivi tatizo la maji maeneo hayo hakuna kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa mwezi mtukufu wa Ramadhani umekaribia, na kwa kuwa uhaba wa maji unaendelea kuongezeka siku hadi siku katika maeneo mbali mbali. Je,

Wizara yake imejipangaje kuwasaidia wananchi kuwapelekea magari ya maji hasa mwezi mtukufu wa Ramadhani ili kuweza kuwapunguzia usumbufu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Wizara yangu inajua kwamba karibu tutakabiliwa na Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, na unaweza kushuhudia kwamba Mhe. Waziri hayupo hapa anakabiliana na tatizo hilo, tutoe wito kwa Wawakilishi wote kuwa tayari kushirikiana na Wizara kuhakikisha katika maeneo yetu tunafikisha maji, aidha yale ambayo yapo katika miundombinu yetu ama njia mbadala.

Nam. 4

Ujenzi wa Barabara ya Kwarara

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) – Aliuliza:

Barabara ya Kwarara Meli Tano Msikitini hadi Kwarara kwa Ngulangwa, barabara hiyo ni mbaya kiasi cha wananchi wa maeneo hayo wanapata tabu ya usafiri wa daladala pamoja na watu binafsi. Kwa kuwa wananchi wanaoishi maeneo haya wanasumbuka kwa usafiri.

Je, Wizara ina mpango gani wa ujenzi wa barabara hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele swali lake Nam.4 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla sijamjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 4 naomba kutoa maelezo machache kama ifuatavyo:-

Kwenye Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015/2020 imeorodhesha miradi ya barabara mbali mbali ambazo zimeahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami ndani ya kipindi cha miaka mitano ya Chama kuwa madarakani.

Miongoni mwa barabara hizo ni pamoja na mradi wa ujenzi wa barabara ya Fuoni – Kwarara (1km), Sharifumsa-Mwanyanya-Bububu Skuli (3.6km), Kijitoupele (Mashine ya maji) – Nyarugusu (2.5km). Miradi yote hiyo iko chini ya Halmashauri za Wilaya ya Magharibi "A" na Magharibi "B".

Baada ya maelezo hayo mafupi na kwa faida ya Waheshimiwa Wajumbe wenye Majimbo ya miradi hiyo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 4 kama ifuatavyo:-

Barabara ya Meli tano Msikitini hadi Kwarara kwa Ngurangwa ni sehemu ya barabara ya Fuoni-Kwarara ambayo imetajwa kwenye Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ambayo itajengwa kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

Pamoja na kwamba barabara hiyo iko chini ya usimamizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi "B", Wizara yangu ilishawahi kuifanyia matengenezo makubwa sehemu ya barabara hiyo kwa kiwango cha kifusi kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

Kwa mpango huo huo, napenda kumuahidi Mhe. Mjumbe kuwa ndani ya miaka mitano barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami tema kwa kutumia fedha za mradi wa mfuko wa barabara. Namuomba Mhe. Mjumbe aendelee kuwa na subra wakati Wizara yangu ikijipanga kwa kutekeleza ahadi mbali mbali za Ilani hiyo.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa jitihada yake ya kuhakikisha anatafuta kero katika maeneo mbali mbali na mojawapo nikiri kwamba barabara ya kutoka Meli tano kuelekea Kwarara ni barabara ambayo mbaya, kiasi kwamba wananchi wetu wanaoishi katika maeneo hayo hukosa usafiri siku hadi siku.

Kwa kuwa juhudi ya mara ya kwanza ambayo imefanywa kuziba kifusi yenye kushirikisha Mbunge na Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele tunashukuru hilo tumelipata, lakini kulikuwa na sehemu moja mbaya zaidi inaitwa Madina. Mheshimiwa hakuweza kufika kwa gari yake, nimhakikishie tu kwamba sasa hivi tumepiga *grader* gari yoyote inakwenda hata *saloon* haina tatizo.

Swali langu je, Mhe. Waziri kuna mpango gani wa kutusaidia kifusi maana miaka mitano mingi kungojea lami, na wananchi wanaathirika hadi leo, kutia kifusi ili daladala zifike kule Madina na wao wasitirike na shida na watoto wao kila siku.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi nampongeza sana kwa juhudi anazozichukua yeye katika kuhakikisha kwamba anatatua kero mbali mbali zilizopo katika jimbo lake.

Kusema la kweli sio yeye peke yake nawapongeza Wawakilishi wote humu, kwani wameonesha ari kubwa sana kutaka kuwaletea maendeleo wananchi wao kwa kipindi kifupi. Hakika wametuonesha ari kubwa sana, na hakika sisi tuna dhima kubwa ya kuhakikisha kwamba matatizo yao tunayatatua kila hali inavyoruhusu. Kwa hiyo, napenda kumuahidi kwamba katika kuweka kifusi kwenye barabara hiyo huo ni wajibu wetu, na vile vile kuangalia kwamba barabara zote ambazo tushaanza kuzijenga japo kwa njia ya kifusi tunazifanyia *route* na kuzirekebisha zile sehemu korofi ili zile barabara zipitike wakati wowote.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa katika jimbo langu kuna barabara ya kilomita 4.3 kutoka Konde kwenda Msuka ambapo kuna kituo kikubwa cha KMKM na wakaazi wasiopungua 4000, na sababu barabara hiyo tulipata ufadhili kutoka Serikali ya Japan kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu tuliweza kuijenga kwa kiwango cha kifusi mwaka 2013. Kwa kuwa mvua zinazoendelea kunyesha zinaiharibu barabara hiyo siku hadi siku, kuna dalili kwamba barabara hiyo itarudia kule tulikotoka.

Je, serikali ina mpango gani wa kuikarabati barabara hiyo kuirudishia kwenye uhalisia wake na kuthamini zile nguvu za wahisani walizotusaidia ili tusionekane kama tumezipoteza bure. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa swali sio swali la msingi, sasa kama Mhe. Waziri unaweza kujibu ujibu, kama huwezi basi swali hilo lije kama swali la msingi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, ni kweli tumetembelea maeneo mengi na tukaona kwamba barabara nyingi sasa hivi zimejengwa kwa kiwango cha kifusi na nyengine zimeshaanza kuharibika. Sisi kama wizara pale ambapo tutapata fedha tutahakikisha kwamba zile sehemu ambazo korofi zimeharibika, kama nilivyosema katika swali la nyongeza la Mhe. Ali Suleiman (Shihata) tutahakikisha kwamba tunazirekebisha.

Vile vile kuna barabara nyingi sasa hivi kama nilivyosema zimeshafika mpaka kuwekwa kifusi kama vile za *MIVARF*, lakini tunasema kwamba iwapo uwezo utakuwepo basi angalau tutaanza kwa kuzitia lami ya maji ili baadae hizi barabara zisiharibike na tukapata gharama zaidi ya kuzitengeneza.

Nam. 53

Ajira za Wahitimu Chuo cha Kilimo Kizimbani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Wahitimu 93 katika Chuo cha Kilimo Kizimbani walimaliza masomo yao ya stashahada na cheti mwaka 2015.

(a) Kwa kuwa sekta ya kilimo na ufugaji inakabiliwa na changamoto kubwa ya upungufu wa wataalamu, hatua gani zimechukuliwa za kuajiri vijana hao haraka na kuondoa kero za wataalamu. Mpaka sasa ni wataalamu wangapi wamepewa ajira serikalini.

b) Kwa kuwa sekta ya kilimo na ufugaji soko la mahitaji ya mazao yake limekuwa kubwa tangu kuimarika kwa sekta ya utalii, serikali ina mpango gani wa kuongeza wataalamu zaidi baada ya wataalamu 93 kuhitimu kwa mwaka.

c) Je, ni wataalamu wangapi wanahitajika wa kilimo na mifugo kwa Zanzibar ili kuondoa tatizo la uhaba katika sekta hiyo ili wakulima na wafugaji waweze kupata huduma katika kiwango kinachokubalika kimataifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 53 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kupitia Chuo cha Kilimo Kizimbani kina jukumu la kutoa mafunzo katika fani za kilimo, mifugo na maliasili kwa vijana wanaomaliza skuli (Kidato cha Nne au cha Sita), ili waweze kujiajiri wenyewe baada ya kuhitimu kwenye masuala ya kilimo na ufugaji au kupata ajira serikalini.

Kwa mwaka 2014/2015 jumla ya wataalamu 21 ndio walioajiriwa kati ya hao 93. Wizara pia imeajiri wataalamu wengine 5 (3 madaktari na 2 wataalamu wa

maabara) katika jitihada za kupunguza uhaba wa wataalamu. Hata hivyo masuala ya ajira kwa kawaida yanasimamiwa na Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, serikali inaendelea na jitihada za kuongeza idadi ya wataalamu mbali ya hao 93. Mwaka wa masomo 2014/2015 chuo kina jumla ya wanafunzi 197, wanawake 125 na wanaume 72 ambao wamegawanyika katika kada zifuatazo; Stashahada ya Kilimo 52 (wanawake 28 na wanaume 24), Stashahada ya mazao 14 (wanawake 9 na wanaume 5) na wenye cheti 131 (wanawake 88 na wanaume 43). Mafunzo katika kada zote yanajumuisha mbinu na vifaa vya kisasa na kiasili kwa lengo la kuwaandaa wanafunzi kuweza kufanya kazi katika sekta ya kilimo na ufugaji.

Mhe. Naibu Spika, mbali na juhudi hizo zinazochukuliwa, wizara pia inashirikiana na taasisi binafsi na *NGO's* katika kuhamasisha na kushajiisha wakulima, kuzalisha mazao ya mboga na matunda kwa lengo la kufikia soko la kitalii linalokuwa kwa kasi. Hivi karibuni wizara imekuwa ikishirikiana na taasisi za *Tanzania Horticultural Association* (*TAHA*), *TAP*, Kampuni inayojihusisha zaidi na usambazaji wa vifaa vya kilimo, Umoja wa Wazalishaji wa Mboga Wilaya ya Magharibi (UWAMWIMA) na nyenginezo katika kuhakikisha tunaongeza ajira na kipato cha wakulima. Wataalamu wa taasisi hizo wamekuwa ni chachu ya ongezeko la mazao ya mboga na ajira hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, katika kila shehia tunahitaji mabwana au mabibi shamba mmoja, hapa Zanzibar tuna shehia 384, ukitoa shehia 55 za Mjini, 200 Unguja na 129 Pemba. Upungufu tulionao ni 65 kutoka Unguja na 85 kutoka Pemba.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana Mhe. Naibu Waziri kaniomba nizungumze kidogo kidogo, kwa hiyo naomba nijitahidi kuzungumza kidogo kidogo usije ukafikiria nasoma maandishi yangu Mhe. Naibu Spika.

a) Hatua ya kuajiri wahitimu 21 wakiwemo wataalamu 5 kati ya wataalamu 93. Je, serikali haioni kuwa inafanya masihara, haiendi na wakati na ukizingatia hotuba ya Mhe. Rais aliyokuja kutuletea ukurasa wa 29 kuhusu Chuo cha Kilimo Kizimbani kitaimarisha ili kuongeza idadi ya wataalamu wa kilimo. Huoni Mhe. Naibu Waziri unaifanyia masihara au sijui nitumie lugha gani hotuba ya Mhe. Rais ambaye ni kiongozi wetu.

b) Wakulima ili waweze kupata huduma ya kilimo bora na waende na wakati ni wataalamu wangapi wanahitajika Zanzibar kwa muda huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Kizimbani kinatoa taaluma ili vijana waweze kujiajiri, na wanaochukuliwa ni wale ambao labda ni wachache na wale ambao wanaoachwa si kama hawa-*qualify* bali serikali haiwezi ikawachukua wanafunzi wote kwa kuwapa ajira.

Kwa kumsaidia Mhe. Mwakilishi tungesaidiana Wawakilishi wote na zaidi wale wa majimbo hawa vijana wetu ambao wamekamilisha ile elimu yao pale Chuo cha Kizimbani, basi wangekusanywa wakawekwa ma-*group* kwa ajili ya kuwawezesha na kuweza kuwaendeleza kimaisha.

Mhe. Naibu Spika, pia ninavyohisi mimi swali lake la (b) alivyoliuliza tayari nimeshalitolea maelezo, kuhusu upungufu wa mabwana au mabibi shamba wangapi wanahitajika. Sasa sijui kama hajanielewa au labda nirudie tena.

Mhe. Naibu Spika: Ametaka upungufu wa wataalamu tulionao ambao pengine labda tunatarajia.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, ndio hao niliomwambia upungufu tulionao wa wataalamu wa mabibi shamba na mabwana shamba, kwa sababu haja-*specify* upungufu wa watu gani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, swali la (b) ili Zanzibar tupige hatua ya kilimo tunahitaji wataalamu wangapi, na tuna upungufu wa wataalamu wangapi, Kiswahili kidogo tu hicho Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, ili Zanzibar tufikie tunahitaji wataalamu nimesema kila shehia mtaalamu mmoja anahitajika ili aweze kutoa taaluma kwa wale wenye mashamba ukitoa Mjini shehia 55.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, naomba kuongezea kwamba swali la Mhe. Mwakilishi ni kwamba anataka kujua ni wataalamu wangapi katika kila fani ya kilimo wanahitajika ili kuwa na utoshelezo Zanzibar.

Kwanza katika wizara ambayo imejitahidi sana kusomesha wataalamu ni Wizara ya Kilimo na Mifugo, cha kusikitisha Mhe. Naibu Spika asilimia 42 ya

wataalamu wetu wamechukua likizo bila ya malipo kwa hiyo tuna upungufu wa wataalamu wasiopungua asilimia 60 hivi sasa. Bahati nzuri baada ya Rais kuunganisha wizara wataalamu ambao tunaweza sasa tukachukua kutoka wizara zilizounganishwa na kuweza kuunganisha na wizara zetu.

Sasa katika *section* ya utafiti ambayo ndio *section* muhimu sana katika kilimo, tuna upungufu wa wataalamu wasiopungua 60 hivi sasa. Katika *section* ya utaalamu wa umwagiliaji maji tuna upungufu wa wataalamu wasiopungua 150. Kwa hiyo, tuna idadi kubwa kidogo ya wataalamu ambao wamepungua, na sio rahisi kumwambia sasa hivi ni kiasi gani cha wataalamu hasa watapatikana baada ya serikali kuunganisha hii wizara, tutakapofanya hivyo tutampatia takwimu kamili.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa wakulima na wafugaji wanahitaji sana wataalamu ili wakulima waweze kulima kilimo cha kisasa na wafugaji waweze kufuga ufugaji wa kisasa na wataalamu tulionao ni kidogo.

Je, serikali itafanya hatua gani za ziada ili kuhakikisha elimu hiyo ya wataalamu hao inawafikia wafugaji wetu na wakulima wetu ili waweze kupata tija katika ufugaji wao na kilimo chao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, ili tuweze kufikia malengo hayo ambayo aliyoyasema tunahitaji wataalamu jumla ya shehia kama nilivyosema kwa Unguja 200 na kwa Pemba 129, tukishakupata hawa mabibi shamba na mabwana shamba wao ndio watakaosaidia katika masuala ya kulima na ufugaji.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri, Wizara ya Afya ina utaratibu wa wahitimu wao wanapomaliza pale chuoni wanawapeleka mahospitalini kwa ajili ya kupata ajira na kufanya yale ambayo wameyasoma.

Je, wizara yako imepanga utaratibu gani juu ya wale wahitimu wanaomaliza vyuoni na kwenda kusaidia katika zile nafasi ambazo zinakosekana, na

wanaifanyia nini elimu yao kama hawapelekwi katika maeneo hayo na sisi tuna uhaba wa watu hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, naona kama haya maswali yanajirudia. Kama nilivyosema Wizara ya Kilimo inatoa taaluma na ikishakumaliza kusomesha inachukua baadhi yao, wale ambao wamebakia basi tusaidiane Waheshimiwa Wawakilishi ili tuweze kuwawezesha, na wale ambao tunawahitaji tunawachukua na wale ambao labda sisi kwa muda ule hatuwahitaji basi naomba tusaidiane tuweze kuwawezesha, ili ile elimu yao waiendeleze na wasikae tu nyumbani kuisahau.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, naomba niongezee majibu ya Mhe. Naibu Waziri. Ni kwamba wahitimu wote wanapomaliza mafunzo yao kama vile ambavyo wanafanya Wizara ya Afya na wizara nyengine kuna mafunzo yanaitwa *internship* huwa tunawapeleka vijana hao kupata mafunzo ya vitendo katika sehemu mbali mbali, ndani ya wizara na nje ya wizara yetu. Kwa hiyo, ni kweli alivyosema kabisa na ndio maana *programme* zetu kubwa za kilimo sasa hivi ni kuwafundisha watu waweze kwenda kuwahudumia kule walipo.

Kwa hivyo, suala la *internship* ni la lazima kabisa ndio maana pale Chuo cha Kizimbani utakuta tuna *section* ya mifugo, ukimaliza kusoma pale wanaendelea kufanya kazi pale halafu huwapeleka pahala pengine. Kama hivi karibuni mulikuta kuna wanafunzi fulani tuliwa-*train* tukawapa na baiskeli, wakajiunga wenyewe na wakaenda kuzalisha na kukaa, kazi yao kubwa ni kwenda kusaidia *communities* kule kijijini baada ya kupata ile taaluma, na wizara inaendelea kuwasaidia na sasa hivi tuna *programme* na *FAO* kuhakikisha wale vijana wetu wote waliopata *training* wanaeneza taaluma hiyo kwa wananchi vijijini. Nakushukuru sana kwa swali lako Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, baada ya kumaliza maswali mimi nitaondoka hapa na nitamkabidhi Mwenyekiti wa Baraza Mhe. Shehe Hamad Mattar atakuja kuendelea na majadiliano.Kwa hiyo, niwashukuru sana kwa mashirikiano yenu lakini kabla ya kuondoka nitasoma matangazo mawili.

Kuna wageni wetu ambao ni wa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy, wageni hao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi Jimbo la Chaani, naomba wasimame kama wapo. Jumla yao ni 20 na wanaongozwa na Ndugu Twaha Hija Khamis, Diwani wa Chaani pamoja na Ndugu Haji Kidawa Mkali, Diwani wa Kinyasini. Ahsanteni, naomba mkae. (*Makofi*)

Wageni wengine ni wa Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) Mwakilishi wa Kijitoupele ambaye ni Ndugu Saleh Yahya Saleh, Diwani wa Kijitoupele. Ahsante tunakushukuru karibu sana.

Wageni wengine ni wa Mhe. Moudline Cyrus Castico, Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ambao ni wanafunzi wa Skuli ya Francis Maria ya Tomondo. Jumla yao ni 10 naomba msimame na wanaongozwa na Mwalimu wao Suleiman Amour na Mwalimu Faynes Kasote, karibuni sana.

Wageni wetu wa mwisho ni wageni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi wa Skuli ya Bambi Jimbo la Uzini, ni viongozi wa serikali ya wanafunzi wa skuli hiyo jumla yao ni 39 naomba msimame kama mpo, karibuni sana; wanaongozwa na msaidizi Mwalimu Mkuu Ndugu Hamdu Zubeir, karibu sana.

Tangazo jengine linatoka kwa Mwenyekiti wa UWAWAZA ni kwamba leo baada ya kumaliza kikao wanaombwa Wajumbe wote wa UWAWAZA wafike katika ukumbi wa juu kwa ajili ya uchaguzi.

Waheshimiwa nawashukuru sana natarajia kwamba mtatoa mashirikiano mazuri kwa Mwenyekiti wa Baraza.

(Hapa Mhe. Shehe Hamad Mattar, Mwenyekiti alikalia kiti)

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Mwaka 2016/2017

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) aliyenipa uhai na kuniwezesha kuingia katika Baraza lako hili tukufu asubuhi ya leo. Pia nikushukuru wewe Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ya kuichangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar kwa ushindi mkubwa alioupata wakati wa uchaguzi, ushindi ambao umeweka historia kwa Zanzibar.

Nimpongeze Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa ushindi mkubwa alioupata jimboni kwake na pia kupata uteuzi wa Rais kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Pia niwapongeze wote wale waliopata uteuzi wa Mhe. Rais, tunao humu na wale wote waliochaguliwa majimboni mwao kwa kura za kutosha kabisa.

Niwashukuru wananchi wa Jimbo la Wingwi ambao ndio walinifikisha katika Baraza hili tukufu, lakini pia niwashukuru wake zangu ambao walinipa utulivu na uhuru mkubwa wakati wa heka heka za safari ya kuja huku.

Pia niwaombee wazazi wangu waliotangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema peponi, Mwenyezi Mungu awabadilishie yale mabaya yao yawe ndio mema yao na waingie peponi mtu na mke wake.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo niingie moja kwa moja kwenye hotuba, nianze na uchumi. Nianze basi kwa kuishukuru na kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jinsi ilivyofanya kazi mpaka ikafikia kuukuza uchumi ukawa katika hali ya matumaini. Lakini uchumi huu haukujipandisha tu, huo uchumi uliopanda haukujipandisha ulipandishwa. Kwa hivyo, sina budi niwapongeze wakulima, wavuvi na wafanyabiashara wa Zanzibar ambao kwa kiasi kikubwa ndio waliochangia kupanda kwa uchumi wetu wa Zanzibar.

Mimi naamini kwamba wananchi wa Zanzibar wanaipenda serikali yao, wanawapenda viongozi wao, wanawapenda ndugu zao labda patokee waharibifu ndani yake. Lakini hata wakitokea waharibifu ni kama waliokwenda kuharibu maji kisimani, maji yakiharibiwa si baadae yanatulia, naamini kwamba wananchi wa Zanzibar pamoja na kuharibiwa kwao bado wataiunga mkono Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Endapo kasi kubwa ya uharibifu kama ambavyo inatokea sasa hivi Pemba, watu kupita nyumba hadi nyumba kutakiwa wananchi waikane serikali, wawakane wawakilishi, pia Wazanzibari hawaipokei, lakini kama wameipokea sisi humu ndio tutakaokuwa watengezaji. Kama hiyo wataipokea Wazanzibari kukanusha wawakilishi wao watakaowaletea maendeleo yao, kukanusha serikali yao itakayowaletea maendeleo yao, sisi tuliomo humu ndio ambao tutatengeza tutawatengeza wao, sisi tukitoka humu kazi yetu kubwa ni kuwatengeneza wao baada ya kuharibiwa.

Mhe. Rais wakati wa kampeni alikuwa kila mgombea anamwita pale alipo na anamkamata mkono anawauliza watu mnamjua huyu? Huyu ni fulani bin fulani

bin fulani, huyu namuombea kura. Kila Mwakilishi hapa aliombewa kura na Mhe. Rais na wananchi wakamkubali Mhe. Rais wakatupa kura sote.

Mhe. Rais hakutuombea kura bure, alituombea kura kwamba tuje tumsaidie kazi yake, kama kuna majipu anayetumbuliwa majipu hakubali ati hatulii lazima akamatwe, sasa sisi ndio wakamataji halafu yeye ndiye mtumbuaji.

Kwa hivyo, wananchi wetu tujue kwamba wako pamoja na sisi, na kwamba wanaharibiwa lakini sisi tukitoka hapa twende tukawatengeneze. Sasa kutokana na hali ya uchumi wetu hali hiyo ambayo inawawezesha wananchi kuweza kuwapa matumaini ya shughuli zao basi tunamuomba Mhe. Waziri awatupie macho wakulima, wavuvi pamoja na wafanyabiashara popote Unguja na Pemba sio sehemu moja, kwamba hawa wote ndio waliochangia na wao wanataka kuyapata matunda yao baada ya kuelewa uchumi ulikuwaje na sasa ukoje, je wao wakoje.

Mtoto anaposikia kuwa mikarafuu yao imezaa anafurahi sana na anajenga matumaini na anaweza akawa anasema peke yake ah! mimi nilikuwa sina nguo ya skuli, nguo yangu maraka maraka matupu, sina sare lakini nategemea kuwa baba baada ya kuvuna karafuu ataninunulia sare mpya na huenda akaninunulia baskeli na anakuwa karibu karibu pale. Kwa hivyo, na Wazanzibari sasa hivi wako karibu nasi, wanaangalia vipi tutawajali, jinsi walivyochangia kwa kukuza pato la nchi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninatoka Jimbo la Wingwi, wananchi wa Wingwi wanaishi kwa kutegemea kilimo, uvuvi na biashara. Kilimo ni uti wa mgongo wa Zanzibar, kilimo hakikanushwi na anayekanusha kilimo kimo katika *rank* yake ile, tunaona wengi walihama mashamba kuhamia mjini kwa ajili ya kukimbia kilimo na wengi walikuwa wanasema mimi siwezi nishachoka kulima nakwenda mjini, lakini sasa yaani waliisahau ile kauli ya Mwenyezi Mungu aliyosema kwamba, "*Mkimaliza kusali tembeeni katika ardhi, mchawanyike katika ardhi mkatafute fadhila za Mwenyezi Mungu*". Sasa fadhila za Mwenyezi Mungu ni zipi katika ardhi kama si kilimo. Wataalamu wanasema kwamba, kama yatagawanywa mafungu kumi ya riziki, mafungu tisa yanatokana na kilimo na biashara.

Kwa hiyo, mambo haya yatabakia katika *rank* yake, sasa wale waliohama mashamba kwenda mjini kwa ajili ya kukimbia kilimo hii aya inafanya kazi kule. Leo utatoka wewe shamba kwenda kumuangalia jamaa yako mjini, ukaenda kule saa nne kwa mfano umefika hayupo, kwa hivyo rejea nyumbani nenda saa kumi ukifika hayupo, haya vipi huyu? Ah, yuko kondeni hapa haingii

mpaka saa 12 za jioni, akimaliza kusali tu anakwenda huko. Hiyo ni ile ile aya ilivyosema ndio hivyo hivyo, hatuwezi tukaishi bila kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu au wakulima wetu wanafanya kazi kubwa ya kulima wanapoteza muda mrefu kwa kulima, wanatumia fedha nyingi kwa kulima, lakini kwa leo kilimo hakiwapi tija kutokana na changamoto zilizowakabili.

Changamoto ya kwanza ni ukosefu wa wataalamu. Watu wanalima tu kwa mazoea kwamba mimi najua kulima na kupanda wakati ule mmea unaota kisayansi. Sasa kama ule mmea unaota kisayansi lazima pawe na taaluma ya kuweza kupata matunda.

Hakuna lolote Mhe. Mwenyekiti, ambalo litakuwa bila ya taaluma hata kulala usingizi, usingizi unakuja tu *automatically* hata juu unalala, hata baharini unalala, lakini bado unahitaji taaluma na kama utalala bila ya taaluma ukifumba jicho tu tayari jinamizi hilo, ukifumba jicho unamuona mtu anakuangusha kisimani ndio, unataka taaluma. Kwa hivyo, na ukulima ndio zaidi unaotaka taaluma, na changamoto ya kwanza inayowakumba wakulima ni kukosa taaluma. Hivyo, tunamuomba waziri husika atupelekee wataalamu wa kilimo ili tuweze kupata kilimo chenye tija.

Changamoto ya pili ardhi ni ndogo, ardhi yetu ni ile ile lakini sisi tunaongezeka na tutazidi kuongezeka. Kwa sababu kila anayekuja anakuja na ari mpya wakati huo huo bahari imeshaivamia ardhi. Kwa hivyo, ile ile ardhi na ongezeko la watu kuna ziada ya uvamizi wa bahari. Tunamuomba Mhe. Waziri atupelekee wataalamu ambao watatafuta namna ya kukinga bahari ili isiathiri vilimo vya wakulima.

Changamoto nyengine ni pembejeo. Pembejeo hazipatikani kwa wakati muafaka. Kwa hivyo, tunamuomba sana Waziri wa Fedha na Mipango achangie kasma fulani kwa ajili ya wakulima na kuwapelekea pembejeo ili waweze kuridhika na wao kwa uchumi wao ambao umekua na wao ndio wahusika.

Mhe. Mwenyekiti, Jimbo langu la Wingwi lina shehia tano; Shehia ya Sizini ambako ndiko niliko mimi, Shehia ya Mjini Wingwi karibu ya Micheweni, Shehia ya Mapofu, Shehia ya Njuguni na Shehia ya Mtemani Wingwi. Shehia zote hizo ziko karibu na pwani, kwa hivyo ndani yake miongoni mwa watu wa Wingwi ni wakulima na wavuvi, lakini sasa, wavuvi waliiacha sekta ya uvuvi

wakakimbilia kwenye zao la mwani wala sio Wingwi tu hata Tumbe, Tumbe ndio kwenye bandari kuu.

Pemba ziko bandari nyingi lakini bandari hasa inayopendwa ni Tumbe, na Tumbe ndiko kulikojengwa soko la samaki, soko kubwa tu, tunaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutujengea soko la samaki Tumbe. Soko la aina yake, soko limewekwa pahala ndipo. Lakini sasa wavuvi wameacha uvuvi kwa zao la mwani.

Sasa kuingia kwenye zao la mwani mwani ukaanguka bei sasa hawako kokote, hawako huku wala hawako huku. Kwa hivyo, serikali yao tunaomba iwatulizanishe, ima iwapelekee vyombo vya uhakika ambavyo vitawawezesha kufika bahari kuu kwa sababu samaki tunao wengi tu, lakini wavuvi wanabakia humu humu karibu karibu na mikandaa hawana uwezo wa kwenda kwenye bahari kuu na tunao mahodari tu, lakini wanahitaji vyombo vya usafiri, vyombo vya kuvulia ambavyo vitafika huko waliko samaki. Kwa Kufanya hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ndio serikali italifikia lile lengo la kuweka lile soko kule Tumbe, ikiwa wavuvi watakwenda watapata vyombo waende wakapate samaki watauza samaki na serikali itapata pato, na wananchi watafaidika katika maisha yao.

Namuomba sana Mhe. Waziri awaweke pahala maalum hawa watu, kwamba hawako huku wala huku hilo la kwanza.

Pili ili awatulizanishe ningeomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hili zao la mwani ikawa liko mikononi mwa serikali. Tunajua kwamba makampuni mengi tu yalikuja, wawekezaji wengi walikuja, wengi majajiri walitaka hata karafuu ibinafsishwe. Lakini kwa kuwa serikali inaona mbali ilijua tukiibinafsisha hii watadhalilika Wazanzibari, ingawaje wenyewe walikuwa wakipenda hivyo wanunue tu watu binafsi. Lakini walikuwa hawajui mbele kuna nini. Sasa tuangalie hapa mwani, watu wameshatoka kwenye uvuvi wanaingia kwenye mwani, sasa itabidi warudie kule kule. Mimi nadhani kwamba haya makampuni yanayokuja yanakuja kuwababaisha tu hawa wakulima wetu au wavuvi hapa.

Kwa hivyo, ningeomba mimi serikali ichukue hatua ya kununua mwani wa Zanzibar. Kwa sababu mwani ikiwa ni biashara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakapopanda bei katika masoko ya nje Mhe. Waziri atawaeleza wananchi, itakaposhuka bei masoko ya nje Mhe. Waziri atawaeleza wananchi wataelewa, lakini leo wanakwenda tu hawajui kupanda wala kushuka na wao hawako huku wala hawako huku.

Kwa hivyo, ningeshauri ima Mhe. Waziri awapatie maboti wavuvi warejee baharini, au wadhibiti mwani na wanunue mwani iwe ni biashara endelevu ili wajue pa kwendea.

Nije katika sekta ya Afya. Mhe. Mwenyekiti, ili tupate taifa la uzalishaji mali lazima tupate taifa lenye nguvu na afya. Mimi niishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuweza kueneza vituo vya afya kila kona Zanzibar. Hii neema kubwa lazima tuishukuru, ukikishukuru kidogo Mwenyezi Mungu atakupa kikubwa, lakini ukikanusha kikubwa na hicho kidogo Mwenyezi Mungu hakupi, kile kitapotea na hicho kidogo hakupi.

Kwa hivyo, sina budi niishukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kueneza vituo vya afya kila pembe, kila kona ya Zanzibar. Lengo la serikali ni kuona kwamba vituo vya afya vinawahudumikia wagonjwa, hilo ndilo lengo lake. Sasa tulifikie lengo la serikali, ndio maana inatawanya vituo vya afya, wasi wasi wangu ni kuwa kujageuka misikiti.

Mhe. Mwenyekiti, kila hatua ishirini Zanzibar kuna msikiti, tunamshukuru Mwenyezi Mungu tumebarikiwa, kila hatua ishirini huu msikiti. Lakini kila msikiti una ugomvi, sasa wale wajengaji wa msikiti halikufikia lile lengo. Kwa hivyo, twende kulingana na malengo ya serikali kwa vituo vyetu vya afya, na vipi kufikia malengo lazima litangulie jambo moja wasemaji walisema "*Jambo haliwa, likitiwa msimamizi na majaliwa*" ufuatiliaji hilo ndilo jambo.

Wafanyakazi hawamuogopi muajiri lakini wanamuogopa mkaguzi, kama atakwenda kiongozi yoyote wa juu atapita skuli walimu bado watakuwa hawana wasi wasi wanaendelea na shughuli zao. Lakini akija mkaguzi tu kila mmoja wahaka, wakaguzi ndio ambao wanaoleta ufanisi wa kazi yoyote iliyopo. Ufuatiliaji unapokosekana malengo ya serikali yote yanaanguka. Lakini unapofatilia utajua kwamba kituo cha afya cha Sizini kilianguka.

Mhe. Mwenyekiti, huo si mfano katika Shehia ya Sizini hakuna kituo cha afya hasa kama kuna ufatiliaji angekuwa keshajua Mhe. Waziri muhusika kwamba Sizini hakuna kituo cha afya, na Sizini pia kuna wagonjwa wanahitaji kutibiwa.

Kituo cha afya cha Sizini kilianguka wakalazimika wahusika haraka haraka wakahamisha mizigo yao mule wakaenda wakaazima nyumba ambayo haina sifa, kwa sababu ikiwa watakuja wakandarasi au wajengaji wa hospitali au wa kituo cha afya watakuwa wana mpango maalum, wana jengo maalum, wana vipimo maalum; hapa pa daktari, hapa pa kukaa watu wanaosubiri nafasi zao, hapa pa kupimia. Lakini nyumba ya kuazima haina sifa na huu ni mwaka wa

tatu wananchi wa Shehia ya Sizini hawana kituo cha afya. Ingawa wanapata huduma lakini kituo ambacho hakina sifa, na pia ni nyumba ya mtu na mwenyewe keshaitaka. Namuomba sana Mhe. Waziri muhusika kutokana na uchumi wetu aingize jengo hili la kituo cha afya cha Sizini ili na sisi tufaidike na uchumi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 21 katika kifungu cha 51 kuna maelezo yafuatayo naomba kwa ruhusa yako ninukuu:-

"Kutokana na muelekeo wa hali ya fedha, sera kuu ya matumizi inahitaji kubana zaidi matumizi kulingana na vyanzo vya mapato viliopo. Kutokana na muelekeo huo mkazo katika matumizi utalenga katika mambo yafuatayo".

(ii) Kuendeleza jitihada za uimarishaji wa huduma za jamii hasa elimu, afya na upatikanaji wa maji safi na salama. Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Mwenyekiti, ...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa angalia muda, jitayarishe muda wako unakaribia kumalizika.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante, tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuweza kutuenezea maji mijini na mashamba. Tumbe kiko kisima cha maji lakini si maji safi. Hilo kama watendaji hawaelewi ndio nawajulisha.

Hapa Tumbe yako maji ya kutosha lakini kisima cha maji kilioko Tumbe kina maji hayaeleweki, maana yake maji mekundu, mara buluu mara manjano. Sasa hayaeleweki vipi hii rangi hii ni nini. Kwa maana hiyo watu wa Tumbe wanayatumia maji hayo kwa mambo mawili tu kupikia na kukogea basi hawatumii kwa kunywa kutokana na maji yalivyo.

Kwa hivyo, tunaomba Mheshimiwa muhusika aende Tumbe akafanye utafiti haya maji yanatoka wapi na yana nini, ili awape amani wananchi wa Tumbe waweze kutumia maji yao kama hayadhuru waweze kuyatumia, kama yana madhara patafutwe kisima chengine.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa umenikumbusha muda basi na mimi niungane na wenzangu kwamba niunge mkono hotuba hii ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante kwa michango yako na kuzingatia muda.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi na mimi asubuhi hii kuweza kuchangia katika hotuba hii ya mpango wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu kwa kunijaalia afya njema asubuhi ya leo nikaweza kusimama hapa, nikaweza kutoa mchango wangu ambao ninaamini ndio utasaidia katika muelekeo wa bajeti yetu kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu wa Zanzibar waliotuchagua kwamba tuje tuwe watetezi wao katika Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii pia kumpongeza kwa dhati Spika wetu kwa ushindi mkubwa alioupata tulipomchagua pale Afisi Kuu ya CCM Kisiwandui na tukaja kumthibitisha hapa.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kusema kwamba sisi Wawakilishi hatukufanya makosa kumchagua Mhe. Zubeir Ali Maulid kuwa Spika wetu, kwa sababu vigezo vya kutuongoza anavyo. (*Makofi*)

Pia napenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa ushindi mkubwa alioupata wakati wa uchaguzi wa marudio wa Machi 20 mwaka huu 2016.

Ushindi wake huo Mhe. Rais ni imani ya Wazanzibari walionayo juu yake kutokana na utendaji wake wa miaka mitano iliyotangulia. Ni wajibu wetu sisi sote tuliomo humu kumuombea Mwenyezi Mungu ampe hekima, busara na uwezo ili aweze kuliongoza taifa letu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Ni matumaini yangu kwamba sisi Wawakilishi tuliochaguliwa kutoka kwa wananchi na wale Wawakilishi waliopata uteuzi wa viti maalum tutashirikiana naye Mhe. Rais kikamilifu ili kuhakikisha kwamba dhamira ya Rais ya kuleta mabadiliko ya kiuchumi ndani ya kipindi hichi yanatimia, Mwenyezi Mungu ampe afya njema, hekima na busara. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza kwa dhati Makamu wa Pili wa Rais ambaye ndiye kiongozi wetu katika shughuli zetu za Baraza. Nachukua fursa hii kumpongeza kwa ushindi wake katika Jimbo lake la uchaguzi na pia kwa dhamana aliyopewa ya kuwa Mtendaji Mkuu wa Serikali.

Vile vile ni imani yetu kwamba weledi wake uwezo wake, busara yake na hekima yake aliyonayo katika kutekeleza majukumu yake ya kazi ndio dira yetu sisi humu katika Baraza hili. Tunamuomba Mwenyezi Mungu na yeye ampe afya njema. Amin. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mawaziri wote waliochaguliwa na Manaibu wao. Pongezi hizi nazitoa nikiamini kwamba uwezo wao wa utendaji ni mkubwa na mashirikiano yao ya karibu walioanza kutuonesha sisi Wawakilishi. Ni dhahiri kwamba umoja wetu ndio nguvu zetu, na ndio utakaotufanya tusonge mbele katika kulitumikia taifa kufikia malengo ya kukuza uchumi hadi ifikapo mwaka 2020. Kuwatoa watu wetu katika kipato cha chini kuwapeleka katika uchumi wa kati.

Mhe. Mwenyekiti, pongezi zangu za moja kwa moja ziende kwa Waziri wa Fedha. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Fedha kwa hotuba yake nzuri aliyotuwasilishia hapa Barazani yeye pamoja na watendaji wake hasa Katibu wake Mkuu, inaonekana ni mtu aliyebobea katika mambo haya.

Ni imani yetu kwamba viongozi wetu hawa wataweza kulivusha jahazi hili kwa salama na amani. Kwa hiyo natoa pongezi zao za dhati kwao.

Pia napenda nisiwasahau watumishi wa taasisi zinazokusanya kodi *ZRB* na *TRA* wanafanya kazi nzuri, kazi ya kupigiwa mfano, na tunawaomba waongeze bidii kwa sababu bila ya wao sisi hatupati kodi, na kodi ndio tunayohitaji kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Haiwezekani nchi yetu kwenda bila ya kodi, kodi ndio kila kitu ulimwenguni kote. (*Makofi*)

Pamoja na kutanguliza shukurani kwa Waziri wa Fedha na timu yake lakini pia napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa watendaji wa chini yao, viongozi hawa wa Mamlaka ya Mapato. Lakini pamoja na pongezi hizo ninapenda kuwakumbusha jambo moja kabla sijaingia kwenye mchango Mhe. Mwenyekiti, kwamba pamoja na kazi nzuri wanayoifanya maafisa hao, ni lazima wakumbuke na wajue kwamba wana jukumu lakini si kwa serikali tu na wananchi, pia kwa Mwenyezi Mungu. Wakumbuke kwamba wana dhima kubwa.

Tumewapa mzigo mzito wa kukusanya kodi ambao ni haki za Wazanzibari. Kwa hivyo wana jukumu la kufanya kazi kwa uaminifu na uadilifu ili kuondoa zile shutuma za baadhi ya watu kwamba maafisa wa kodi wanapoingia pale baada ya muda wanakuwa tayari wametengeneza wigo wa kujitayarisha. Sina

maana ya kuwasema kwa vibaya lakini ni tahadhari kwamba kipato na hasa fedha ni kitu kibaya kinachoweza kumbadilisha mtu mara moja, kikamtoa katika mwelekeo wake aliokuwa nao kikampeleka pahala kwengine. Hii Mhe. Mwenyekiti, ni kama nasaha kwangu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo baada ya kusema ningependa kidogo nichangie mambo kidogo kidogo yafuatayo. Kwa sababu mchango wetu mwingi tumeupeleka kwenye Kamatiya Wenyeviti. Ndiyo maana ukaona wenzangu wengi hawajasimama kuchangia kwa sababu sisi wenyeviti tulikusanya mawazo yetu na michango yetu tukaipeleka kwenye Kamati yetu ya Wenyeviti ambayo jana iliwasilishwa.

Pamoja na hayo Mhe. Mwenyekiti, kidogo mimi nitajipeleka moja kwa moja kwenye sehemu ijapokuwa dakika moja moja ya uwekezaji, utalii, mawasiliano, ardhi, kilimo, afya, elimu na mazingira na ikisha nitakuja kwenye mambo ya ulinzi hasa kwa Vikozi Maalum vya SMZ ambalo hili litakuwa ni ombi maalum.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu uwekezaji; mimi ninapenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, hasa kupitia katika Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi (*ZIPA*) ambayo kwa kweli taasisi hii inafanya kazi yake vizuri sana na kwa uledi mkubwa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mapungufu madogo madogo ya kibinadamu lakini hatuna budi kuwa wakweli kwamba Mamlaka ya Ukuzaji ya Vitega Uchumi inafanya kazi yake kwa uadilifu. Kwa sababu anapokwenda mwekezaji, Mamlaka inachukua jukumu la kumpima kwanza. Ingawa upande mwengine wawekezaji wanalalamika kwamba tunapoteza muda. Kweli muda ni mrefu kwa wawekezaji. Lakini pia isingekuwa busara hata kidogo kwa wawekezaji au kwa Mamlaka kukurupuka haraka kutoa vibali kwa wawekezaji bila ya kumfanyia utafiti wa kutaka kujiridhisha. Na kwa kweli kwa upande wangu mimi ninaona utaratibu wanaotumia watu wa *ZIPA* unaniridhisha. Ingawa wanatakiwa wapunguze muda kidogo kabla ya kutoa vibali, waharakishe muda. Lakini ni vizuri kujiridhisha kabla ya kutoa vibali. Kwa sababu gani Mhe. Mwenyekiti.

Ninazungumza hivi kwa sababu unapompa mtu *lease* unamilikishwa mwekezaji kwa muda wa miaka 33, ina-*extend* mara tatu kwa muda itakuwa miaka 99. Sasa kama bila ya kufanya utafiti wa kina ukataka kujua *business plan* yake na ukataka kujua na mambo yote, ukampa kibali kwa siku mbili kwa nchi ya kisiwa kama chetu, umeshammilikisha ardhi. Kesho asubuhi yule

bwana anatafuta kazi nyengine ya kufanya, ardhi aliyopewa na mamlaka anaiwacha. Kwa kweli tutakuwa hatujawatendea haki Wazanzibari kwenye ardhi yao hiyo. Kwa sababu lengo la serikali la kutoa ardhi ile ilikuwa ni kwa ajili ya maendeleo ya Wazanzibari.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa upande wangu na matumaini yangu kwamba Idara hii ya Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi kutoa vibali kwa wawekezaji kwa ajili ya kuendeleza mradi wa *Fumba Satellite City*, mradi wa kuendeleza wa mji wa kisasa wa Fumba na mradi wa ujenzi wa maeneo ya kupumzikia *(Fumba Uptown Living).* Miradi hii ni sahihi na kwamba ina mwelekeo mkubwa wa kutoa ajira kwa vijana. Jambo ambalo ni kilio kikubwa kwa vijana wetu hapa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kuzingatia ni kwamba wawekezaji pamoja na maneno nzuri na ahadi nzuri wakati wanapoomba vibali. Pia ni vyema wakafuata maelekezo wanayopewa na Mamlaka hii ya Vitega Uchumi kwa kuwashirikisha wananchi kwa asilimia mia katika miradi yao waliopo kwenye Shehia zao. Kufanya hivi kutaondoa manung'uniko na malalamiko ya baadhi ya maeneo yanayoekezwa kwamba wananchi wazawa wazalendo wa maeneo hayo, wananyimwa fursa za kazi.

Hili naiomba Wizara ya Kazi kusimamia vyema makubaliano yanayofanywa kati ya wawekezaji na wananchi kwenye maeneo ya uwekezaji, kwamba kutoa kipa umbele kwa nafasi za kazi kwa wananchi wa maeneo husika ya miradi inayokusudiwa kutekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utalii; kama nilivyosema mimi nitapita kidogo kidogo mbio mbio. Kuhusu sekta ya utalii. Pia sina budi kuipongeza sana Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mimi mwenyewe sekta ya utalii imenigusa katika jimbo langu. Kwenye Jimbo langu la Konde kuna vivutio vingi vya utalii. Kama vile msitu wa Ngezi, ufukwe wa Vuma Wimbi na chumba cha baharini ambacho kipo Hoteli ya *Manta Reef*. Chumba hiki unaweza kusema kwa hapa Zanzibar ndiyo pekee iliyoweza kujenga chumba baharini na ni kivutio kikubwa kwa watalii.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mambo mazuri na dhima nzuri ya serikali, lakini katika sekta hii kwa upande wa jimbo langu kuna changamoto nyingi. Moja ya changamoto ni kilio cha wananchi wa Shehia ya Makangale na Shehia ya Tondooni inayozungukwa na biashara hiyo ya utalii.

Mhe. Mwenyekiti, lengo la serikali ni zuri la kutoa ardhi kuwapa wawekezaji. Mimi ninakumbuka kwa mara ya kwanza pale Makangale, ardhi ya kwanza iliyoanza kutolewa kwa Hoteli ya *Manta Reef* ilikuwa miongoni mwa miaka tisini. Baada ya kutolewa ardhi hiyo *Manta Reef* wakaanza kujenga hoteli nyingi au wawekezaji wengi walionesha dhamira ya kutaka kuwekeza. Lakini hadi hivi leo tunazungumza Mhe. Mwenyekiti, ni hoteli tatu tu ambazo zinafanya kazi. Ni Hoteli ya *Manta Reef* na ipo moja maarufu wanaita Mti Mweupe na Hoteli ya Swahili *Diver*. Hii Hoteli ya Swahili Diver, huyu mwenyewe anaitwa Rough na ni rough kweli huyu Mhe. Mwenyekiti. Hoteli hii inajishughulisha zaidi na mambo ya *diving*.

Sasa ninawaomba watu wa *ZRB* na *TRA* kwamba huyu Bwana Rough ambaye ni *rough* wamuangalie kwa makini jinsi ya ulipaji wake wa kodi kwenye hoteli anayoiendesha. Mhe. Mwenyekiti, sina uhakika wa mambo lakini na ndiyo maana nikawaomba *ZRB* na Mamlaka ya Kukusanya Mapato ikishirikiana na Idara ya Kazi waifuatilie kwa makini utaratibu wa ulipaji wake wa kodi.

Sambamba na Hoteli ya Mpapindi ambayo tumeisoma katika ripoti kwamba inadaiwa zaidi ya Dola laki tatu za Kimarekani. Mimi ninataka nihoji kitu kimoja. Ikiwa kweli mtu anadaiwa zaidi kodi ya Wazanzibari, kapewa ardhi kwa ajili ya kuendeleza Wazanzibari wanufaike. Mtu anadaiwa Dola laki tatu. Hajanyang'anywa umiliki. Kuna sababu gani ya msingi inayomfanya mtu huyu aendelee na ni kigezo gani kinachompa kufanya kuitwa mwekezaji. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaomba sana taasisi inayohusika na mambo ya kodi ifuatilie nyenzo za hoteli mbili hizi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kilio cha wananchi wa Makangale na Tondooni ni kwamba ardhi walizokuwa wakizitumia kwa kilimo zimezuiwa kwa ajili ya uwekezaji. Lakini hakuna kitu chochote kinachoendelea hadi hii leo zaidi ya kunyanyasika kwa watu wa Makangale kwa kukosa maeneo ya kulima, maeneo ya kuchunga na maeneo mengine. Kwa sababu maeneo mengi waliyopewa wawekezaji wameshayamiliki kwa kuyapiga ukuta, huoni kilichomo ndani lakini pia huoni faida yoyote inayopatikana kwa uzuiaji huo. Ina maana hainufaishi wananchi wa Makangale wala serikali. Kwa sababu lengo la serikali pamoja na kuwa watalipa kodi, lakini ni kuona kwamba ile kazi inafanywa na wananchi wanapata ajira kwenye eneo husika.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba hili lichukuliwe hatua kidogo za ufuatiliaji, kutaka kujua wale watu au wanaojiita wawekezaji, waliokuwa wameshapewa hati na kwa nini hawataki kuyaendeleza maeneo yale. Kwa sababu sheria ipo kwamba utakapofika muda fulani ukashindwa kuliendeleza

eneo hilo lirudi serikalini. Naiomba Wizara inayohusika ya Ardhi ikishirikiana na Mamlaka ya Ukuzaji na Uendelezaji Vitega Uchumi (*ZIPA*) na watu wa Kamisheni ya Utalii, wawaite na wawapate wawekezaji wote, wawape muda na watakaposhindwa kuyaendeleza maeneo yale, maeneo hayo yarudishwe ima kwa wananchi au warudishwe na umiliki wa serikali, yatafutiwe wawekezaji wengine waweze kuyaendeleza. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, huo ndio mchango wangu kuhusu utalii. Sasa nakwenda kidogo kwenye Wizara ya Mawasiliano. Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi ni dhahiri kwamba sekta ya mawasiliano imepiga hatua kubwa katika nchi yetu. Imeweza serikali kutujengea barabara nzuri. Ni jambo la kufurahisha. Mwenyezi Mungu awajaalie viongozi wetu hawa, awape hekma na busara, kwa sababu kilio cha barabara hasa katika barabara yangu ya Konde/Wete, kilikuwa ni kilio. Barabara yangu ya Konde/Wete iligeuzwa jina, ikaitwa mkunga. Maana yake ukitoka Konde kwenda Wete mja mzito alikuwa akiingia mule kwenye gari hafiki Wete, anazalia njiani.

Sasa unaweza barabara ya Konde/Wete ni barabara ya kwanza kwa Zanzibar iliyo nzuri. Kwa hivyo ninaipongeza sana. Nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati na kumuombea dua nyingi Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa bidii yake aliyoionesha na kutekeleza ahadi yake ya kwamba barabara ya Konde/Wete, shida ya wananchi wa Konde mutaisahau. Na kweli tumeisahau kwa muda mfupi. Eeh! Mwenyezi Mungu mjaalie umpe afya na umri mrefu Rais wetu aweze kutuongoza vyema. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo ya kuwa na barabara nzuri. Kuna changamoto nyingi zinazojitokeza juu ya utumiaji wa barabara hizo. Mhe. Mwenyekiti, kila kitu kizuri hakikosi kasoro. Kasoro za matumizi mabaya ya barabara yameanza kujitokeza kwenye barabara hizo ambazo sasa zinasababisha ajali kutokana na watumiaji wa barabara wa kutokuheshimu sheria za barabarani.

Mhe. Mwenyekiti, kadhia hii siyo kwa Pemba tu. Kadhia hii nimeishuhudia zaidi kwa upande wa Unguja. Nimeshuhudia kwa baadhi ya barabara hasa ya Bububu. Watumiaji wake kutokuwa waangalifu. Ni jambo la kusikitisha sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba serikali inapoteza nguvu kazi nyingi. Kwa sababu ya vijana wanaendesha vyombo hasa vya maringi mawili. Kila wiki barabara hizi zinagharimu maisha ya vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako karibu kumalizika. Angalia vizuri.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Mengine nikikosa muda nitachangia kwa maandishi.

Kwa hivyo naiomba Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ichukue hatua za dharura ikishirikiana na Jeshi la Polisi na kuwapa adhabu kali wale watumiaji waliokuwa hawajali, wanaovunja sheria za barabarani, hasa wenye daladala na madereva wenye vyombo vya matari mawili.

Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, utamkuta mtu mwenye daladala anasimama bila ya kujali, kwa sababu kamuona abiria mmoja wa shilingi 200/- anahatarisha maisha ya abiria 30 alionao kwenye gari yake. Mheshimiwa ni jambo la kusikitisha na linalohitaji kuchukuliwa hatua za dharura, kama hatukufanya hivyo tutakuja kujikuta tunapoteza nguvu kazi nyingi za taifa.

Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na ikishirikiana na Jeshi la Polisi itachukua hatua madhubuti juu ya watu wanaovunja sheria za barabara.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo kwa sababu umeniambia muda wangu umekwisha, basi nachukua nafasi hii kurudia kuwapongeza viongozi wetu wakuu wa kitaifa na kuwaombea dua kwa Mwenyezi Mungu awape hekima na busara. Kama nilivyoahidi kwamba michango yangu mingine nitaitoa kwa maandishi. Basi napenda kutamka kwamba naiunga mkono hotuba hii ya makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2016/2017 kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uwezo wa kuwepo hapa asubuhi hii. Kadhalika niwe mchangiaji katika hotuba hii ya bajeti. Pia napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuchaguliwa tena kwa kura nyingi kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Vile vile napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Mawaziri wote waliochaguliwa. Zaidi nawapongeza wananchi wa Jimbo la Welezo kwa kumchagua Hassan Khamis Hafidh, kuwa Mjumbe wa Baraza la Tisa la Wawakilishi la Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, juzi hapa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango aliingia na begi lililojaa pesa kwa ajili ya bajeti ya mwaka 2016/2017. Kwa hivyo, na mimi naomba nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa jinsi alivyoingia kwa kujiamini, kwa mbwembwe nyingi na akiwa hana wasi wasi, kwamba begi lile limejaa fedha za maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

Halikadhalika Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kaingia na bajeti iliyojaa mipango na mikakati madhubuti ya maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar.

Vile vile napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, mara tu baada ya kuingia alikuja na wazo ambalo mimi kwa kweli nimelipenda sana, kwa sababu ilikuwa ni kadhia ya wafanyabiashara na Wazanzibari wengi kila siku wakilalamika, kwamba tunachukua gari hapa Zanzibar tunazipeleka Bara, tunachajiwa na mapesa yale yanabakia Bara hayarudi Unguja. Lakini mara alipoingia huyu Waziri wa Fedha mpya Dkt. Khalid Salum Mohamed, yeye alihakikisha kwamba anakuja na maamuzi kuwa pesa hizi sasa gari inapokwenda Dar es Salaam utachajiwa hapa hapa na pesa zetu zitabakia hapa Zanzibar kwa matumizi na maendeleo ya Zanzibar. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, naomba nichukuwe nafasi hii kukupongeza sana kwa hili. *(Makofi)*

Aidha, Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kitabu cha ukurasa wa 27 kuna mambo 8 ambayo yanaashiria kubana matumizi, kwa lugha ya kitaalamu tunaita *structural Adjustment programme,* yaani taifa lolote linapotaka kuendelea au mtu ni lazima kwanza ahakikishe anabana matumizi, ili apate fedha nyingi kutumia katika masuala ya maendeleo. Napenda kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuliona hilo na kulitekeleza kwa vitengo.

Vile vile napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Rais tena wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kutekeleza ahadi yake aliyosema kwamba mara tu baada ya kuingia madarakani kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja, basi atawaongezea mshahara wananchi wa Zanzibar kufikia shilingi 300,000/-.

Kwenye bajeti hii ya mwaka 2016/2017 tumeona Mhe. Waziri wa Fedha kaja nayo na kaitekeleza kwa vitendo kwamba kuanzia mwezi wa Aprili mwakani *Insha-allah*, wananchi wote wafanyakazi wa Zanzibar kima cha chini cha mshahara cha Zanzibar kitakuwa mara mbili. Kama ulikuwa unapata shilingi 200,000/- basi ukienda kwenye banki mwezi wa Aprili basi utakuta shilingi

500,000/-. Kwa hivyo, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais kwa kutekeleza azma yake hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nianze hotuba yangu kwa kuanza kuchangia. Mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, utaanza kwa Wizara ya Afya. Mhe. Mwenyekiti, tunayo Wizara ya Afya ambayo kama sikosei itakuwa na jukumu la kututibu na kutulinda tusipate maradhi. Tunapokwenda hospitali za Zanzibar tunajua zipo changamoto nyingi, lakini kuna baadhi ya maradhi unashindwa kutibiwa Zanzibar kutokana na sababu mbali mbali za kimsingi, inabidi madaktari waku-*refer* upelekwe nje.

Mhe. Mwenyekiti, jana waliposoma hotuba ya wenyeviti walisema wazi wazi kwamba deni tunalodaiwa nje kwa sababu ya matibabu ni milioni moja dola. Lakini kibaya zaidi unapokuwa umekuwa *referred* na daktari upelekwe nje, unapokuwa katika *waiting list* maskini wengine huwa hawawahi kupelekwa nje wanafariki. Kwenye jimbo langu kuna mwananchi wangu mmoja alikuwepo katika *waiting list* wakati ninagombania, anasubiri kupelekwa India alifariki, na wengi hutokezea; Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema wale wote waliokuwa wanasubiri na huwa hawawahi na wanafariki.

Kwa hivyo, ukiangalia Mhe. Mwenyekiti, kadhia hii ni kubwa na inatu- *cost* kiuchumi na kijamii, kwa sababu unaumwa unajua unaweza kutibiwa, lakini ndio huna uwezo wa kujitibu, unaisubiri serikali ikupeleke nje huna uhakika kama utafika huko nje na wengine hufa.

Kwa hivyo, mimi nataka kuiomba serikali kwa nia njema kabisa, hebu ifanye utafiti kwa siku zisizokuwa nyingi kutafuta madaktari Cuba wapo wengi, wawalete Zanzibar tupate na vifaa vilivyokuwa bora, ili haya matibabu baadhi yao tunayotibiwa India tuweze kutibiwa hapa Zanzibar. Mimi naamini tunaweza kupunguza gharama, tutapunguza *stress* za wananchi na wananchi wa Zanzibar wataishukuru sana serikali kwa hili.

Naiomba sana Wizara ya Fedha ijaribu kuratibu hili suala huko kwenda kutibiwa nje kupunguwe kunatugharimu kwa kiasi kikubwa sana serikali yetu. Hilo moja Mhe. Menyekiti.

Jambo la pili Mhe. Mwenyekiti, kuna Mkoa wa Mjini na Magharibi na hii Magharibi imegawika makundi mawili sasa hivi. Kundi la kwanza Magharibi A na Magharibi B. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka huu Magharibi A na B si zaidi ya watu 400,000 wanaishi katika Magharibi A na B.

Kwa maana hiyo, kwa mujibu wa *population* ya Zanzibar watu wengi Zanzibar nzima wako Magharibi, lakini cha kusikitisha Magharibi huku hakuna maji, njia, umeme wala hakuna chochote na ndio kunakoishi watu wengi. Juzi mwananchi wangu mmoja anaishi kule Michikichini Welezo, aliita gari kumpeleka hospitali kujifungua basi hakuwahi kufika alizalia njiani na mambo kama haya yapo kila siku.

Kwa hivyo, naiomba sana serikali itazame kwamba huku Magharibi ndiko kulikohamia watu wasikuangalie mjini tu, likiwemo Jimbo langu la Welezo kuna watu wengi sana Zanzibar nzima inaishi Magharibi, hii miundombinu inayotakiwa na binadamu basi waharakishe kuipeleka, watu wanafariki siku zao bado kutokana na kutokuwa na miundombinu huku Magharibi.

Mchango wangu mwengine naupeleka katika ukusanyaji wa mapato. Naishukuru sana taasisi yetu ya Zanzibar inayoitwa *ZRB, Zanzibar Revenue Board* ambayo inakusanya mapato ya Zanzibar kwa matumizi yetu ya kijamii. Lakini utafiti wangu mimi hasa, nimefanya utafiti wa kina nimegundua hii *ZRB* inafanyakazi nzuri, inazo changamoto za kibinadamu, lakini nimegudua inafanyakazi nyingi. Ukilinganisha na nchi nyengine, nitatoa mfano *ZRB* ina majukumu kama sikosei ya kukusanya kodi, ina majukumu ya kuwatafuta wasiolipa kodi,ina jukumu la kuwatafuta wasiolipa kodi kwa wakati, ina jukumu la kuwatafuta wasiyolipa kodi inayotakiwa na vile vile ina jukumu la kuwashitaki. Hawa wote wanafanya makosa yanayohusu kulipa kodi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa natoa ombi au pendekezo. Nchi za wenzetu kwa mfano Spain, Ghana wanazo hizi *Revenue Board*, lakini *Revenue Board* kazi yake kama nchi ya Ghana na Spain inafanyakazi ya kukusanya kodi tu, kwa vile ina jukumu moja basi inafanyakazi kwa ufanisi.

Kwa hivyo, naomba *ZRB* nayo Mhe. Waziri ifanye kazi ya kukusanya kodi tu, halafu iundwe taasisi nyengine iitwe *Zanzibar Revenue Monitoring Agency*, iwe na jukumu la kuwatafuta wasiolipa kodi, iwe na jukumu wasiolipa kodi kwa wakati, wasiolipa kodi kwa kiwango kinachotakiwa na kuwashitaki.

Nchi kama Spain na Ghana imefanya hivyo basi inafanyakazi kwa ufanisi na kodi hapa nasema wasi wasi itapatikana nyingi. Namuomba sana Mhe. Waziri kama wazo hili analikubali basi aende tu kwa nia safi kabisa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na akaseme Mhe. Rais kuna wazo limetolewa tulitekeleze kodi itapatikana nyingi. Nimetoa mfano wa nchi mbili baada ya kufanya utafiti ambapo zimefanya hivyo na zimefanikiwa.

Pia Mhe. Waziri alipokuja na bajeti yake juzi hapa alituambia kwamba tunahitaji bilioni zaidi ya 840. Bilioni zaidi ya 400 tutazipata kwa kukusanya kodi ya ndani, lakini bilioni zaidi ya 300 alisema tutazipata kutoka nje. Kwa hivyo, namuomba hebu akija hapa mimi Hassan Khamis Hafidh Mwakilishi wa Jimbo la Welezo, atuambie ni uchawi gani, utaratibu gani au njia gani atatumia; maana yake isijekuwa tunapitisha bajeti hapa tumeambiwa tu hatujajua, basi atujuze na sisi kidogo. Ni utaratibu gani au uchawi gani atatumia na atazipata wapi hizi pesa. Isijekuwa tumeshaipitisha bajeti wananchi wetu wakienda hospitali wakaambiwa bwana pesa hakuna, kumbe zile pesa nyengine tulizoambiwa zitapatikana hazijapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naingia katika sekta ya kilimo. Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu inakula mchele kwa mwaka tani elfu 85,000 na nchi yetu inalima kwa mwaka tani 15,000. Katika kukuza uchumi na kutafuta ajira kwa vijana, basi naiomba serikali ije na azimio mahususi la kuongeza kulima mchele angalau nusu ya tunachokila.

Nchi kama Nigeria imefanya hivyo, kuna Waziri wa Rice na imefanikiwa sana na inalima mpunga mwingi. Lakini kwenye hii sekta hii ya kilimo kuna vitu kama karoti na pilipili boga, hivi vitu tunavitumia siku hizi vingi na vinatoka Bara.

Hivi kweli Zanzibar mabonde tuliyonayo ya mpunga na eneo tulilonalo tunashindwa kuulima mpunga. Utafiti unaonesha wazi mabonde tuliyonayo Zanzibar ya mpunga yanatosheleza kulisha mpunga mara mbili ya nchi kama Zanzibar. Lakini mabonde tunayo hatuyatumii, naomba tuyatumie ipasavyo mabonde haya kulima mpunga ili uweze kuwalisha Wazanzibari.

Kadhalika na hizi *vegetable* nilizozitaja nazo pia Mhe. Mwenyekiti, umefika wakati wa kuweka mkakati wa kuzilima wenyewe ili wananchi wetu hasa vijana wapate ajira na tuwache kuagiza kutoka nje. Huu utegemezi wa kuagiza kutoka nje una hatari zake.

Mhe. Mwenyekiti, naingia katika sekta ya uvuvi. Katika kisiwa kilichofanikiwa duniani kimoja ni Zanzibar, Alhamdulillah tumezungukwa na bahari. Lakini cha kushangaza na cha aibu, siku hizi ukisogea mbele kidogo kama mita 600 pana mtu anauza samaki, sijui anawatoa wapi, marehemu samaki.

Samaki hao mpaka wafike hapa wanachukua miezi sita ndio samaki tunaokula. Sasa mimi naiomba Serikali ya Zanzibar hebu ifanye utafiti ije na azimio la kuwafundisha wavuvi wetu, kila siku wanahangaika kulima.

Mhe. Mwenyekiti, mvuvi anakwenda mpaka baharini siku tatu hajui kama atapata samaki wala hajui vipi, anakwenda kwa kubahatisha lakini ndio haya hana la kufanya jengine, inambidi maskini jamaa zangu wa Uroa, Charawe na Paje wende tu hawana kazi nyengine maskini ya Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikwenda Sweden pale, unamkuta mvuvi anafanya mahesabu kwanza kabla hajenda baharini, akifika baharini anajua hasa ninakwenda kuvua tani ngapi. Ukienda Norway na Finland basi akirudi mvuvi yule ana tani kuliko zile alizozivua. Nilichogundua kwa sababu kwanza wana vifaa, elimu na wametaalamika, kwa sababu serikali yao inawasomesha kila siku, ina waelimisha na inawapa vifaa.

Kwa hivyo, naiomba na Serikali ya Zanzibar kwa sababu tumezungukwa na bahari, katika kuwatafutia ajira vijana basi ije na azimio nayo ya kutupa vifaa, kutufundisha na ipo haja kwa mahususi kuanzisha Chuo cha Uvuvi Zanzibar, ili Wavuvi wetu waache kuishi maisha ya kubahatisha, wakienda baharini waje na samaki na sisi pia tuwache kula samaki wa *perdue*, samaki kafa miezi sita tunamla leo Zanzibar haipendezi.

Mhe. Mwenyekiti, naingia katika Sekta ya Utalii. Utalii Mhe. Mwenyekiti, ndio roho ya Zanzibar ukiwacha karafuu. Lakini kuna mambo matatu makuu katika utalii ambayo yanahitajika. La kwanza amani na utulivu. Kwa hapa naiomba sana serikali ifanye kila jitihada ihakikishe isimuonee mtu huruma wala haya, inalinda amani na utulivu wa Zanzibar tulionao. Wakati wa muhali umekwisha ni lazima tulinde amani na utulivu wa nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kitu cha pili kinachohitajika ni soko, kuwaita wale watalii njooni Zanzibar msiende Mombasa, watalii msiende Mauritius njooni Zanzibar ni lazima tuwaite. Cha ajabu ukienda hizo nchi nyengine matangazo unayoyakuta yale ya biashara yameletwa na Serikali ya Muungano, sisi Zanzibar tupo, watalii tunawataka wanatutilia pesa, lakini hatuchukui jitihada ya kuutangaza ule utalii.

Kwa hivyo, naiomba serikali sasa ije na azimio maalum ili upate samaki ni lazima utie samaki. Tusiogope kuutangaza utalii, mbona Kenya wanatuibia mpaka Mlima Kilimanjaro anasema ni wake.

Ukishuka *underground* ya Uingereza utakuta Mlima wa Kilimanjaro umeandikwa Kenya kumbe wa Tanzania, yote ni kuutangaza utalii kwa sababu unafaida. Naiomba serikali iwaongezee pesa tena nyingi Kamisheni ya Utalii waendelee kuutangaza utalii ili tupate pesa. *(Makofi)*

Chengine Mhe. Mwenyekiti, katika utalii kitu muhimu mazingira bora. Mhe. Mwenyekiti, tusiseme uongo nchi yetu hasa mjini chafu, mji mchafu. Juzi Mhe. Haji Omar Kheir alikuja na utaratibu wa jinsi gani atausafisha mji. Alisema kwa kujiamini na akiwa amesimama ametunisha kifua na alisema akiwa amejiamini kwamba safari hii "...nimeazimia kuusafisha mji, hata ng'ombe sitomkamata barabarani nitamfuata aliko". Nanukuu maneno ya Mhe. Haji Omar Kheir, hebu mimi namuombea apewe pesa ausafishe huu mji.

Kwa sababu katika utalii mgeni anapokuja kuna soko linaitwa *word of mouth*. Mtalii anapokuja Zanzibar na anapomuhadithia mtalii mwengine kwamba Zanzibar *is marvellous, is wonderful, you better go and see yourself,* itatusaidi kuja watalii wengi kuliko njia yoyote nyengine tunayoitumia. Kwa hivyo, naiomba sana serikali itumie njia hii katika kuhakikisha inautangaza utalii.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kusema kuna aina tatu kuu duniani za utalii. Aina ya kwanza utalii wa nje, yaani mtalii kutoka nchi nyengine kuja nchi nyengine. Aina ya pili *Diaspora Tourism* na aina ya tatu ni utalii wa ndani.

Serikali ya Zanzibar bado imejishughulisha na utalii wa aina moja tu, utalii wa wageni kutoka nje bado haijajishughulisha na utalii wa ndani. Leo hii Mhe. Machano Othman akitaka kwenda Lagema kulala na familia yake, akikutana na bei kule ya dola 350 kwa siku anasema bora nikamalize nyumba yangu.

Kwa hivyo naiomba serikali Mwenyekiti ije na azimio la kuja na sera itakayohamasisha utalii wa ndani, ihamasishe ili waheshimiwa na watu wengine wakitaka kwenda mahoteli wasikutane na ile bei ya dola 350 kwa siku. Marekani wameweza kufanya hivyo, mtalii wa ndani wa Marekani anapokwenda mji mwengine anakutana na *half price* ya bei lakini mgeni anakutana na *full price*. Hii itatusaidia zile siku alizozisema Mhe. Simai Mohammed Said na mimi nitaweza kwenda mahoteli kulala. Itakuwa tunafanya utalii wa ndani, pamoja na Diaspora wetu watakapokuja nchini, watapata kwenda kufanya utalii wa ndani.

Kipato cha serikali hapa kitaongezeka Mheshimiwa, naomba sana sera ya utalii wa ndani kuwanufaisha wananchi wa ndani kama *Diaspora* itumike kwa sababu ni hatari mwananchi kazaliwa Zanzibar lakini hata yale maeneo ya hoteli kupita anayaogopa, anajua ukipita huko bei yake utakufa tu, naomba iwe hivyo.

Mhe. Mwenyekiti. chengine ajira kwa vijana; nchi yetu ina tatizo kubwa sana la ajira kwa vijana, kubwa vijana wetu hawana ajira naiomba Serikali ije na

azimio mahususi la kuhakikisha kwamba inarudisha ule mfumo wa zamani. Tulikuwa tuna viwanda vidogo vidogo hapa mimi. Nakumbuka Zanzibar yakitengenezwa madishi Viwanda vidogo vidogo yakiuzwa Comoro na nchi nyengine, sabuni, samli, mafuta yakitengenezwa. Hebu tujaribu kuja na utashi wa kutangaza na kuwaita wawekezaji katika *small industries* ili wananchi wetu na vijana wetu wapate ajira. Ni hatari Mheshimiwa, leo vijana wamefikia kuowa na kuolewa lakini anajiuliza nifanyeje, hatimae wanaangukia kula unga na kuvuta bangi tunawalaumu, kumbe masikini ya Mungu cha kufanya wakati mwengine wanakuwa hawana. Sina maana kuwaambia wakavute bangi au wakale unga *no,* lakini cha kufanya wanakuwa hawana.

Mhe. Mwenyekiti. katika bajeti yako kuna pahala pameandikwa mfumko wa bei Zanzibar ni kama nchi nyengine za dunia ilipohama kutoka mfumo wa ki-*socialist* ilipohamia kwenda katika mfumo wa kibepari, tulipowaachia matajiri kufanya biashara kosa tulilolifanya matajiri hawa tuliwaachia kila kitu.

Leo wanatufanyia wanavyotaka, zamani tulikuwa tunafanya utafiti ninaambiwa Wizara ya Biashara kulikuwa kuna Tume ya Bei, hii kazi yake ku-*regulate* au kufuatilia mfumo mzima wa bei ya kitu chochote kinachoingia Zanzibar, ili kimfike mwananchi katika bei nafuu asiachiwe tajiri akawakomoa wananchi. Kinachofanyika sasa hivi Zanzibar, matajiri wanaofanya biashara hasa ya vyakula wanawakomoa wananchi na ni kwa sababu hakuna taasisi inayo-*regulate* au inayofuatilia mifumo hii ya bei.

Nitatoa mfano, mimi nilikwenda Bama kuangalia mchele niliwahi kufanya biashara, niliukuta mchele huu wa mapembe unauzwa 10 *pens* ya dola na mchele wa jasmin unauzwa 25 *pens* ya dola, lakini Zanzibar wakati huo ulikuwa unauzwa 1600 na Mheshimiwa kila mtu namuomba afanye *research,* naonesha jinsi gani matajiri walivyoachiwa wafanye watakavyo kunako masuala haya ya bei. Kila mchele wa jasmin na mchele wa mapembe unapokuja nchini siku zote bei inakuwa mpya, kwa sababu hakuna taasisi inayo-*regulate*.

Chengine cha kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, tajiri alivyoachiwa afanye atakavyo anakuwa na mafuta ndani ya *petrol station* yake anafika pahala anasema siuzi nasubiri bei, anaitia nchi katika shida, anawasababishia wananchi kuitukana Serikali bila ya sababu, anatutia mazonge, inakuwaje mfanya biashara wa *petrol* aliyepewa leseni na Serikali leo hii kwa kuwapa huduma wananchi anaifunga huduma ile, anasema siuzi nasubiri bei, anafanya anavyotaka na Serikali ipo.

Mhe. Mwenyekiti. naomba kusema mwananchi yeyote mfanya biashara atakayekuwa anasumbua wananchi kwa kutowapa huduma anyang'anywe leseni, wapo watu wengi wanataka kufanya biashara, pesa wanazo, mawazo wanayo lakini wengine wameshahodhi maeneo.

Kwa hivyo Mheshimiwa naomba sasa mfanya biashara hasa *petrol pump* hizi wanyang'anywe leseni, kila baada ya miezi miwili hapa utakuta mafuta hamna kumbe yamo lakini wanatusumbua.

Mhe. Mwenyekiti, taifa lolote duniani likitaka liendelee ni lazima liangalie mambo mawili; liangalie kinamama na vijana, na kama kuna mtu ananiambia si kweli hapa ajitokeze. Ghana wameendelea kwa kuwaangalia kina mama na imetokana na *theory* ya Rais wao Kwame Nkurumah aliposema *If you educate the woman, you educate the whole family* (ukimuelimisha mwanamke itakuwa umeelimisha jamii nzima) na ni kweli Mheshimi.

Mimi naiomba Serikali ya Zanzibar, imekuwa inazugumza siku nyingi itaanzisha *bank* ya akina mama, Ghana kuna *women bank,* leo wanawake wa Ghana wametajirika wamekuwa wafanya biashara wakubwa wa kupeleka nje kwa sababu Serikali yao iliwawezesha kwa kuanzishia *bank* na kuwasomesha.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana *bank* ya akinamama na *bank* ya vijana ianzishwe ili tuweze kuhakikisha tunawaelimisha kinamama na vijana kujiajiri, Serikali haiwezi hata siku moja kuajiri watu wote na nalikubali hilo, lakini pia tuchukue hatua ya makusudi kuhakikisha tunawaanzishia *bank* na kuwasomesha, ili waweze kujiajiri kinamama. Kinamama wanapoweza kujiajiri akiweza kupata kipato ndio mlezi wa watoto na watoto wale kila siku watakuwa wamenyooka.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakuja katika mawasiliano na miundombinu, kwanza Mhe. Waziri jana Naibu Waziri wa Miundombinu alipokuwa akisema, alisema anajenga barabara ya fuoni ya kimataifa, ni kweli nakubaliana na maneno yake lakini kila nikiipima na nikiitizama ile barabara nzuri, mimi nakaa fuoni haina viegesho vya gari, dala dala haya, magari ya shamba yatakuwa yanasimama wapi, ili kusitokee *disturbance* ya wanaokwenda na kupunguza ajali.

Ajali nyingi zinatokea hasa katika barabara yako ya Mkapa *road,* kwa sababu barabara ile haina pa kusimama daladala. Kila siku wanagongwa watoto, wanauliwa kwa sababu inakosa sehemu ya kusimamia daladala. Naomba sana barabara tunazozijenga tukaziita za kimataifa ni lazima tuziangalie jinsi gani

gari za abiria zitakuwa zinapo pa kusimama, lazima tuliangalie hilo ndipo ifikie *standard* ya kuwa na umataifa.

Chengine Mhe. Mwenyekiti, naamini Shirika la Bima lipo katika Wizara yako, Zanzibar kuna shida moja kubwa Mhe. Mwenyekiti, ya ajali zisizokuwa za mpango, halafu hakuna kinachotokea, na dereva wa dala dala akishakumgonga mtu Mhe. Mwenyekiti, anakwenda siku mbili hospitali anampelekea soda.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda angalia, muda wako umebakia mdogo sana.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante anampelekea soda na maji halafu anaingia mitini. Mheshimiwa, nchi zilizoendelea unapokata *insurance* au inaitwa Bima inakuwa ina-*cover* dereva, inam-*cover* abiria, inam-*cover* mwenda kwa baskeli, inam-*cover* aliyepakiwa, mpaka yule mtu wa kawaida anayetembea ambae yupo kwenye *risk.* Lazima nchi yetu sasa itizame hivyo.

Ninamjua mwananchi wangu kakatwa uti wa mgongo na mwenye dala dala, pesa ya kupelekwa India hana, leo yupo juu ya kitanda anakufa uwezo hakuna, na mwenye dala dala anaendesha dala dala yupo, lakini ingekuwa kuna *insurance,* yule angeweza kulipwa. Naomba sana hili tuliangalie, na natoa mfano Uingereza imeendelea sana kwenye suala hili.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, ardhi ya Zanzibar ni masikini na nchi yetu ni masikini tunategemea ardhi ili tuweze kuendelea. Kuna ardhi nyingi wanazo matajiri huko mashamba kunako bahari kuna wawekezaji wengi wanataka kuwekeza, lakini wakifika wanapigwa rungu la dola milioni kununua ardhi. Dola milioni tatu ardhi wanayo wameikumbatia, wanataka mapesa mengi.

Namuomba Mhe. Waziri wa ardhi awafutie wale wote matajiri wenye ardhi wasiyoitumia na akitokea muwekezaji akitaka kuwekeza kunako ardhi ya hoteli apewe muwekezaji. Wameweka ardhi hawaitumii umasikini unazidi kutuingia.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache niliyoyaeleza, kwa mbwembwe alizoingia nazo Mhe. Waziri wa Fedha na kwa jinsi alivyoingia kwa kujiamini na mambo mazuri aliyoyaeleza katika bajeti yake hii, na Daktari wa kwanza kama sikosei kuiongoza Wizara ya Fedha. Mimi Hassan Khamis Hafidh Muwakilishi wa wananchi jimbo la Welezo, naomba sana na nachukua fursa hii kuiunga mkono bajeti hii mia kwa mia, na pia kumuombea dua Mhe. Waziri huyu wa fedha wa Zanzibar, kesho awe bwana mwenye fedha, aende vizuri katika kutuletea maendeleo wananchi wa Zanzibar maendeleo endelevu.

Mhe. Mwenyekiti baada ya hayo machache naomba sana kwa unyenyekevu mkubwa kuwasilisha ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii uliyonipa kutoa mchango wangu katika bajeti hii nzuri sana ya Wizara ya Fedha, lakini kabla sijatoa mchango wangu napenda nimpongeze sana Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa bidii zake anazozichukua katika kuliendesha taifa hili la Zanzibar kwa mafanikio. Tunaelewa Dkt. Ali Mohammed Shein ametoka mbali tukianza tu na uajiri wake Serikalini alianza Wizara ya Afya akiwa ni mfanyakazi katika Wizara ya Afya, kwa mafanikio yake hatimae aliweza kuwa Naibu Waziri wa Afya na baadae kuwa Waziri wa Utawala bora wakati ule.

Mhe. Rais wa Zanzibar aliwahi pia kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muda wa miaka tisa, hivi sasa Mhe. Rais anaiongoza Zanzibar kwa kipindi cha pili kwa mafanikio makubwa. Nampa hongera nyingi sana na inshaallah Mwenyezi Mungu amuwezeshe atuongoze kwa heshima na busara.

Mimi kwa upande wangu huwa nasononeshwa sana na wale wanaopinga maendeleo haya ambayo tunayapata, yaani tumebarikiwa kuwa na uongozi mzuri sana, kiongozi mwenye sifa zote, anaendesha kwa upendo mkubwa nchi yetu hii ana mapenzi makubwa na wananchi lakini bado kuna wachache wanajaribu kuyapinga maendeleo haya wanaharibu hata miundombinu.

Mimi nasema kwa kweli wajirekebishe, maana wasiilazimishe Serikali kuchukua hatua ambazo hawatazifurahia, waangalie wenzetu wa Afghanistan walianza hivi hivi choko choko ndogo ndogo, sasa hivi wananchi kule hawajijui. Unaweza kufuatana na mwenzako mnatembea mara yeye bomu limempata, wewe kwa manusura pengine bomu.

Hivyo hivyo Iraq ilikuwa nchi imetulia wakaanza choko choko *dictator* nani, matokeo yake hivi sasa Iraq haina salama kila siku vita. Tukiingia katika bara letu la Afrika hapa Libya tu karibuni choko choko kama hizi zimekwenda mpaka wamemuua Gadafi. Gadafi katusaidia sana hapa hapa Zanzibar. Huko bara kuna misikiti mizuri mizuri mingi kasaidia kujenga, kuna mahoteli kasaidia alikuwa anashirikiana sana na waafrika wenzake, matokeo yake wameleta choko choko, wamemuua hivi sasa Libya hakukaliki.

Nawaomba sana ndugu zangu hawa wajue, wanajua lakini nataka wafahamu kwamba kiongozi wetu wa Zanzibar na viongozi wote wa Zanzibar hapa na sisi sote ni Wazanzibari kama wao, hakuna budi kuweka mapenzi baina yetu, tuendeshe nchi yetu linalofanywa kwa maendeleo ni kwa jamii nzima sio kwa mtu binafsi, wala sio kwa mtu mwenye itikadi fulani.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana Wizara ya Fedha ijitahidi sana kutoa mchango wake mkubwa sana kwenye kuleta amani utulivu na upendo katika nchi yetu.

Niingie kwenye Baraza letu, sasa nalipongeza sana Baraza letu limeanza kwa umahiri na umakini mkubwa sana linatoa michango ya busara ya kuendesha nchi hii, linakosoa, linapendekeza, linaonya; naliombea sana Baraza hili liendelee. Hivyo kwa manufaa ya wananchi wetu, lakini pia napenda kulionya sana Baraza letu hili na sote na mimi mwenyewe najionya kwamba ni vizuri tuwepo katika vikao vyetu vyote tukiwa kamilifu, kwani tukiwa wengi ndio michango itakuwa mingi. Haitapendeza sana kuona wawakilishi si chini ya thamanini wapo, ukija kuhesabu pengine utakuta nusu yao hawapo.

Baada ya kuzungumza hayo sasa niingize mchango wangu kwenye Wizara ya Fedha; nasema Wizara ya Fedha kwa vyovyote vile kama ulivyo moyo wa binaadamu na kiwili wili hakiwezi kufanya kazi kama moyo haufanyi kazi na hii Wizara ya Fedha pia, nchi haiwezi kufanya kazi zake za maendeleo bila ya Wizara ya fedha. Wizara ya Fedha ndio inayowezesha mambo yote yafanyike sasa kutokana na hayo na kutokana na uongozi bora wa Mhe. Rais ambao aliueleza waziwazi katika hotuba yake alipolizundua baraza hili, ikaja bajeti ambayo kwa kweli ina manufaa kwa sote.

Sasa mchango wangu ni kwamba Wizara ya Fedha ina vianzio vya mapato ilivyonavyo na kila baada ya muda nadhani huwa wanafanya marekebisho ya viwango vya kodi kuongeza kodi, nasema *solution* ya kuongeza kodi si aula sana, kitu cha muhimu sana nadhani ni kuongeza wigo wa mapato, kodi zitaongezeka tu *automatically* badala ya kuongeza kodi kwenye sehemu ya mafuta au kwenye bidhaa nyengine kuongezea mzigo tu wananchi.

Wizara ya fedha wanaweza kufanya mambo kama yafuatayo kama walivyopendekeza wenzangu hapa, wamesema yafunguliwe benki ya akinamama, mie naunga mkono mia kwa mia, zifunguliwe benki za vijana naunga mkono, lakini pia nasema zifunguliwe benki za nyumba, wananchi wakitaka kujenga nyumba wakopeshwe, waweze kujenga nyumba.

Aidha, tunaweza kuongeza mapato kwa kuzingatia haya yafuatayo, nitajaribu kusema Wizara baada ya Wizara na nitajaribu kuzungumza kwa uchache sana kwa sababu mengi yameelezwa, tukianza na Mawasiliano na Miundombinu; wengi wamezungumza matatizo ya barabara, matatizo ya mitaro na n.k.

Mimi naongezea ni budi Wizara ya Fedha itilie mkazo sana kwenye usafiri wa nchi kavu, baharini, na anga kwa sababu hii ni miundombinu basi pamoja na kuwa na maghala ya akiba ya chakula, kwa sababu hapa Zanzibar nadhani ikija ikitokezea zahma yoyote duniani kukawa na upungufu wa chakula hatutakuwa na chakula hata cha kutuwezesha kuishi kwa mwezi mmoja, kwani hakuna maghala ya kutosha. Wenzetu wana maghala ya kuweza kuwatosheleza inapotokea zahma duniani kwa muda usiopungua miaka 10, sisi hatuna maghala hayo. Nadhani tuanzeni kuwa na maghala ya kuweka akiba ya chakula.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye usafiri wa nchi kavu kuna barabara hizi, barabara zetu tumeziona kuna ongezeko kubwa sana la magari yanayoingia kila siku. Mimi nashauri Wizara ya Fedha ifanye tathmini *percent* gani ya magari yanaingia pengine kwa wiki, kwa mwezi, kwa mwaka halafu tujitathmini barabara zetu hizi zitaweza kuzibeba ongezeko hili kwa kipindi gani, tutapata jawabu.

Kuna haja kubwa sana ya kuanzisha utaratibu wa kuweka ili kulinda usalama barabani. Kuanzisha utaratibu wa kuweka mabango katika barabara, mabango haya yaoneshe *speed limit,* yaani ukipita barabara hii usizidi *speed* 5, ukipita barabara hii usipungue *speed* 60 kuwe na mabango mengi tu. Kule Uingereza nadhani kuna mabango kila mahala na watafiti wamesema kwamba mabango yale yaking'olewa yakakusanywa yanaweza yakarundikwa pamoja urefu wake unaweza kupita mlima wowote mrefu duniani.

Pia na sisi hapa tuanzisheni utaratibu huu ukipita barabarani huko mabango unayaona ya *ZANTEL*, ya *TIGO* lakini hukuti bango linalosema barabara hii inakwenda mpaka wapi, barabara hii inaelekea wapi, barabara hii iende *speed* gani, barabara hii ufanye nini hakuna.

Kwa hiyo, wakati umefika sasa kuwe na mabango barabarani yanayoonesha kila ambalo linatakiwa katika barabara ile kwa wakati ule. Hii iende sambamba na ujenzi wa vituo vya daladala sio kila pahala mwenye daladala asimame, hii haiwezekani kabisa. Mwenye daladala inawezakuwa gari inakwenda anakuja kuikata mbele uuh anasimama hapo, anapotaka.

Mwenzangu mmoja amesema hapa kwamba anakimbilia abiria wa shilingi 200 anahatarisha maisha ya watu pengine si chini ya 30 kwenye gari lake. Kwa hiyo, hayo Wizara ya Fedha iwawezeshe wizara husika ili yatatuke matatizo haya, yaambatane pamoja na ujenzi wa *pedestrian bridge* yaani madaraja ya kuvuka kwa zile sehemu kama vile Darajani na kwengineko ili kuepusha hizi ajali za mara kwa mara.

Mhe. Mwenyekiti, usafiri wa baharini iko meli yetu nzuri imekuja pongezi sana kwa serikali kwa kupata meli ile inasaidia sana sasa hivi. Kuna vyombo vyetu pia vya kienyeji vinachukua abiria kama vile majahazi na kadhalika. Kwa hiyo, naiomba Wizara ya Fedha nayo isimamie kupatikana kwa vyombo vya kuokolea maisha ya watu kwa sababu bahari haiaminiki, bahari haiaminiki kabisa wakati wowote inaweza ikatokea zahma Kimbunga watu wakapata ajali, kama kuna maboya ya kuokolea basi naamini ajali hizi zitakuwa zinapungua sana. Hii iambatane na uangalizi wa mara kwa mara wa vyombo vyote vinavyosafirisha abiria.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye bandari, tuna bandari moja kubwa Zanzibar ni hiyo iliyopo Malindi na kuna mpango wa bandari hii kuikuza, itasaidia sana kupata ajira kwa vijana wengi sana. Lakini kuwa na bandari moja na katika hali ya uchumi unaokuwa nadhani haitoshi, kuna bandari za Mkokotoni, kuna bandari za Wete, kuna bandari ya Chake-Chake, kuna bandari kila sehemu ni vizuri bandari hizi zikakuzwa.

Sisi hapa Mkoa wa Kaskazini tulijaribu kupendekeza tuwe na bandari ya Mkokotoni ambayo itakuwa ina-*jet*, hiyo *jet* nafikiri imeshakubaliwa na nadhani itajengwa *jet* pale yenye urefu wa mita 240. Halafu tukapendekeza pia ijengwe *boat-yard* maana tunachotaka ni kukuza mapato, sasa kukiwa na sehemu ya kuegesha haya majahazi, maboti kwa utaratibu maalum tunaweza kuongeza mapato.

Maana yake hata ukim-*charge* pengine shilingi 5 kwa kuegesha gari lake pale au kuegesha boti yake hapo na maboti yale yakawa 20 yanawekwa pale basi mapato haya yataongezeka. Kwa hiyo, tujengeni na bandari ambazo zitasaidia bandari hii kubwa ambayo sasa hivi kuna *congestion* kubwa sana makontena pakuweka hakuna, mambo mengine imebidi yawekwe hapo Bwawani. Kwa hiyo, kukiwa na bandari nyingi zikawekewa na nafasi kubwa basi tutaweza kuwa na mapato mazuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ardhi, maji na nishati, tuna ardhi. Zanzibar ardhi yetu kwa kweli ni ndogo mno haitoshi sasa kila siku inaliwa na bahari.

Bahari inakula sana ardhi. Mimi nakumbuka pale Mkokotoni nilipokuwa mdogo kabisa kuna sehemu inaitwa Fungu refu, pale tulipokuwa tunakaa zamani palikuwa pana mivinje ambapo wavuvi na watu wengine wanafikia pale sasa hivi pameshamezwa na bahari hapapo. Ukisimama hapa juu mwisho wa bahari unakuona mbali sana baharini. Nadhani sasa hivi wakati umefika tuanze ku-*reclaim* bahari zetu maeneo yaliyokwisha kuliwa na bahari tuyafukie, mpango maalum uwepo kufukia bahari ili kuongeza ardhi.

Wenzetu Netherlands wanafukia bahari na maeneo haya wanaita *polders* watu wanajenga kwenye maeneo hayo baada ya kufukia bahari, watu wanalima kwenye maeneo hayo na yanarutuba nzuri sana.

Nadhani na sisi tusijiweke mbali kisiwa hiki kinakwisha wenzetu wakifukia bahari huko maji yale yanafuta pakwenda. Angalia wewe una bakuli lako hapa utie jiwe mle ndani basi maji yafurika, sasa yakifurika yanatafuta pakwenda, yakienda yanatafuta mle mwahala ambapo hamshughulikiwi. Kwa hiyo, utakuta kama kwetu sisi huku bahari inazidi kula kila siku na *speed* ya ulaji kila siku inazidi kwa sababu wanafukia bahari sisi hatuna kinga yoyote ya ardhi yetu kutokana na kulikuwa kwa bahari.

Nashauri sana moja katika mipango madhubuti ambayo ichukuliwe kwa makusudi na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na mataifa ya nje ama kwa kuandika miradi mbali mbali ni kufukia bahari ili tupate maeneo makubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi nakwenda kwenye maji, maji ni uhai na tunaambiwa siku zote zaidi ya asilimia 70 ya mwili wa binadamu ni maji. Ukikosa maji utapata *dehydration* maji mwilini yatakuwa hamna hivyo huwezi kuishi. Maji ni afya, maji ni kila kitu, maji ni usafi, maji ni kila kitu. Sasa katika maeneo mengi sana Zanzibar maji hayapatikani, hususan kwenye hilo Jimbo la Mtopepo na jirani yangu hapa kasema Jimbo la Welezo maji kule yamekuwa ni bidhaa muhimu sana, tena yamekuwa ni siasa.

Maana sasa hivi kuna wenzetu wengine wanachimba visima hata mwahala musimotakiwa mradi wavuruge tu huu utaratibu uliopo nyumba hii, nyumba hii kati kati kinachimbwa kisima karo ipo pale, vyoo viko pale kila kitu kipo pale mtu anachochea watu wakachimbe na ukiwakataza wanakuiteni Makafiri.

Sasa nadhani na hii pia inakuwa si tabia mbaya kuitumia siasa katika kupatikana kwa maji. Tunaishauri sana Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na wizara husika ihakikishe maji yanapatikana kule Mtopepo na sehemu nyengine

za Zanzibar ili tatizo la maji lisiwepo na wananchi wapate maji kwa maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie nishati ya mafuta, hii nishati ya mafuta tutakayochimba hii inakuja pole pole nashauri iharakishwe, lakini nazungumzia nishati ya mafuta tuliyonayo. Kwa kawaida mafuta yanakuwa ya aina mbili au tatu hasa *petrol* kunakuwa na *leaded* na *unleaded*. Sasa haya mafuta tunauziwa hapa sijui tuseme ni *leaded* au tuseme ni *unleaded* au *tuite super*.

Ni aina moja tu ya mafuta kuna *engine* nyengine tunanunua magari hatujui tunaleta hapa, kuna *engine* nyengine zinataka mafuta ya aina fulani ziweze kudumu sasa wewe lazima utumie mafuta ya aina ile. Kwa hiyo, ningependa sana labda wizara husika itueleze haya mafuta yanayouzwa ni ya *super* au ni *ordinary* na kama ni *super* yale ya *ordinary* yako wapi?

Nakwenda kwenye habari, michezo na utalii tunajua kwamba habari ni muhimu sana katika maendeleo, na tunajua kwamba habari zinazopotoshwa zinapotosha pia jamii. Naomba sana wizara husika kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha walisimamie suala hili la habari ili habari zinazotolewa zilete funzo kwa wananchi, funzo la kuendeleza nchi sio kuibomoa nchi.

Hata hawa wanaotumia ma-*internet* kukashifu nchi, kukashifu watu, kukashifu nini na hawa nadhani ingekuwa ni jambo la busara sana wakafatiliwa na wakachukuliwa hatua zinazostahiki, kwa sababu hawawezi kudhalilisha watu kwa kutumia vyombo hivi, hivi vyombo havikuundwa vizalilishe watu vimeundwa vielimishe. Kwa hiyo, ifate maamuzi hayo waliyoewekewa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la michezo. Michezo ni afya, michezo ni burudani, michezo ni urafiki, michezo ni upendo, michezo ni ushirikiano... Mwanamichezo yeyote aliye mzuri akitoka hapa nchini akienda nchi yoyote anakuwa ni rafiki popote anapokelewa. Naishauri sana wizara husika pamoja na Wizara ya Fedha iliangalie sana suala la michezo, na hili liambatane na hivyo nilivyovitaja mbele maji yapatikane, kwa sababu mwanamichezo akishacheza lazima apate maji safi akoge, anywe aweze kupata afya, apate barabara nzuri kama mfano kule Jimboni kwangu Mtopepo barabara zilizopo sasa hivi tunasubiri mvua tupige *grader* lakini kuzipiga *grader* ukatia kifusi bado unakaribisha mvua itakapokuja irudishe mashimo yawe vile vile. Sasa barabara zile zinatumiwa na vipofu, wanatumia walemavu wengine, wanatumia wagonjwa na kadhalika na kadhalika barabara hazipitiki.

Kwa hivyo, naunganisha hapa kwamba na hili nalo lishughulikiwe ili wananchi waweze kama wanafanya michezo ndani mle watembee kwenye barabara zao ndani mle baadae waende kwenye viwanja vyao. Pia na viwanja vilioko kwenye majimbo viimarishwe ili tupate wachezaji bora kwani uzalishaji mkubwa wa wanamichezo unatoka huko.

Kwa hiyo, viwanja vile vidogo vidogo viliopo viangalie na wizara husika pamoja na Wizara ya Fedha ili michezo iweze kuendelea katika nchi yetu na sisi tutoe wachezaji bora waweze kuwa wachezaji wa kimataifa wapate ajira huko.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naingia kwenye utalii. Utalii yamesemwa mengi wengine wamependekeza utalii wa mikutano *conference tourism*, wengine wamependekeza utalii wa ndani. Mimi naongezea kidogo tu hapo kusema kuna kitu siku hizi kimeingia duniani, wanaita utalii wa kiafya ambao zile wanaziita *International Healing Center* nawaomba wawakilishi wenzangu waingie kwenye *internet* waangalie nini *International Healing Center*.

Hizi ni sehemu ambazo kwa kweli zinakuwa ni kama vituo vya afya ambavyo vinakaribisha watu waliopata *frustration*, kwa sababu huko Ulaya kuna majitu yana fedha zao nyingi sana wanatafuta mahala pakuzitumia, sasa matokeo yake wanapata hata *frustration*, wanapata *stress*, wanapata mambo mengi.

Kwa hiyo, hizi *International Healing Center* zinahusika na kuwahudumia watu wa namna hiyo na wakijua kuna kituo kama hicho hapa Zanzibar na kwa uzuri wa Zanzibar ulivyo na kwa sifa iliyonazo itapata watalii wengi matajiri watakuja hapa, mradi tu yale mahitaji ya *International Healing Center* yawepo na yawekwe kwenye sehemu hizo.

Niende haraka haraka kwa sababu muda nadhani unakwenda. Sasa naingia kwenye afya tuna hospitali ya Mnazi Mmoja, tuna hospitali nyengine za binafsi na kadhalika. Nasema huduma zinazotolewa nadhani sasa hivi umefika wakati wale wanaotoa huduma zile waangaliwe ipasavyo.

Mimi mwenyewe nina mwanangu bahati mbaya alipata mtoto wake mgonjwa akaenda hospitali kule Mnazi Mmoja nimeyashuhudia. Kwa bahati mbaya mtoto yule alikuwa ni mgonjwa sana, sasa katika kutapatapa yule mtoto akawa analia sana, akaniambia baba nisaidie mwanangu siku hizo sio leo, nisaidie mwanangu kuna daktari mmoja pale akasikia yale maneno kijana, kijana. Basi alimwambia mimi nitakuachia maiti wako sasa hivi niondoke hapa unanifanyia

zogo tu, sasa hii sio lugha nzuri kabisa kwa mtu aliyeaminiwa kwenye chombo cha afya kama kile kufanya mambo kama yale.

Mimi kwa kweli niliyaziba sikutaka kuripoti popote kwa sababu niliona yule ni kijana labda hajui maadili ya kazi yake, lakini mimi nasema hapa kwamba madaktari wa namna ile lazima washughulikiwe.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye hospitali zetu hizi, kuna kitu kinaitwa *hospital waste* (mabaki ya hospitali), mabaki ya binadamu ni mabaya sana yanaambukiza magonjwa vibaya sana yakikosa kuwa-*dispose* kwa uangalifu yanaweza yakaleta madhara makubwa. Sasa hapa Zanzibar nimeshaona baadhi ya sehemu utakuta *bandage* la kidonda limetupwa sehemu ambayo haistahiki. Utakuta *syringe* imetupwa mahala ambapo haistahiki, bahati mbaya mtu kenda kajichoma ile si ndio anapata hiyo *AIDS* au anapata maradhi mengine. Tunawaomba sana mahospitali yetu haya yaweke sehemu maalum za kuchomea mabaki haya ya wagonjwa…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa angalia muda wako, malizia…

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti: Naziomba sana watafute *incineration* ambazo kwa kweli zitasaidia kuchoma na wasichomee hapa Mjini kwa sababu huu moshi unakuwa na *heavy metals* ukiendelea kuuvuta, kuuvuta, kuuvuta kuna miaka ya mbele utapata maradhi ambayo kwa kweli huwezi kuamini umeyapata vipi. Utaanza kusema umerogwa, umefanywa nini, umefanya nini.

Bahati mbaya muda umekwisha sikuingia kwenye kilimo, uvuvi, tawala za Mikoa lakini kwa vile wenzangu na wao wamechangia na muda wangu huu naambiwa umeisha naheshimu sana muda. Napenda kurejea tena kuipongeza sana, sana bajeti hii ni bajeti nzuri narudia kumpongeza Mhe. Rais kwa kutoa muongozo, alitoa muongozo kwenye uzinduzi wa Baraza hili na matokeo yake tumepata bajeti hii ambayo ni ya sifa kabisa. Kwa hiyo, nawapongeza sana na ahsante sana kwa kuniruhusu. (*Makofi*)

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana awali ya yote na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai tukaweza kukutana mahala hapa. Lakini pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe mwenyekiti kwa kunipatia na mimi fursa ili niweze kusema machache katika hotuba hii. Kabla sijaendelea na mimi naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein kwa ushindi mkubwa alioupata wa asilimia 91.4 katika uchaguzi wa marudio.

Pia nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Makamu wetu wa Pili wa Rais kwa kuendelea kuaminiwa na Mhe. Rais ili awe kiongozi wetu katika Baraza hili. Lakini pia nichukue fursa hii kuwapongeza mawaziri wote waliopata uteuzi wa Mhe. Rais pamoja na Manaibu Waziri akiwemo Mwanasheria wetu Mkuu wote nawapongeza kwa kupata nafasi hizo na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atawapa nguvu na uwezo waweze kulitumikia taifa hili.

Pia nichukue fursa hii adhimu kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, kwanza nimpongeze sana Mhe. Rais kwa macho yake ya kuona mbali katika kututeulia kijana huyu ambaye kwa muda mfupi tuliyoishi naye katika Baraza lakini anaonekana ni waziri mahiri, makini, mbunifu, msikivu, tunaomba Mwenyezi Mungu ampe nguvu na uwezo zaidi aweze kutekeleza majukumu yake kama alivyopangiwa. *(Makofi)*

Vile vile niwashukuru watendaji wake wote ambao alishirikiana nao katika kuandaa hotuba hii mwanana na wakaja kutuletea. Pia nampongeza kwa uwasilishaji wake mzuri kabisa ambao kwa yeyote aliyesikiliza alipokuwa akisikiliza basi aliweza kupata mvuto maalum wa jinsi alivyoweza kuwasilisha vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, katika shukurani zangu hizo niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Kaskazini kwa kuniamini na kunirejesha tena katika Baraza hili, ili nami nije niwatumikie na naomba Mwenyezi Mungu anipe nguvu na uwezo huo niweze kufanya kazi hiyo kama nilivyowaahidi.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwapongeza wanawake wote wa Zanzibar kwa juhudi zao kubwa kabisa wanazozichukua katika kujituma na kuitikia wito wa serikali wa kujipunguzia umasikini wakaweza kujishughulisha na miradi mbali mbali, ili kujikwamua wao na familia zao na kuacha utegemezi, wakaweza pia kuwasaidia kinababa katika kuzihudumia familia.

Mhe. Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu hili halitaki tochi, wanawake wameonekana kuchukua juhudi kubwa kabisa katika uzalishaji mali. Wanajishughulisha na ni watu ambao wanastahiki sifa na pongezi, lakini pia wanastahiki juhudi kubwa ya serikali iwaone kile kilio chao cha kuona basi wanapata misaada mbali mbali pale wanapohitaji ili waweze kuimarisha uzalishaji wao huo.

Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza kinamama hawa katika kazi zao wanazozifanya lakini ndani ya kazi zao hizi kuna changamoto ambazo

wanakabiliana nazo, naiomba serikali iwaangalie katika changamoto zao hizi waweze kinamama hawa kufanikiwa na kama mnavyosema ukimuelimisha mwanamke mmoja tumeielimisha jamii. Kwa hiyo, naomba serikali iangalie changamoto, kwanza kinamama wana changamoto wanazalisha mali lakini hawana masoko. Kwa hiyo, suala la soko ni suala la kuzingatia sana kwa sababu wanazalisha lakini baada ya kuzalisha vitu vyao hivi au bidhaa zao hizi hawana mahala pa kuziuza.

Kwa hivyo, serikali iangalie msaada wa kuwatafutia masoko hawa kinamama na kwa sababu wameonesha moyo wa uzalishaji mali hivyo tuweze kuwatafutia masoko ili waweze kujisaidia wao wenyewe lakini pia wataweza kulisaidia taifa lao kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, kinamama wanakabiliwa na ukosefu wa fedha za kutosha katika kusarifu zile bidhaa zao wanazozitengeneza ili zikaweza kuwa katika *standard* nzuri ya kuweza kuuza ndani na hata nje ya nchi. Kwa hivyo, Mheshimiwa nimuombe Mhe. Waziri kuliangalia hili mapungufu haya ambayo kinamama wanayapata na yanafanya kurejesha nyuma juhudi zao za uzalishaji mali, serikali ione kilio chao hiki na wawaongezee fedha pale ili wapate kusarifu bidhaa zao.

Mhe. Mwenyekiti, nikichukulia kama katika Mkoa wangu wa Kaskazini kuna waanikaji wa dagaa, kinamama hawa ni hodari na wanajishughulisha sana katika uanikaji wa dagaa lakini bado wanakumbana na changamoto mbali mbali na sasa hivi inaonekana wanakuja watu kutoka nje kulinunua dagaa lao, wanakuja watu kutoka Kongo. Inaonekana hii bidhaa hasa kama ina soko.

Kwa hiyo, serikali lazima iangalie pale pahala ambapo inaweza kusaidia kinamama hawa wakaweza kufanya vizuri na wao wakaweza kupata soko kubwa, zuri, ambalo litaweza kuleta tija.

Mhe. Mwenyekiti, pia niiombe serikali iangalie kinamama hawa ambao wanajishughulisha na wale ambao waliokuwa tayari wamepata uweledi wa juu kidogo, kuwapa fursa za kushiriki katika maonesho katika nchi zile za Kiafrika ili na wao kuongeza ujuzi wao lakini pia kupanua wigo wa uzalishaji mali wao.

Mhe. Mwenyekiti, kinamama tutakapowatoa hapa kuwapeleka katika nchi za wenzetu watapata kwenda kujifunza na wao, lakini watakuja kuwa wazalishaji wazuri na wao katika nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia niseme katika juhudi kubwa za kinamama bado kuna vitu ambavyo vinarejesha nyuma na hili sio jengine isipokuwa ni wimbi kubwa la udhalilishaji. Kwa hiyo, mimi naiomba sana serikali iangalie jinsi kinamama tunavyopata tabu katika kudhalilishiwa watoto wetu, naomba sana serikali ijikite katika kukinunua kile kifaa cha *DNA*, ili tuweze kuwagundua wahalifu hawa na wasiwe wanaepukwa kila siku kesi zinapatikana lakini hazifikii maamuzi yaliyo sahihi na bado udhalilishaji unaendelea. Naamini tukijikita katika kuwagundua hawa mambo haya ya udhalilishaji yataweza kupungua.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende katika msisitizo wa afya ya uzazi salama wa akinamama. Tunaomba serikali iangalie na mwenyewe Mhe. Rais tunamshukuru kwa hili kwa sababu yeye ameweza kututetea kinamama katika suala zima la uzazi salama basi tupatiwe vifaa na huduma hizi bure. Tunampongeza sana Mhe. Rais kwa hatua yake hiyo ambayo kaichukua lakini sasa tuendelee kuchunguzana kwa sababu bado kuna watu wanalalamika kwamba kunakuwa kunapatikana usumbufu katika hili. Kwa hiyo, serikali iwe makini ili kinamama hawa waweze kupata huduma hii vizuri na afya yao iweze kurudi vizuri ili tuweze kupata kinamama wazalishaji wa bidhaa katika nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nieleze katika suala zima hili la afya. Kuna masuala haya ya UKIMWI ambayo mara zote yanaombewa fedha nyingi lakini mimi niiombe sana serikali bado kuna tatizo kubwa ambalo hatujalishughulikia kwa umakini. Kwa sababu ili maambukizi haya ya UKIMWI yaendelee kupungua kwa kasi kwanza tunatakiwa sisi wenyewe tujilinde kwa kujiepusha na zinaa, lakini pia serikali isimamie kuona vile viashiria ambavyo vinasababishwa na suala hili litakalopelekea zinaa basi kuvizuwia.

Kwa sababu kama hivi sasa kunaonekana kuna mitindo ambayo inaonekana hata katika waigizaji wetu katika sanaa inaonekana hatuko makini kuziangalia zile sanaa zinazoelimisha hasa na sio zinazochangia katika kupotosha. Kwa hiyo, mimi niiombe sana serikali iangalie sana suala hili kuweza kuepukana na vile viashiria ambavyo vinatupelekea kufikia katika hilo suala la UKIMWI.

Pia kuangalia mila, silka na utamaduni wetu. Mila, silka na utamaduni wetu unapotea na haya ndio yanayosababisha matatizo mengi baadae yanajitokeza. Kwa hiyo, mimi bado naiomba serikali, tuliomba hapa sheria ya mavazi iletwe ili tuweze kuwa na mavazi mazuri ambayo yanaendana na mila na desturi zetu. Kwa hivyo, bado tunasisitiza vitu hivi viendelee kuletwa ili na sisi viweze kutujenga katika maadili yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niungane na wale wenzangu wote ambao wamesema jinsi ya uvujaji wa mapato katika serikali na mimi naungana nao. Ni kweli serikali lazima ijikite katika kuzuwia uvujaji huu wa mapato na hili mimi nalisema kwanza, pia iangalie pamoja na usajili wa vyombo vya moto, lakini usajili wa vyombo vya baharini kuna vyombo baharini bado ukitizama mashua zetu hizo nyengine hazina usajili. Serikali bado iangalie suala hili lakini pia kuwa na doria katika zile bandari bubu ambazo zinasababisha kupatikana uuzwaji wa mafuta ya magendo na bidhaa nyengine zinazotoroshwa huko pembeni pembeni.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee katika kuipongeza serikali katika juhudi zake kubwa za kuona imeweza kulisimamia suala zima la malaria, tukaweza kupunguza kazi ya malaria katika nchi yetu lakini pia ndani ya upunguzaji huu wa malaria.

Zamani mimi nilikuwa naona katika upigaji ule wa dawa za malaria niliona wale wapiga dawa wanapiga mpaka labda katika vyoo. Kwa sababu katika vyoo kuna maambukizi, kuna vimelea vingi vya mbu au katika makaro, lakini siku hizi naona kukipigwa sioni kama sehemu hizo zinapigwa dawa au ilikuwa pia katika vidimbwi vilivyotuzunguka karibu ya majumba vilikuwa vikipigwa dawa, lakini siku hizi naona dawa inapigwa katika kuta tu basi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba serikali bado iangalie kwa sababu hili ni suala ambalo serikali imejitahidi kwa hiyo iendeleze jitihada zake hizo kuona tunafanikiwa.

Pia niiombe serikali kukemea kwa vile vitendo ambavyo vitaonekana vinakwenda kinyume kwa sababu serikali imejikita katika suala zima la kuwapatia wananchi wake vyandarua, lakini utakuta vyandarua hivyo siku hizi vimekuwa ndio vinajengewa uzio wa kuoteshea mboga mboga. Jamani huku ni kurejesha nyuma serikali jitihada zake ambazo inazifanya. Kwa hiyo, mimi naomba kwamba tujikite katika hilo ili tuone zile juhudi za serikali basi zinafikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia niseme kuhusu kilimo. Mhe. Rais alipokuja hapa katika kutuzindulia Baraza katika hotuba yake ya uzinduzi alikazia kilimo kile cha *green house* ambacho akasema atakipeleka kila wilaya. Mimi naiomba serikali kwa juhudi hizi ambazo imeamua kuzileta kwa hiyo iungane na wawakilishi wa majimbo katika kuuhamasisha mradi huu ili wawakilishi wahamasishe vijana wetu ambao wamo katika maeneo yetu ilimradi huu utakapokuja basi badala ya ule ambao mwenyewe Mhe. Rais katutengea na wawakilishi na wao waweze kuzalisha pale kwa ajili ya kufanikisha mradi huu. Kwa sababu mradi unaonekana una tija kubwa tunaweza tukapata masoko ya ndani, lakini

tunaweza tukapata masoko ya nje ya nchi. Kwa sababu kilimo chake kinaonekana kina tija kubwa.

Kwa hiyo, tuchukue fursa hii kuwahamasisha wawakilishi wa majimbo mradi huu utakapokuja na wao waweze kutumia fursa hii ili tuweze kupunguza ile kasi ya ajira ya vijana wetu, wakipata kujikita vijana wetu katika kilimo hiki wanaweza wakapata na wao sababu ya kupunguza makali ya maisha.

Mhe. Mwenyekiti, pia nizungumzie kuhusu suala zima la bandari ambalo serikali inakusudia kuzijenga. Mimi nilikuwa naomba katika bandari zetu na *airport* zetu huwa kuna vitengo pale ambavyo vinahusika na uangalizi wa mimea na mifugo.

Kwa hiyo, mimi nasisitiza vitengo hivi viendelee kuwepo na viwe makini. Kwa sababu tunaweza tukaja tukapoteza nguvu kazi za wananchi wetu ambao wanajitahidi kufuga, wanajitahidi kulima lakini akatoka mtu na mfugo huko ambao tayari umeshakuwa na ugonjwa ukaja ukaingizwa katika nchi yetu tukaweza kupata tatizo.

Sasa vitengo hivi utaikuta bandari ipo lakini hivi vitengo unaweza ukauliza ukaambiwa havipo au kama vipo hapana vifaa. Mimi nasisitiza vitengo hivi vikiwepo viweze kuwa na vifaa vyake lakini pia viweze kutoa huduma, kwa sababu unaweza kuliona tatizo dogo lakini likaja likaathiri sana katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka kusema machache tu katika bajeti hii kwa sababu najua bajeti zinakuja za wizara moja moja huko tutapata kusema mengi *Inshaallah*.

Baada ya kusema hayo nina jambo moja dogo nilikuwa nimeliacha, nilikuwa naomba sana serikali iangalie katika ushirika na *SACCOS*. Serikali huwa inapeleka fedha nyingi katika vikundi vyetu hivi ili kutoa mikopo, lakini ufuatiliaji unakuwa mdogo.

Kwa hiyo mimi naomba serikali ichukue juhudi za makusudi kuweza kufuatilia fedha hizi nyingi zinazotolewa, ili tuhakikishe wanaokopeshwa wanaweza kulipa kwa wakati na wenzao wafaidike na mikopo hii ili tuweze kupiga hatua.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na *Inshaallah* naomba Mwenyezi Mungu atufanikishe katika kuyatekeleza haya, atuwezeshe kwa manufaa ya wananchi wetu. Ahsante sana.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa kunipa nafasi hii adhimu ili nitoe mchango wangu katika Bajeti hii ya Serikali.

Nataka nimshukuru Allah *(S.W)* kwa kunipa nafasi hii tukufu nami kuchangia bajeti hii ya wizara mama katika serikali zote duniani.

Kabla sijaanza kuchangia bajeti hiyo nataka nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuchaguliwa kwa ushindi wa kishindo kabisa.

Pia nataka nimpongeze Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa kwake kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Spika wa Baraza hili tukufu kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Pia nataka nimpongeze Naibu Spika wa Baraza hili naye kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Baraza hili.

Nataka niwapongeze Wawakilishi wenzangu wa majimbo kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi katika majimbo yote ya Unguja na Pemba na wale wananchi wenzangu waliopata uteuzi kutoka kwa Mtukufu Rais Dkt. Ali Mohammed Shien.

Pia nachukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Ole, Ole yenyewe, Vitongoji, Mjini Ole, Uwandaji, Vikunguni pamoja na Gawani kwa kunichagua mimi kuwa Mjumbe wao wa Baraza la Wawakilishi.

Vile vile nachukua nafasi hii kumpongeza mke wangu mama Salma Mussa kwa kuishi na mimi vizuri na kunipa maliwazo ili niweze kukitetea Chama hiki cha Mapinduzi na kunitaka nisirudi nyuma, akitambua kuwa hiki ndio chama bora hapa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache nataka sasa niichangie bajeti hii ya serikali hasa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni wizara mama, wizara ambayo kwa sasa majengo yake ni machakavu na mengine ni mabovu kabisa hasa katika jimbo langu la Ole. Kwa hiyo, naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iangalie sana majengo ya skuli, mabanda yote asilimia 50 yanavujisha, yana mashimo si mazuri kwa kusoma watoto wetu wa kimapinduzi.

Hili ni tatizo kubwa na mimi kama ni Mwakilishi wa Jimbo la Ole nimeshaanza kuisaidia Wizara ya Elimu kwa kutoa mifuko ya saruji 100 kwa kusaidia majengo hayo ya skuli kama vile Vitongoji pamoja na Ole yenyewe. Mhe. Mwenyekiti, nataka nikuthibitishie kwamba watoto wetu watakapopata makazi mazuri katika mashule pamoja na walimu wazuri tutapata viongozi wazuri katika miaka ijayo.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kukwambia tena kwamba Wizara ya Elimu kwa sasa ina wanafunzi wengi katika mashule ya Unguja na Pemba lakini walimu ni kidogo mno. Kwa maana hiyo, tumeona tuwashawishi walimu ambao wameshamaliza mafunzo yao ya ualimu warudi kwenye mashule wakajenge taifa kuwasaidia watoto wetu ili tuongeze idadi ya walimu.

Sasa ninachotaka kukiomba naomba kwamba walimu wale tuliowamba ambao wamekubali kwenda kuwasaidia watoto wetu zikitokea ajira waangaliwe mapema. Na kwa sasa kwa kuwa walimu wale wanahitaji sabuni nimekubali mimi Mwakilishi wa Jimbo la Ole kulipa katika mshahara wangu asilimia hamsini kuwapatia walimu wale kumi na tatu kila kima mwalimu kima cha shilingi hamsini elfu ili waweze kuwasaidia watoto wetu.

Hili ni jambo zito kwa upande wangu lakini nimeliona ni jambo rahisi. Kwa hiyo, naiomba Wizara ya Elimu iwaangalie walimu wale na itakapofanya ajira wale walimu wawe ni wa mwazo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikiachia hapa nataka nirudi kwenye Wizara ya Ardhi pamoja na Ujenzi. Wizara ya Ardhi pamoja na Ujenzi naiomba sana iipatie viwanja Shehia yangu ya mjini Ole, kwa vile Shehia ile ina tatizo la makazi ya kudumu. Kijiji cha Mjini Ole ni kijiji kidogo sana lakini kina wakaazi wengi sana, kwa sasa watu wale wanaishi pacha pacha kama vile vidole vya miguu ni tatizi likitokezea maradhi ya kipindupindu.

Kwa hivyo, ipo ardhi ya serikali ambayo ilikatiwa watu wa Magereza au Chuo cha Mafunzo kwa ajili ya kulima na kwa bahati nzuri Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar haina wanafunzi wengi wa Chuo cha Mafunzo kwa sababu wananchi wa Zanzibar wameelimika si wengi sasa waokwenda tena Chuo cha Mafunzo ni wachache kabisa. (*Makofi*)

Kwa maana hiyo ardhi ile imekaa bure inatumiliwa kwa watu kuchungia mifugo ya ngombe, mbuzi na mambo mengine yasiyokuwa na tija. Kwa hiyo, naiomba serikali kupitia Wizara ya Ardhi kwenda kuikata eneo lile kwa

kuwapatiwa wananchi wangu wa Mjini Ole makaadhi ya kuishi pamoja na watoto wao na vizazi vijavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande mwengine nianachotaka kukizungumzia migomo. Migomo imekuwa tatizo kwa maendeleo ya sie Wawakilishi. Mimi Mwakilishi wako nimejaribu kufanyiwa migomo kwa kurejeshewa kile nilichokitowa kwa ajili ya kuwapatia umeme wananchi wa jimbo la Ole msikiti mmoja unaoitwa Mchangani. Baada ya kupeleka milioni nne na maguzo matano yamerejeshwa kwangu, hili nalo ni tatizo linaloweza kuonesha kwamba Wawakilishi tutapata mitihani tunakokwenda hasa sisi Wapemba.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nakuomba jambo hili nalo ulifikishe kwa Waziri wa Fedha alifikishe mahali panapohusika ili liangaliwe kwa macho mawili. Pamoja na kueleza hayo nataka nigusie Wizara ya Miundombinu hasa ile barabara inayotoka Ole-Vitongoji kumalizia Kengeja.

Barabara ile wamepewa watu wa Mawasiliano kuijenga huu ni mwaka wa nne hapana kilichofanyika ile barabara ina majipu. Kwa hiyo, ninachotaka kukwambia Mhe. Mwenyekiti, naiomba Wizara ya Fedha itafute mkandarasi wa kujenga barabara ile, Mawasiliano hawawezi kujenga barabara ya kilomita 139 hata siku moja. Huko Kengeja kuna milima kuna madimbwi na wao hawana zana. Kwa maana hiyo, barabara ile itakaa zaidi ya miaka kumi wengine tutakufa hatutapata kuitumia. (*Makofi*)

Pia Mhe. Mwenyekiti, katika barabara hiyo wakati inafanyiwa matengenezo wananchi wameharibiwa nyumba zao na wamepigwa picha kufanyiwa makisio lakini huu ni mwaka wa nne picha hazionekani, makisio hayaonekani watu hawaitwi majumba yameharibika, vipando vimengolewa, minazi, miembe, mihogo na huu ni mwaka wa nne hawaulizwi lolote.

Naiomba Wizara ya Fedha kupitia Wizara ya Mawasiliano kuwapatia malipo haraka wananchi hao, ili kuondosha mabovu ya nyumba zao yaliyobakishwa kupisha ujenzi wa barabara. Si vizuri kuona barabara inajengwa ndani ya mivungu ya kitanda.

Barabara inatakiwa iachiwe kilomita sita na zaidi ili ipate nafasi hasa barabara za kisasa na huko tunakokwenda. Barabara ya Ole Kianga umepita ndani ya mivungu ya vitanda vya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuelezao hayo nataka niuunge mkono Wizara ya Fedha na Waziri wa Fedha kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mussa Ali Mussa kwa sababu ya muda umebakia dakika kumi tutamalizia kidogo na Mhe. Masoud lakini baadae atamalizia jioni.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kusimama hapa katika kikao kitukufu cha Baraza la Wawakilishi.

La pili nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kupata ushindi wa kishindo wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2016.

Pia nichukuwe nafasi hii ya kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumchagua tena Balozi Seif Ali Idd kuwa Makamu wa Pili wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. (*Makofi*)

La tatu nimpongeze Mhe. Rais kwa kumteuwa Waziri wa Fedha Dkt. Khalid Salum Mohamed kafanya kazi nzuri ya kuhakikisha anatuchagulia Mheshimiwa ambaye atatusaidia kwa wakati huu ambao tunaelekea mwaka 2020.

Pia niwashukuru Wajumbe na kuwapongeza kwa kuchaguliwa kwao kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi sote tuliomo ndani huu.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii pia kumpongeza Mhe. Spika, kwa kuchaguliwa kwake kwa kura nyingi za kishindo. (*Makofi*)

Nichukuwe nafasi hii kumpongeza Naibu wake Spika pamoja na wenyeviti wote ambao tumewapigia kura katika ukumbi huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende moja kwa moja katika mchango wangu kwenye suala zima la umuhimu wa maji safi na salama. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuunda hili Shirika la *ZAWA*.

Kwa kweli wanafanyakazi nzuri sana wanajitahidi, lakini bado kuna tatizo katika maeneo yetu mbali mbali. Kwa mfano mimi katika jimbo langu visima vingi ambavyo vinatao maji vinaleta mjini vinatoka katika jimbo langu la uchaguzi, lakini kwa bahati mbaya eneo hili halifaidiki sana kwa hayo maji. Kwa hiyo, ningeiomba serikali iandae utaratibu mzuri kwa sababu visima

vinaanzia kwenye majimbo huko basi kuwe na *pipe* maalim ambayo itatoa maji kuwanufaisha wale wananchi ambao maji yanatoka katika eneo lao.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili kuna visima vingi sasa hivi *pump* zake ni mbovu. Kwa hiyo, ningeomba utaratibu *pump* zile zikatengenezwa, ili wananchi wetu wakapata kufaidika kwa maji safi na salama.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye hili hili la maji najua visima vingi vimechimbwa kwa muda mrefu *pipe* zake ni zile za chuma ambazo sasa hivi zimeshachoka maji mengi yanavuja njiani. Kwa hivyo, niombe serikali kupitia Wizara ya Fedha iandae utaratibu maalum ambao utakuwa wananunua mipira mipya ya kusambaza kwenye maeneo mbalimbali ambayo mipira hiyo inapita.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye suala la umeme, niwapongeze sana wenzetu wa *ZEC* wanafanya kazi nzuri lakini bahati nzuri shirika hili liko peke yake, pamoja na kujitahidi lakini wanaonekana kazi zao zinasua sua.

Ninaloliomba serikali iandae utaaratibu mzuri wa kuhakikisha wanapata fedha nyingi za kununua nguzo na waya. Kuna muda unakwenda katika Shirika la Umeme unaambiwa nguzo hakuna. Kwa hiyo, wananchi wanasubiri pamoja na fedha inakuwa tayari umeshatoa lakini unakaa zaidi ya miezi mitatu, minne usubiri kuungiwa umeme.

Kwa hiyo, nikuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha uandae utaratibu mzuri wa kuhakikisha Shirika lile linajiendesha liwe na fedha na nyingi za kujiendesha na hasa ukizingatia shirika lile liko pake yake kwa hapa Zanzibar. Pia ikiwezekana na wao wenyewe watu wa Shirika la *ZEC* waandae utaratibu wa kuwakosha wananchi kwa sababu wananchi wetu ni wanyonge hawana uwezo wa kulipia bili zike kubwa. Sasa niombe tu Shirika la Umeme waweze kuwakoposha wananchi wetu mbali mbali, ili na wao wapate kunufaika na huduma hii ya umeme.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende suala la kilimo. Kilimo kama alivyotangulia kusema wenzetu wa Wizara ya Fedha ni uti wa mgongo wa taifa hili. Lakini serikali ina nia nzuri ya kuhakikisha inasaidia wakulima wake. Lakini tatizo ambalo linaonekana linajitokeza serikali ina nian nzuri lakini inaonekana watendaji hawana nia nzuri....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe muda hauruhusu, naomba uje umalizie jioni tukijaaliwa. Waheshimiwa Wajumbe naomba niwatangazie kwamba wafuatao watakuwa ni wachangiaji wa jioni kwa kuanzia Mheshimiwa

aliemaliza sasa hivi atamalizia muda wake na baadae watachangia Waheshimiwa wafuatao:-

Mhe. Asha Ali Mussa, Mhe. Tatu Mohamed Ussi, Mhe. Nassor Salum Ali, Mhe. Miraji Khamis Mussa hawa watakuwa ni wachangiaji wa jioni kama itakuwa muda unaturuhusu.

Baadae naomba niwatangazie wenyeviti wa kamati za Baraza wanatakiwa baada ya kumaliza Baraza hili wakapitie na kujadili Mswada wa Sheria wa Fedha katika ukumbi mkubwa wa juu na Waziri wa Fedha na baada yake wale waliokuwa na uchaguzi wa UWAWAZA utafanyika ukumbi namba 3.

Baada ya hapo naomba niwatangazie rasmi kwamba katika ukumbi wetu huu leo tuna Mheshimiwa mwenzetu hapa mtoto wa Muasisi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Ali Abeid Aman Karume kwa umaarufu tunamwita Ali Karume kwamba leo anatimiza miaka 66 ya kuzaliwa kwake. Nasi Mwenyezi Mungu atujaalie tufike umri kama huu *inshaallah*. Ahsanteni. (*Makofi*)

Baada ya hapo naomba Wajumbe wote kusitisha Baraza hili hadi itakapofika wakati wa saa 11:00 jioni. Ahsanteni sana.

(Saa 6:56 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea. Tunaye Mhe. Masoud Abrahman Masoud na baada ya hapo atafutia Mhe. Asha Abdalla Mussa na baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Tatu Mohamed Ussi.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kuendelea na mchango wangu.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kwenye sekta kilimo. Sekta ya kilimo ni muhimu kwa uchumi wa wananchi wetu. Mhe. Naibu Spika, ndani ya maeneo yetu kuna kilimo cha umwagiliaji maji lakini pia serikali imehimiza kilimo cha kutegemea mvua. Mhe. Naibu Spika, kuna tatizo la matrekta. Nimuomba tu Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kila mwaka unapofika msimu wa kilimo, serikali huwa tunasikia inaagiza matrekta. Lakini inapofika msimu wa pili

utasikia bado kuna upungufu wa matrekta. Sasa nimuombe tu Mhe. Waziri, atakapokuja kutupa maelekezo hapa basi atwambie Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, sasa hivi tuna matrekta ambayo yanaendelea kufanya kazi katika maeneo yetu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kuna kilimo cha umwagiliaji maji. Sasa hivi kilimo cha umwagiliaji maji Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inahimiza sana. Na tunaambiwa ili tujitosheleze kwa chakula lazima tulime kilimo cha umwagiliaji maji. Ni kweli kilimo cha umwagiliaji maji kipo, lakini kiuhalisia ukenda huko mabondeni kilimo hichi kipo kwa asilimia ndogo sana. Ninasema hivyo kwa sababu ninatembelea huko kwenye mabonde ya mpunga wa umwagiliaji maji.

Kuna maeneo mengi ambayo visima vyake sasa hivi havifanyi kazi. Lakini tukikaa kwenye maofisi, Waziri na watendaji wanasema wanasema kuna kilimo cha umwagiliaji maji. Lakini ukenda huko mabondeni kiukweli uhalisia ni kuwa mashine hazifanyi kazi, unakuta maeneo tayari yameshatayarishwa kwa ajili ya umwagiliaji lakini umeme haupo. Kwa hivyo, niiombe sana serikali hasa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango atusaidie yale maeneo ambayo tayari yameshatayarishwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji. Kama kuna tatizo la umeme basi lilipitishwe ili wananchi wetu wapate kufaidika na kilimo hichi cha umwagiliaji, lakini pia na serikali nayo ilifikie lile lengo ambalo limekusudia.

Mhe. Naibu Spika, suala la mbolea. Nikichangia kwenye eneo hili kuhusu suala la mbolea, unapofika msimu wa kilimo huwa serikali inaagizishia mbolea. Na kawaida mfuko wa mbolea unafika hata shilingi elfu hamsini, lakini serikali inafidia mpaka mfuko mmoja unauzwa shilingi elfu kumi. Lakini la kusikitisha sana ambalo wakulima wengi huwa wanaliona kama ni tatizo. Mfuko mmoja wa mbolea wanapewa wakulima wanne wagawane. Bahati nzuri ninasema hivyo na yeye mwenyewe Waziri wetu wa Fedha na Mipango alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo. Kwa hivyo, tatizo hili analielewa na ninaamini atalifanyia kazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nitaendelea kwenye sekta ya afya. Sekta ya afya tumeambiwa kuna wataalamu ambao wanakwenda kusomeshwa. Lakini kwa bahati mbaya niseme kuwa kila mwaka huwa kuna ajira zinazotokezea. Lakini kama walivyosema wenzangu kuwa wale wanaokwenda kusoma kwa mwaka mmoja, wanaporudi wanaoajiriwa ni asilimia ndogo sana. Sasa serikali inakuwa tayari imeshawatolea fedha nyingi za kwenda kupata mafunzo huko walikwenda kuchukua elimu yao. Wakati wa ajira inakuwa haipatikani. Badala yake sasa wanaondoka hapa wanakwenda Tanzania Bara kufanya kazi na huku

serikali iliwapa mkopo wa kujisomeshea. Sasa sina uhakika Waziri atakuja kutwambia wale wanaondoka hapa kwenda kufanya kazi Tanzania Bara, mikopo yao wanailipa kwa utaratibu gani.

Mhe. Spika, kwenye Wizara hii hii ya Afya, Mhe. Rais ninakumbuka wakati wa miaka miwili iliyopita alikuja kwenye jimbo langu la sasa hivi. Jimbo la Bububu lakini kwenye Shehia ya Mbuzini. Alikuja kuweka msingi Kituo cha Afya cha Mbuzini. Katika mazungumzo yake alisema kituo hichi anategemea kiwe kituo cha afya cha Wilaya.

Lakini kwa bahati mbaya sana mpaka leo kituo kile hakijafanywa lolote au hakijaanza matengenezo ya aina yoyote. Katika ufunguzi wa Baraza hili Mhe. Rais alitaja kuwa jengo lile anatamani sana limalizike. Sasa Mhe. Waziri, utakuja hapa labda utuelekeze tu kuwa kuna mwelekeo gani ambao tunategemea kituo kile kitusaidia.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niende kwenye suala zima la ajira. Bahati nzuri mimi nilikuwa Diwani katika kipindi kilichopita, lakini nilikuwa mwenyekiti wa Halmashauri. Kwa bahati mbaya sana kuna Halmashauri nyingi za Unguja na Pemba, zina wafanyakazi wale tunaowaita vibarua. Wana zaidi ya miaka kumi wanafanya kazi kwenye Halmashauri zile. Lakini inapotokezea suala la ajira, wale wanaendelea kubaki *bench*. Niseme sisi kama Halmashauri tuna waajiri pale, lakini wanapoajiriwa na Halmashauri wanalipwa pesa ndogo sana. Ni aibu hata kuzisema. Maana yake kuna wafanyakazi wanalipwa mpaka shilingi sabini. Shilingi elfu sabini ukiziangalia ile nauli tu ya mfano mtu anayetoka Mbuzini kuja Halmashauri akenda akirudi, ukipiga hesabu ya mwezi na huo mshahara anaopata, basi nauli itakuwa kubwa zaidi.

Kwa hivyo, niiombe serikali kwa kupitia Waziri wa Fedha na Mipango na Tume ya Utumishi Serikalini, waangalie sana wale wafanyakazi ambao wamefanya kwa muda mrefu kwenye Halmashauri ni waanzilishi, wale vijana wafanya kazi ngumu za kuzoa taka na maeneo mengine. Lakini inapotokezea ajira basi anakuwa mtoto wa fulani na fulani ndiye anaajiriwa, wale wanaendelea kubakia pale pale bila ya kupata ajira.

Hivyo, naomba sana kwa kupitia Waziri wa Fedha na Mipango labda kuwe na mpango maalum wa kuangalia wale wafanyakazi wanaofanya kazi kwenye Halmashauri zile ili inapotokea ajira basi waajiriwe maalum kwa zile Halmashauri. Kwa sababu inapotangazwa nafasi ya kazi kupitia Tume ya Utumishi Serikalini, wanaoomba nafasi ile wanakuwa wengi sana. Kwa hivyo,

hatima yake wanapata wale ambao hata hukutegemea kuwa wataajiriwa, wanakuja watu wapya kabisa.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri, aangalie kwa jicho la huruma, iwe kuna nafasi maalum za watu waliokuwa wamefanya kazi kwa muda mrefu ndani ya Halmashauri. Lakini kwenye eneo hilo hilo, siyo Halmashauri peke yake lakini hata katika eneo langu la kazi la Kizimbani. Kwa kweli Kizimbani kuna wafanyakazi wanayohudumia yale mashamba ya Kizimbani, ni vibarua, yaani tunasema. Wanafanyakazi kazi kwa mkataba.

Lakini mikataba yao zinapotoka huwa wanachukuliwa wengine, wale waliokwishakufanya kazi pale kwa muda miaka kumi na tano, wengine miaka kumi, wanaendelea kuzeeka na hatima yake wanaachishwa kazi bila ya kupewa kiinua mgongo cha aina yoyote. Kwa hivyo, tumuombe tu Mhe. Waziri, atakapokuja hapa au tuombe tu Waziri wa Kilimo pale anapotoa ajira katika maeneo hasa yale ya Kizimbani, basi waangaliwe sana wale wafanyakazi ambao wanakuwa ni wafanyakazi wa kibarua wa kila siku. Na hasa ukizingatia hao vibarua wanaoajiriwa pale wanatoka mjini na huko mjini kuna gari kila siku ziwalete asububi saa moja na nusu, saa saba au saa nane ziwarejeshe mjini. Serikali inapata gharama lakini bahati nzuri na sisi tunapata lawama kwa wafanyakazi wa vibarua wa kulimia yale mashamba bado wapo katika maeneo yetu na wana uwezo mkubwa. Hivyo, nimuombe tu na Waziri wa Kilimo naye anapopata nafasi ya kutoa ajira, basi wawasaidie vijana wetu ambao wanakaa karibu na mashamba yale ya eneo la Kizimbani.

Mwisho, niseme ninaipongeza hotuba ya Waziri wetu wa Fedha na Mipango. Mimi pamoja na wapiga kura wangu wa Jimbo la Bububu tunaipitisha kwa asilimia mia. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ninakushukuru Mhe. Masoud. Sasa anafuata Mhe. Asha Abdalla Mussa na baadae ajitayarishe Mhe. Tatu Mohamed Ussi.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Kwanza nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuichangia bajeti hii ambayo imebeba kura ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar pamoja na serikali kwa jumla.

Pia, nimpongeze Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi kubwa anazozifanya kwa maendeleo ya wananchi wa Zanzibar. Lakini pia nimpongeze Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendeleza sera ya hapa, "Hapa kazi tu". Lakini ninapenda pia nimpongeze Mhe. Balozi

Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa kwake tena kuwa Makamu wa Pili wa Rais. Pia, nimpongeze Waziri wa Fedha na Mipango kwa umakini mkubwa aliounesha wakati wa kuwasilisha hotuba ya siku ya tarehe 23/05/2016 katika Baraza hili. (*Makofi*)

Pia, niwapongeze Waziri, Manaibu Mawaziri walioteuliwa. Pia, niwaombee kwa Mwenyezi Mungu awape wepesi katika kazi zao. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii ya serikali kwa kupitia vipengele vitatu. Kama walivyotangulia Waheshimiwa wenzangu. Wamezungumzia mambo mengi ambayo yanawahusu wananchi wa Zanzibar kwa jumla. Mimi nitazungumzia masuala matatu.

Suala la kwanza tutazungumzia kuhusu huduma ya maji safi na salama. Mhe. Naibu Spika, suala hili limekuwa ni changamoto kubwa kwa hapa Zanzibar. Na suala ambalo linawasumbua jamii yetu nzima. Hususan katika Jimbo langu la Kiwengwa. Wananchi wa Jimbo la Kiwengwa baadhi ya maeneo ikiwemo Shehia ya Kiwengwa, Upenja, Kisongoni, Mgambo, Mbaleni na Kwa Gube.(*Makofi*)

Shehia hizi zimekuwa zikisumbuliwa na tatizo kubwa la maji. Kuna visima vitano ambavyo vimechimbwa lakini mpaka sasa visima vile bado havijaweza kutoa huduma hiyo. Mhe. Naibu Spika, ninaiomba serikali kupitia suala hili ilitazame kwa kina au itafute mbinu ya kuweza kuliondosha tatizo hili. Kwani suala la maji limekuwa ni tatizo sugu. Hususan ukizingatia kwenye kipindi kijacho cha mwezi wa Ramadhan. Wakati Mhe. Balozi Seif Ali Iddi akiwa ni Mbunge wa Jimbo la Kitope, yeye alikuwa kila mwaka alikuwa akihudumia kuleta magari ambayo ya maji kuwahudumia wananchi wale. Lakini kwa hivi sasa tunaiomba serikali ifanye juhudi za makusudi ili kuweza kuwaletea maji kwa haraka wananchi wa Jimbo langu la Kiwengwa.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naishukuru Serikali ya Mapinduzi kwa kupandisha bei ya karafuu. Kwani inawapunguzia wakulima wale kuondokana na umaskini. Lakini kinachonisikitisha kuna wakulima wa mwani na katika Jimbo langu la Kiwengwa; Shehia ya Kiwengwa kuna vikundi vya akinamama ambao wanajushughulisha na kilimo hichi cha mwani. Lakini kwa masikitiko makubwa akinamama hawa wanajitolea nguvu zao kwa kulima kilimo hichi na kwa ajili ya kujipatia kipato chao ili kuondokana na umaskini. Tunaomba sana serikali nayo itazame kama ilivyopandisha bei ya karafuu basi na wakulima hawa wa mwani, basi wapandishiwe bei ya zao hili.

Mhe. Naibu Spika, pia, nitapenda kuzungumzia kuhusu uboreshaji wa huduma ya afya. Tunafahamu kwamba Mhe. Rais alitoa agizo kwamba wananchi wetu watapatiwa huduma ya afya kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja katika baadhi ya vipimo. Kwa mfano *CT-Scan, Ultra sound* na *X-ray.* Huduma hizi zitakuwa ni bure. Cha kusikitisha Mhe. Naibu Spika, wananchi wanakwenda pale lakini wakifika pale wanaambiwa huduma hizi hazipo, vifaa vimeharibika.(*Makofi*)

Naiomba serikali Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa tumeamua kuwapunguzia wananchi huduma hizi ziwe bure. Kwa hivyo, ningeomba sana viongozi wa kitaifa wangefanya ziara za kushtukiza kama wanavyofanya viongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili waweze kufika katika hospitali ile na kuona kitu gani ambacho kinachokwamisha huduma hizi zisiweze kupatikana. Kwani wananchi wetu wanapata shida sana. (*Makofi*)

Ukitazama kuna wananchi wetu wengine ni watu wazima. Anatoka shamba, anakodiwa gari mgonjwa anapelekwa pale na akifika pale huduma ile haipo. Anarudishwa tena. Kwa kweli linakuwa tatizo hili ni la usumbufu sana. Kwa hivyo, naomba serikali itazame suala hili na ilichukue kwamba ilione suala hili ni la msingi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, pia, ninapenda niishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuamua kwa makusudi katika mpango wake huu wa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa kuamua kwa makusudi kuzijenga barabara ambazo zimetajwa katika bajeti hii. Lakini pia ningeomba kwamba serikali nayo itazame na zile barabara za ndani ambazo zina usumbufu mkubwa kwa wananchi hususan wanawake. (*Makofi*)

Wanawake wanapata tabu sana wakati wapo waja wazito wanataka kwenda hospitali, wanaumwa na uchungu, wakati wa usiku katika maeneo kwenye jimbo langu kuna eneo linaitwa eneo la Boma, Mbaleni Kitope. Maeneo haya wananchi wangu wanapata shida kutokana na hali ya barabara kuwa chafu sana. Ningeiomba serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kuliangalia suala hili kwa kina ili wananchi wetu waweze kuondokana na tatizo hili.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu kuipongeza hotuba hii ya bajeti na kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba yake ambayo aliyotuletea hapa. Naipongeza na ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Asha Abdalla Mussa. Sasa anayefuata sasa hivi ni Mhe. Tatu Mohamed Ussi. Baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Nassor Salim Ali, baadae ajitayarishe Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kwa kunipa nafasi hii.

Kwa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tukakutana tena hapa jioni hii leo. Pia, niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba kwa kunichagua na mimi kuingia katika chombo hichi kikubwa cha maamuzi. Lakini nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na pia nimpongeze kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi zenye ushindi asilimia 91.4. (*Makofi*)

Pia, nimpongeze Mhe. Balozi Seif Ali Iddi ambaye Makamu wa Pili wa Rais kwa ujasirii wake na ukakamavu wake kwa kuweza kuitumikia nchi hii kwa uledi mkubwa. Pia, nimpongeze Spika, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuliongoza Baraza hili. Nisiwasahau Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri kwa kuteuliwa na Mhe. Rais kuliongoza Baraza hili. Nawaombea wawe na uvumilivu katika kujibu hoja za wajumbe. *(Makofi)*

Baada ya hapo nisiisahau familia yangu ambayo inanipa mashirikiano katika kipindi hiki kigumu nilichonacho. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu na mpango wa maendeleo. Nije katika sekta ya huduma. Kwenye mpango wa maendeleo wa mwaka 2016/2017, katika kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri, ukurasa wa 8 na 9 kifungu cha 20 kuhusu sekta ya huduma za umma, zipo tarakimu nyingi zinazoeleza hali ya ukuaji na ushukaji wa sekta ya huduma, ambapo mwaka 2014 sekta ya huduma ilikua kwa asilimia 10 ambayo imeshuka hadi asilimia 8. Mhe. Waziri, kaeleza sababu za upunguaji huo ni kupungua kwa sekta ndogo ya habari na mawasiliano kutoka asilimia 24. 7 kwa mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 7.7 kwa mwaka 2015. Kupungua kwa sekta ya biashara na ukarabati kutoka asilimia 13 mwaka 2014 na kufikia asilimia 1.2 mwaka 2015. Kupungua kwa sekta ndogo za taaluma ya sayansi na ufundi kutoka asilimia 43.4 hadi kufikia asilimia 15 mwaka 2015. Zote hizo zimechangia kushuka kwa sekta ya huduma.

Naomba Mhe. Waziri, atueleze kwa nini sekta hizi ndogo zimeshuka sana na kuna mkakati gani wa kuziimarisha ili sekta ya huduma nayo iimarike. Mhe. Waziri, katuwekea tarakimu pekee, lakini hajatuwekea sababu za punguzo hilo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo niende kwenye sekta ya mapato. Kwanza nitazungumzia mwelekeo wa mapato ya ndani ya nchi. Mhe. Naibu Spika, kama tunavyoelewa kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar alifanya jitihada zake na tukaweza kupata meli yetu ya Mapinduzi II. Meli ile ya Mapinduzi II unapoingia ndani ya meli unaambiwa meli hii ina uwezo wa kuchukua abiria kiasi kadhaa na pia ina uwezo wa kuchukua mizigo tani kadhaa. Lakini Mhe. Naibu Spika, la kusikitisha meli hii wanaingia abiria na mapato yanatokana na abiria tu, wakati meli yetu ina uwezo wa kuchukua mizigo kama vile gari na mizigo mingine mikubwa kwa lengo la kuongeza mapato ndani ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, la kusikitisha meli hii tangu ianze safari zake za kwenda Pemba na Unguja haijawahi kupakia mizigo kama vile gari na mizigo mingine mikubwa, isipokuwa ukiuliza unaambiwa kwamba hii meli mjengo wake uko chini na gati yetu kubwa, kwa hivyo, mizigo kama hiyo haipaswi kuingizwa katika ya meli ile.

Sasa je, Mhe. Naibu Spika, hatuoni kwamba hapa serikali inapoteza mapato, kwa sababu unapoitoa gari Unguja ukipakia kwenye meli ya Bakharesa unalipia shilingi 500,000. Sasa je, ingekuwa meli yetu hii ya Mapinduzi II inafanya kazi hizo, si tungeongeza mapato katika meli yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nina jengine ambalo limenikwaza ndani ya wilaya yetu. Kwanza niishukuru Wizara ya Habari, Utalii na Michezo na pia niishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kujenga viwanja vya kuchezea watoto, kwa Unguja Kariakoo na kwa Pemba walijenga Tibirinzi Pemba.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina masikitiko makubwa katika Wilaya yangu ya Mkoani, kwani unapofika wakati wa Skukuu watoto wetu hawana pakucheza, watoto wetu wanacheza barabarani ambapo ni pahali hatarishi kwa kweli. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, kutokana na hali hii nilikuwa naishauri serikali iweze kujenga viwanja angalau japo visifikie hatua kubwa kama ile ya Kariakoo na Tibirinzi, lakini iweze kutujengea viwanja ambavyo vitaweza kuwaweka watoto wetu pamoja kwenye mazingira yaliyo mazuri.

Mwisho, Mhe. Naibu Spika, nilikuwa na jengine, lakini Mhe. Bi Panya, kuhusu vikundi vya ushirika alilizungumzia vizuri mchana pale, kwa hivyo, sina haja ya kulirejea.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye sekta ya viwanda. Nchi yetu ina mazao mengi kama vile; maembe, mapapai, machungwa na mbirimbi. Lakini tunashindwa kuvitunza kwa sababu ya ukosefu wa viwanda. Mimi naishauri serikali iongeze

viwanda vya matunda, kwa sababu tukiongoze viwanda na halafu viwanda vyetu viliopo vikifanyakazi basi nafikiria tatizo la ajira kwa vijana wetu litapungua. Kwa hivyo, naiomba serikali ilifikirie suala hili la kutuwekea viwanda vya matunda.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kwa sababu mengi wenzangu wameshayazungumza sina haja ya kuyarejea. Kwa hivyo, na mimi naunga mkono bajeti hii, nimpongeze Mhe. Waziri, kabla sijaunga mkono pamoja na watendaji wake kwa umahiri wao wa kukaa wakatuletea bajeti hii ambayo tunaijadili hapa leo. Bila ya kuwa mahiri basi bajeti hii isingefika hapa na sisi tukaweza kuijadili. Mwenyezi Mungu awalipe kila lenye kheri. Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba, na mimi naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Tatu Mohamed Ussi. Mhe. Nassor Salim Ali na baadae atafuata Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kupata nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ambayo imebeba majukumu yote ya kuleta maendeleo kwa wananchi wetu wa Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya yote kwanza nichukuwe fursa hii kumpongeza Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kuweza kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar katika kipindi hiki cha mwaka 2015/2020. Vile vile, nimpongeze Mhe. Spika, pamoja na wewe Naibu Spika, pamoja na wenyeviti wote, kwa kuchaguliwa kwenu kutuongoza katika Baraza letu hili tukufu katika kipindi hiki ambacho tunakwenda nacho. *(Makofi)*

Vile vile, niwapongeze Mawaziri, Manaibu Mawaziri pamoja na wawakilishi wote walioweza kuteuliwa kumsaidia Rais katika majukumu yake ya kuleta maendeleo katika nchi yetu. Halikadhalika nichukuwe nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa kunichagua mimi na kukichagua Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi huu uliopita, nawahakikishia kwamba wataletewa maendeleo katika jimbo letu kwa viongozi wote waliochaguliwa katika Jimbo la Kikwajuni. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, nianze kwa kuchangia mchango wangu katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwenye sehemu mbili, tatu, na niwapongeze wajumbe wenzangu wote ambao wameanza

kuchangia na wamechangia katika nyanja nzuri sana ili kuleta maendeleo kwa kuunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, nianze na huduma za jamii. Katika kitabu chake Mhe. Waziri, ametuelezea mengi kwenye masuala mazima ya suala la jamii, hususani suala la elimu. Suala la elimu ni muhimu katika kupata rasilimali watu wenye ujuzi na maarifa, kwa kuzingatia hili serikali ipo haja ya kuangalia kwamba inaimarisha shule zetu, nichukuwe fursa hii kuipongeza serikali hasa ukiangalia kwamba tuna majengo 10 ya ghorofa ambayo yameandaliwa kujengwa katika shughuli mbali mbali, ikiwemo shule ya Rahaleo ambapo hii iko katika maeneo ya Rahaleo ambayo ni skuli ya Mwembeshauri. Ni imani yangu kwamba yale mapendekezo ya Mhe. Rais ya kuzitaka skuli zile kuwa skuli moja, lakini kuwa na majina A, B na C, mpango ule nadhani ni mzuri na mimi niunge mkono wazo lile la Mhe. Rais kuitwa skuli ya Rahaleo A, B na C. Huu ni mpango mzuri na nina imani kwamba serikali yetu katika kuendeleza maendeleo kwa wananchi wake na kuwapa elimu vijana wetu katika mwaka huu yatakuwa ni kipaumbele cha kwanza katika kuimarisha suala la elimu.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye sekta ya utalii. Sekta ya Utalii ni muhimu sana hasa kwa uchumi wetu wa Zanzibar. Mhe. Simai Mohammed Said, alieleza kwa kina na mimi niunge mkono yale mapendekezo yake ambayo alizungumza katika Baraza hili. Ukiangalia katika takwimu ambazo zinaonesha katika uingiaji wa watalii hapa Zanzibar kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, mwaka 2014/2015 watalii ambao waliingia Zanzibar ni takribani 294,243. Sasa ukizingatia takwimu zinazoonesha kwa mwaka 2015, utaona kwamba kuna mapungufu makubwa. Katika mwaka 2015 watalii ambao waliingia Zanzibar takribani ni 3,111,891, kwa hivyo, utaona pale kwamba kuna mapungufu. Sasa ni vyema Mhe. Waziri, atakapokuja atueleze ni sababu zipo ambazo zimefanya kupungua kwa watalii katika kipindi hiki. Ili kuweza kushajihisha Mhe. Simai Mohammed Said, alizungumza kwamba lazima tujitangaze, na Waswahili wanasema 'biashara itangazwayo ndiyo itokayo'.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi kilichopita tulikuwa katika masuala ya uchaguzi. Lakini hali nzuri ya usalama na amani kwa nchi yetu ilikuwa ni ya hali ya juu. Sasa ni vyema kuwahakikishia watalii kwa nchi mbali mbali kwamba Zanzibar ni tulivu, ni ya amani ili watalii waje kwa wingi na kuweza kupata fedha za kuendeleza katika maslahi ya taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni visiwa, yaani Unguja na Pemba, lakini ni visiwa ambavyo vina mvuto wa aina yake, mbali na mvuto wa aina yake lakini ni

visiwa ambavyo vina amani na utulivu. Wazanzibari ni wastaarabu, wanapenda watu na Wazanzibari sote tukiwa wamoja tunawapenda wageni. Sasa ni vyema Mhe. Waziri wa Fedha, tukamuwezesha vizuri zaidi Waziri wetu wa Habari, Utalii na Michezo ili kuweza kupata fedha na kuitangaza Zanzibar, kwa sababu bila ya kumpa fedha Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo basi itakuwa ni yale yale. Kwa hivyo, ni vyema tukamuwezesha Mhe. Rashid Ali Juma, ni mtu ambaye anaangalia mbali kweli kweli, namkumbuka tokea alikuwa katika mashirika yale ambayo yalikuwepo, alikuwepo Manispaa kafanya vizuri, alikuwepo *ZSSF* kafanya vizuri. Kwa hivyo, ni mtu makini na ambaye anajali na anaangalia maendeleo ya wananchi wake na Wazanzibari kwa jumla. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikitoka katika sekta ya utalii, nije kwenye sekta ya michezo. Sekta ya michezo pia ni sekta muhimu sana ya kupata ajira kwa vijana, michezo ni afya na michezo ni uunganishaji wa watu wa aina mbali mbali. Sasa sekta hii ni vyema tukaipa kipaumbele. Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitatu, minne au mitano iliyopita kweli sote tunafahamu kwamba sekta ya michezo ni sekta ambayo imekwenda chini sana. Lakini kutokana na mikakati ambayo nina imani kwa waziri huyu ambaye ninamfahamu, katika kipindi cha miaka miwili au mitatu tutakuwa tuko juu sana. Lakini bila ya kuwezeshwa basi hatuwezi kufika popote. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sote tunafahamu kwamba michezo ni kitu ambacho kinaunganisha watu wa tabaka mbali mbali na hasa ulimwenguni kote tunakokwenda, michezo inaunganisha watu wa aina mbali mbali, sasa ni vyema tukawekeza huko. Hasa ukizingatia kama nilivyozungumza kwamba michezo ni sekta ambayo inaunganisha jamii, inatoa ajira kwa vijana na vile vile, sekta ya michezo ni afya.

Kwa hivyo, niiombe sana serikali yetu chini ya kiongozi imara mwenye kujali michezo, mwenye kujali wananchi wake na mwenye kujali taifa lake Dkt. Ali Mohammed Shein. Nina imani nyinyi ambao mmechaguliwa kumsaidia Dkt. Ali Mohammed Shein basi mtafanyakazi kwa bidii na kwa maarifa na mipango endelevu ya kuimarisha miundombinu, michezo na hali ya maisha ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, leo asubuhi nimshukuru sana kaka yangu, rafiki yangu Mhe. Machano Othman Saidi. Mhe. Machano, alitoa mfano kwa wenzetu Tanzania Bara jinsi ambavyo wanathamini, wamewawezesha makocha wetu wazalendo wa Tanzania kwa kuwapa ajira na mikataba, hili ni changamoto kwetu. Mimi nina imani kwa serikali hii ninavyomfahamu Dkt. Ali Mohammed Shein,

ninavyomfahamu Balozi Seif Ali Iddi, ninavyokufahamu wewe Waziri wa Fedha na Mipango na ninavyomfahamu Sheikh Rashid Ali Juma ambaye ni Waziri wa Habari, Utalii na Michezo, basi nina imani katika kipindi kifupi kinachokuja makocha wetu wa Zanzibar, hawa hawa wazalendo watapata ajira na mikataba kwa kuimarisha michezo yetu hususani mpira wa miguu Zanzibar, pamoja na michezo mingine.

Mhe. Naibu Spika, juzi takribani kama mwezi mmoja hivi, nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo, kwa kuweza kufanya dhifa katika sekta ile ya riadha, ni sifa kubwa ambayo tumeletewa hapa Zanzibar kwa vijana wetu na sote tunafahamu hilo, ni vyema vijana wetu hawa tukawatunza na kuwapa mafunzo ya aina mbali mbali, kutuongoza zaidi huko mbele katika mashindano ya kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, nije katika suala zima la kutafuta wafadhili. Bila ya wafadhili basi sekta ya michezo haiwezi kwenda mbele na bila ya kuangalia kwamba tunakwenda wapi, kwa faida ya vizazi vyetu, kwa faida yetu sisi wenyewe na faida ya taifa letu. Ulimwengu wa sasa wa michezo tulionao ni lazima kutafuta wafadhili na bila serikali kulivalia njuga hili, hasa ukizingatia vyama vyetu vya michezo ni masikini, havina mwelekeo, vyama vyengine vinakwenda tu hapa ndipo hapa sipo, sasa bila ya serikali kulichukulia hatua na kuangalia kwamba inatafuta wafadhili kuwawezesha vyama vyetu vya michezo hatutokwenda mbele, sasa ni vyema Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, kuunganisha nguvu zenu kuhakikisha kwamba Zanzibar tunapata wafadhili ili kuendeleza michezo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo nije katika suala zima la vijana, Ajira kwa vijana ni suala ambalo la kutiliwa mkazo sana, hasa ukizingatia kwamba vijana waweze kujiajiri kwa sababu ya tatizo la ajira kwa Zanzibar, lakini tuwawezeshe ili waweze kupata ajira na kujiajiri wenyewe. Katika jimbo la Kikwajuni ambalo zamani lilikuwa jimbo la Rahaleo tumebahatika kuwa na kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo pale, ambacho mwezi unaokuja tutakuwa tunatimiza miaka kumi tokea kuanzishwa kwa kituo kile.

Mhe. Mwenyekiti, kituo kile kilianza kidogo kidogo, lakini kwa bahati nzuri kimezalisha vijana ambao wamepata ajira kupitia kituo kile vijana wengi wamesoma pale, wamejifunza suala la useremala, mamejifunza mambo ya kushona, mambo ya kupika mpaka wapishi wa mahoteli mbali mbali wametoka pale sasa hivi. Sasa niiombe Serikali kuweza kuiunga mkono kituo kile na kukiendeleza zaidi ili kuweza kusaidia vijana wetu kujiendeleza na kutafuta ajira kwa kupitia kituoa kile. Mhe. Waziri wa Elimu, namfahamu sana na najua

kwamba ni muelewa na hili analifahamu ili aongeze nguvu kituo kile ili kiweze kujiendeleza na kuzalisha vijana zaidi na kuondokana na tatizo la vijana wetu kukosa ajira.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo, nije katika suala zima la tabia nchi, yaani mazingira, kabla sijachangia hili kwanza nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya katika kuweka mazingira bora katika maeneo ya Maisara, Kilimani bondeni pale, mradi ule ulikwama kwa muda mrefu, lakini kwa juhudi ambazo zimechukuliwa na Serikali hii pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mradi ule tayari umeshaanza, tayari mikoko inapandwa na hii ni juhudi ya Serikali ya Dkt. Ali Mohammed Shein. Nimpongeze sana dada yangu Mhe. Salama Aboud, kwa juhudi zake ambazo amezianza kwa kazi nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, ukenda pale sasa hivi tofauti na kipindi kilichopita, hali ya mazingira imekuwa inaendelea kuwa nzuri mikoko inakwenda vizuri na programu ya kujenga ukuta iko vizuri fedha zimeshapatikana, kwa hivyo, niipongeze Serikali kwa juhudi nzuri ambayo imechukua. Vile vile, nimpongeze sana Mbunge wangu Mhe. Masauni, kwa juhudi zake ambazo na yeye kazichukua ili kuunga mkono mradi ule ili kuweza kufanikiwa katika kuendeleza maeneo yale.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kuiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha, ni hotuba ambayo ina mipango mizuri na endelevu, ni mpango ambayo tuna imani katika kipindi cha miaka hii mitano Zanzibar tutafika mbali kwa sababu ukija masuala ya barabara tumejipanga vizuri. Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri katika kipindi hichi katika kamati ambayo ilibahatika kufanya ziara ni kamati ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, tulikwenda Pemba kule, mambo ambayo tuliyaona Pemba Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ni ya kusifiwa ni mambo mazuri mno, ukienda barabara ya Wete/Konde barabara ni nzuri safi na ya kupongezwa, ukienda barabara ya Wete/Gando tumekwenda kukuta barabara mpaka chini ya bahari.

Haya ndio maendeleo na ni wajibu wetu sisi kuunga mkono yale ambayo yanafanywa mazuri na niwaombe wananchi wetu wakati umefika huu ni kuunga mkono Serikali yetu kwa kuleta maendeleo, sisi sote ni ndugu na sote ni wamoja, tuachane na siasa hizi ambazo hazina msingi, tuiunge mkono Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Dkt. Ali Mohammed Shein, tuwaunge mkono Mawaziri wetu, tuwaunge mkoni viongozi wetu na Wawakilishi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mambo ambayo Serikali yetu wanayafanya ni makubwa na ni wajibu wetu sote wawakilishi niwaombeni tufanye kazi kuwaletea maendeleo wananchi wetu bila ya ubaguzi wowote, tusijali huyu *CUF* yule *CHADEMA*, yule *TLP*, yule *SAU*, tulete Maendeleo kwa wananchi wetu wote na haya ndio malengo ya Chama cha Mapinduzi, na hii ndio dhamira ya Chama cha Mapinduzi, katika chama ambacho hakina ubaguzi ni Chama cha Mapinduzi, sote tunafahamu hivyo. Kwa hivyo, ni wajibu wetu wananchi wa Zanzibar na Watanzania kwa ujumla kukiunga mkono Chama cha Mapinduzi kwa faida yetu sisi na vizazi vijavyo, hakuna chama chengine kinachopenda maendeleo na wananchi wake kama Chama cha Mapinduzi na hakuna Chama ambacho kinachotoa viongozi bora kama Chama cha Mapinduzi. Nina imani sote humu lengo letu ni moja kuwaletea maendeleo wananchi wetu wote. (*Makofi*)

Kwa hivyo, nimalizie kwa kusema kwamba naiunga mkono hotuba hii ya Waziri wetu wa Fedha kwa asilimia mia moja kwa faida ya taifa letu, kwa faida ya wananchi wetu na faida ya maendeleo yetu kwa wananchi wetu, nakushukuru sana Ahsante sana Mhe. Naibu Spika *(Makofi)*

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi jioni hii na mimi kuwemo katika orodha ya wachangiaji wa leo. Lakini kwanza na mimi niungane na wenzangu kwa kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar kwa awamu ya pili, lakini pia nimpongeze Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa uteuzi alioupata kwa kuliongoza taifa letu hili kwa kuwa mtendaji mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pia, niwapongeze Mawaziri wote walioteuliwa na Mhe. Rais na Manaibu Mawaziri, nimpongeze Mhe. Spika, na Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wa kamati kwa kutoa fursa ya kuja kuliongoza baraza hili. Niwapongeze sana Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi tuliochaguliwa kupitia majimbo, viti maalum kuja kuwawakilisha wananchi humu na naamini malengo yao waliyotuchagua tutayatimiza.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue nafasi ya pekee kumpongeza kaka yangu Khalid Salum kwa kuchauguliwa kuwa Waziri wa Fedha, lakini nimpongeze pia Katibu Mkuu pamoja na Makatibu Wakuu wengine, lakini Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kwa kujitahidi na watendaji wenziwe kutuletea bajeti hii ya Serikali kwangu mie iliyojitosheleza katika kuwatendea haki wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakuwa na michangio midogo sana kwa sababu sehemu kubwa ya michango yangu nimeitoa kwenye Kamati ya Wenyeviti wa

kudumu wa Baraza, lakini yako maeneo mawili matatu naomba nichukue nafasi hii kuyaongezea kidogo tu.

Kwanza eneo la Mapato, kama tunavyojua bajeti hii ili ifanikiwe vizuri basi ni lazima kazi ya ukusanyaji wamapato iwepo, kwa hivyo, yapo maeneo bado mimi nina wasi wasi nayo kidogo, kwa hivyo, naiomba Serikali kupitia Wizara ya Fedha na taasisi zake za ukusanyaji wa mapato hasa kwenye eneo la ukodishwaji wa mikataba ya nyumba zinazowekezwa kwa huduma za benki, benki sina tatizo nao, lakini nina tatizo kidogo kunako mikataba inayotoka kwa sababu kwa asilimia kubwa sana mabenki haya yaliyopo ndani ya Zanzibar majengo wanayotumia yanamilikiwa na watu binafsi, wao wanaingia mikataba na benki, lakini sina uhakika mikataba ile kama yale malipo wanayoyapata kupitia kudi ile kama na sisi tunapata kodi yetu ambayo itakuwa ni sehemu kubwa ya kuongezea mapato ya nchi yetu. (*Makofi*)

Lakini eneo jengine ni eneo la uvuvi wa bahari kuu nalo pia nasema naomba nilichangie bado nina mashaka napo katika eneo hili la uvuvi wa bahari kuu kwa sababu vibali tunatoa kwa meli kubwa zinazoweza kuvua katika eneo hili la bahari kuu, lakini tuna tathmini ipi baada ya kuvua, maana hatuwezi kujua idadi ya tani kama hatuna eneo au sehemu ya kuja kupimia tani alizozivua baadae ile meli ikaweza kuondoka. Kwa hivyo, bado tunatoa fursa ya maeneo yetu kuwapa wawekezaji hawa wakavua sijui utaratibu gani unatumika, lakini nasema utaratibu mzuri wa Serikali iandae utaratibu wa kutengeneza eneo maalum ili waje wapime tani walizovua samaki gani walioondoka angalau tutapata kujua lakini watapata kulipia sehemu kubwa ya kodi walizonazo.

Mhe. Naibu Spika, naomba nielekee kwenye Mashirika ya Umma, tumeona kwenye bajeti hii Mashirika mengi ya umma yanapewa ruzuku na si jambo baya katika Serikali, lakini sasa Serikali naiomba sote kwa pamoja na wale viongozi wa Mashirika tubadilike na tubadilike katika sura ya kuisaidia nchi, ziko taasisi zinapewa ruzuku lakini tathmini ya ukusanyaji wao mpaka leo tukijiuliza hapa hatuijui lakini zinakusanya mapato na ruzuku juu wanapewa, naamini iko taasisi moja kama Baraza la Manispaa, mimi nimshukuru sana Mstahiki Meya aliyekuwepo pale pamoja na maafisa wake, wanafanya kazi kubwa sana ya kujikomboa katika kutengeneza sura nzuri ya kulisaidia baraza lile.

Lakini mipango ambayo wanaipanga kuna sehemu inakwama kwa sababu tupo katika kusukuma gurudumu hilo la maendeleo kwa pamoja tutakuwa tunajua sehemu gani inakwamishwa miradi ile, walileta *concept* moja ya ujenzi wa *Shopping more Complex*, ni dhana nzuri na ni jambo kubwa ambalo kwa

wastani wakati wana muwekezaji wao utaratibu ukitumika na wakiweza kufanikiwa kujenga lile, basi miaka miwili mbele au mitatu hawa wanaondoka kwenye utegemezi, Serikali kuu baada ya kupeleka ruzuku itapeleka fedha zile eneo jengine la maendeleo, kwa nini tusiwape msaada na msukumo kwa jambo zuri walilolianzisha wakalimaliza kwa wakati lakini wakaondoka na masuala yale ya kutoa ruzuku hatua kwa hatua. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie katika eneo moja niliwahi kufuatilia sehemu zile anazokwenda Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, siku moja alikwenda kuwahutubia wafanyakazi wa Mahakama siku ya *Law Day* huko *Victoria Garden*, moja ya malalamiko waliyokuwa nayo wafanyakazi wale wa Mahakama ilikuwa ni *Scheme of Service* ya mshahara wao. Mhe. Rais kwa mapenzi makubwa sana aliwaambia suala lile analijua kama ambavyo analijua jina lake na ni kweli, watandaji wetu kama *Scheme* ilitengenezwa kwa kipindi kirefu kwa nini juhudi za kuwasaidia wenzetu wale ambao wanabeba muhimili mkubwa wa nchi yetu mpaka leo sehemu kubwa ya yale marekebisho angalau ata kama wameomba kumi basi wape mbili hasa kwa jitihada wanayoifanya.

Sasa niiombe Serikali kunako maeneo yetu muhimu kama yale basi tushirikiane katika kutatua changamoto kama zile, lakini kwenye bajeti hii nimesoma sana na nimeangalia sana eneo hilo huikuti nikasema niwasemee angalau inawezekana kunako bajeti za kisekta zile tukaja tukaliangalia kwa moyo mwengine.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa katika kuchangia kwangu leo naomba nilizungumzie suala la umuhimu wa *Diaspora* katika nchi yetu, zana ya *Diaspora* hii ilianza wakati wa Rais Dkt. Salmin Amour Juma au tuna kumbukumbu sahihi aliwahi kumteua mshauri wa Rais anayeshughulikia mambo haya ya uhusiano wa kimataifa, lakini alipokuja Dkt. Karume Rais Mstaafu nae pia alichagua Katibu Mkuu pale, Mhe. Rais wa Zanzibar akaendeleza dhana ile na kwa moyo mzuri tu akamteua Naibu Katibu Mkuu mpaka bajeti iliyopita 2015/2016 zilitengwa pesa za uanzishaji wa Sera ya *Diaspora*, sasa utakapokuja kufanya majumuisho naomba nipate jawabu kwa sera ile imefikia wapi. Lakini pia na tathmini ya kuwatambua, maana moja ya kuanzishwa *Diaspora* ni kuwatambua, kuwajua walipo, lakini kuwapeleka kwenye malengo yaliyokusudiwa, sasa tujue mpaka hatua hii tuliyonayo sasa Serikali imefikia wapi, maana katika jambo hili Mhe. Naibu Spika, lazima kwa pamoja tuunge nguvu za Mhe. Rais mpaka akilihutubia baraza hili la tisa aliligusia jambo hili kwa umuhimu wa pekee.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, atapokuja kufanya *windup* hii atuoneshe kwa sababu ndani ya kitabu hiki nimeangalia sijaridhika zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mwisho naomba na mimi niungane na wenzangu kwa kuiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala* kwa kutuwezesha leo kufika hapa tukiwa katika hali ya uzima na furaha. Pia, niishukuru familia yangu kwa kunipa *support* kipindi chote hiki kwa kuitafutia hali nzuri nchi yetu hadi hii leo. Vile vile, nimshukuru mume wangu kwa mashirikiano yake makubwa na ustahamilivu wake kuwa pamoja na mimi katika kipindi cha kutafuta hadi leo, nimshukuru sana. Pia, nimshukuru mama yangu pamoja na familia yangu kwa kuni-*support* juu ya suala hili, na mimi nawaahidi nitawatendea mema. Nawashukuru pia wajumbe wote wa UWT pamoja na vijana walioniwezesha leo mimi Zulfa kuitwa mwakilishi, nawashukuru sana na niko pamoja nao. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nianze kuchangia suala la *Airport*. Nimshukuru Mhe. Rais kwa kuona umuhimu wa kututengenezea *Airport* yetu ya Pemba, Waheshimiwa leo nina furaha kubwa kwa sababu Shirika la Ndege la *Precision* limeanza safari zake katika Uwanja wa Pemba. Kwa hiyo, kwetu sisi Pemba hiyo ni furaha kubwa sana. (*Makofi*)

Vile vile, nimshukuru Mhe. Rais kwa kufikiria fikra za kutanua uwanja wa *Airport* Pemba. Mhe. Rais, alilizungumzia suala la utanuzi wa *Airport* Pemba kwa sababu suala hili ni muhimu ukiangalia sasa hivi *Airport* ya Pemba ni mbovu, haina eneo la kutosha, eneo la abiria wanaosubiria ndege ni dogo. *Airport* ile haina eneo la watu ambao wanaenda kushindikiza, ukienda kushindikiza mgeni wako unaishia kusimama katika mageti na kuangalia, hamna eneo ambalo watu wanatakiwa kukaa. Kwa vile Mhe. Rais ameliona suala hili na katika Ilani yetu alilitaja suala hili kwamba atalitengeneza. Je, ni lini utanuzi huo wa *Airport* ya Pemba utaanza? Mhe. Waziri, nakuomba unipe jibu hili kwamba ni lini utanuzi wa uwanja wa ndege huo utaanza.

Mhe. Naibu Spika, pia, nichangie katika maeneo ya majenzi. Mhe. Waziri katika matumizi yetu tumeona kwamba ofisi nyingi za Pemba wanatumia majengo ya watu binafsi kwa ajili ya ofisi. Kwa mfano, Ofisi ya *DPP* Pemba, ofisi ya *ZIPA* watu hawa wanatumia majengo ya watu binafsi kwa ajili ya ofisi. Je, huoni kwamba hilo ni tatizo? Pia, ni kiasi gani cha pesa kinatumika katika

kukodia majengo hayo na wakati ofisi hizo wana maeneo ambayo wamepewa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa maofisi. Nahisi ipo haja hizo pesa ambazo wao wanaokodia hayo majengo zipelekwe katika ujenzi wa maeneo ambayo wamepewa ili fedha zile zisipotee kwenda kwa mtu binafsi.

Mhe. Naibu Spika, niende katika suala la taa za barabarani. Ni kwamba tunaona juhudi za serikali kwa wawekezaji wa taa za barabarani hapa Unguja, hayo ni maendeleo makubwa na hiyo ndio adhma ya Ilani ya Chama chetu cha CCM katika uchaguzi wake wa mwaka 2015, naamini taa hizo zitakapoingizwa zitaleta muonekano mzuri wa Zanzibar yetu. Lakini ujenzi huo sijawahi kuona katika maeneo ya barabara za Miji ya Chake-Chake, Wete na Mkoani na Zanzibar hii ni Unguja na Pemba kwa pamoja. Kwa hiyo, ningekuomba Mhe. Waziri wakati wa ujenzi wa barabara hii tu-*balance;* maeneo ya Unguja na maeneo ya Pemba ili tusilete sura mbaya kwa wananchi wetu wengine wanaotuangalia katika uletaji wa maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, pia, nizungumzie katika suala la uwekezaji. Ni muda mrefu sana tokea mwaka 1992 ilipotangazwa maeneo ya Micheweni kuwa ni maeneo huru ya uwekezaji. Je, serikali imechukua umuhimu gani wa kutumia maeneo hayo ya Micheweni katika uwekezaji? Kwa sababu naamini kwamba maeneo haya ya Micheweni yatakapotumika katika uwekezaji serikali yetu itajipatia pesa nyingi sana kutoka kwa wawekezaji na sisi pato letu linakuwa na tunaweza kufanya mambo muhimu ambayo yanahitajika.
Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia, lakini pia naomba masuala hayo niliyoyasema nipate majibu yake ili niweze kujiridhisha zaidi ya hapo. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa jioni hii ya leo ili tupate kuchangia mapendekezo haya ya bajeti na mapendekezo ya mpango wa uchumi wa maendeleo ya nchi yetu uliowasilishwa na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Malindi kwa kuniamini na kunipa kura nyingi za kishindo na kuniwezesha leo hii kuweza kuwepo hapa kuitumikia nchi yangu nikiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. (*Makofi*)

Vile vile, nitakuwa mwizi wa shukurani kama sitomshukuru na kumpongeza Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano

na Usafirishaji. Pia, nawapongeza wawakilishi wote ambao leo wamechangia kwa ufanisi kabisa hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Pia, nitakuwa mwizi wa fadhila iwapo sitowapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri ambao tumekuwa tukimsaidia Mhe. Rais kazi zake ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inapiga hatua kubwa ya kimaendeleo kwa muda mfupi *inshaallah*.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru sana mke wangu ambaye kwa kipindi chote hiki, ameweza kunistahamilia ninapokuwa ninafanya kazi hizi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, namwambia aendelee kuwa na ustahamilivu kwani sisi tumepewa dhamana ya kuwatumikia wananchi wetu, na ninahakikisha kwamba nitakuwa miongoni mwa wale viongozi watiifu na watumishi watiifu kwa serikali yetu *inshaallah*. Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, nianze kuchangia kwa ufupi tu hotuba hii iliyotolewa na wajumbe wameichangia, hasa kwa Wizara yetu ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nianze kumpongeza aliyekuwa akikaimu Mwenyekiti wa Wenyeviti wa Kamati hizi Mhe. Machano Othman Said ambaye alikuwa akimwakilisha Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa ushauri wake mzuri aliotupa, kusema kweli ushauri huo tutaufanyia kazi hasa katika mambo yanayohusu Wizara yetu ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa mambo ambayo ametushauri na ambayo ninahakikisha kwamba tutayafanyia kazi ni yale ya kuhakikisha kwamba tunaangalia umuhimu wa kutoza ada maalum kwa zile gari zinazoingia Mji Mkongwe. Sote tunaelewa kuwa Mji Mkongwe upo katika hifadhi ya *UNESCO* na kuna masharti yake maalum ambayo wametuwekea ili kuhakikisha kuwa huu mji unaendelea kuwa katika hifadhi hiyo. Miongoni mwa masharti hayo wametutaka kwamba tuhakikishe magari mengi yaliyokuwepo kule Mji Mkongwe yanapunguzwa uingiaji wake na vile vile ukaaji wake. Kwa hiyo, kama alivyosema Mhe. Machano kwamba, tutaanzisha utaratibu maalum wa kuhakikisha gari zile ambazo zinaingia zikiwa zinafanya kazi kule kwenye mabenki watu wale hatutawatoza ushuru wowote bali tutawapa vibali maalum vya kuingia kule Mji Mkongwe.

Vile vile, wapo watu wanaoishi kule Mji Mkongwe na wale tutaangalia kuwapa vibali maalum ili na wao wahakikishe wanafaidika na huo Mji Mkongwe. Pia, kuna watu ambao wanatoka sehemu za mbali wanakwenda kufanya ibada zao kule kama vile makanisa, misikiti wale nao tumewaekea utaratibu maalum wa kuwapa vibali. Kwa hiyo, ushauri wake huu tutaufanyia kazi na kwa kweli

tumeshaufanyia kazi na ninamuahidi tutaendelea na utaratibu huo ili kupunguza msongamano wa magari wa kuingia Mji Mkongwe. Suala lake la kuweka mizani kwa hivi sasa bado kwa Mji Mkongwe hatutoweza kuweka mizani, kwani kama tunavyojua tayari tumeshaweka masharti hayo na tunataka kuhakikisha magari makubwa yale yanapungua kuingia Mji Mkongwe kwani yanaleta uharibu wa barabara zetu zile.

Mhe. Naibu Spika, watu wengi wamechangia katika miundombinu tofauti na wana hamu kuhakikisha kwamba miundombinu hii tunahakikisha inafanyiwa kazi; wamezungumzia Miundombinu ya bandari, viwanja vya ndege na vile vile, barabara. Kama alivyosema mwenyewe Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwamba kuna changamoto nyingi, mwalimu wangu mmoja wa mambo ya utawala aliniambia katika maisha yako binaadamu lazima ukutane na vitu viwili; Changamoto na matatizo, mwalimu wangu yule aliniambia kwamba changamoto zinakabiliwa na matatizo yanatatuliwa. Kusema kweli changamoto hizi tutazichukua na kuzifanyia kazi.

Hapa wameelezea na nimshukuru Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, wameelezea kwa nini *Terminal II* mpaka sasa hivi haijamaliza. Alisema Mhe. Waziri katika kitabu chake hiki hapa ambacho ameelezea kila kitu humu cha mapitio ya hali ya uchumi 2015 Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo Zanzibar 2016. Ameelezea kwa ufasaha kabisa; nini tumefanya na tatizo gani lilotukuta kwa nini hatukufanya.

Kwa hiyo, na mimi naamini matatizo ya ukandarasi yaliyotukuta katika kutekeleza mradi wa *Airport* yamefanyiwa kazi na kama tulivyoahidi katika kitabu hiki kwamba wakati wowote akipenda Mwenyezi Mungu mradi huu utaendelea na kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu utakamalika kama ulivyopangwa.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, wameelezea changamoto walizokutana nazo bandarini, tunakubaliana nazo kuna kipindi cha Machi mpaka Mei ilikuwa meli zimefunga gati kwa mfululizo na ukiangalia kwamba bandari yetu ina uhaba wa vifaa, na pia eneo lile la bandarini lilikuwa finyu baada ya Bwawani kupata mwekezaji. Lakini tumejitahidi kadri ya uwezo wetu na hivi sasa tatizo la msongamano wa makontena matupu pale limepungua kwa asilimia 90.

Mhe. Naibu Spika, juhudi kubwa tumechukua kwa kipindi kifupi na hivi sasa kuna maendeleo makubwa hasa baada ya kuwataka wafanyabiashara kuhakikisha yale makontena matupu yanaondolewa haraka ili yasiwepo pale kusababisha msongamano.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, wamezungumzia kuhusu barabara zimetajwa hapa barabara ya Mkokotoni ambayo kusema kweli imeanzia hapa Kwanyanya mpaka Mkokotoni, barabara ile tayari imeshaelezewa katika kitabu chetu hiki cha bajeti kwamba ile barabara katika kipindi hiki cha bajeti kinachokuja cha 2016/2017 itatengenezwa kwa awamu hadi kukamilika kwakwe. Kwa hiyo, nawaomba sana wawakilishi wawe na subra na tunawahakikishia kwamba serikali yao hii ipo tayari kutatua kero zetu zinazohusu barabara, kwani tunajua kuwa barabara ni muhimu kwa usafirishaji wa wananchi, usafirishaji wa mizigo yao na vile vile ina umuhimu wake kwa kuchukulia watalii. Sehemu yenye barabara nzuri basi huduma zake zinakuwa nzuri na uchumi wake unakuwa kwa haraka.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, ningependa kuzungumzia barabara za Pemba, mimi mwenyewe ndio shahidi barabara za Pemba ni barabara za kupigiwa mfano, ni barabara ambazo zimejengwa kwa kiwango cha juu sana kiasi ya kwamba mtu yeyote akienda Pemba sasa hivi haamini kuwa ile ni sehemu ya nchi za ulimwengu unaoendelea. Sote ni mashuhuda barabara zilizojengwa kupitia *MCC* zimekuwa na kiwango cha hali ya juu, tumeshuhudia vile vile barabara zilizojengwa na wakandarasi wetu kama *MECO*, kama vile ya Wete/Gando, Wete/Konde ni barabara ambazo zimejengwa kwa kiwango cha hali ya juu kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kuna barabara ilikuwa na changamoto ya Ole/Kengeja yenye kilomita 35, barabara hii napenda kumuarifu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Ole kwamba tumeshaanza ujenzi wake na kama alivyosema mwenyewe tumeanza kwa Shehia za Ole/Kianga na tunakuja mpaka Mfikiwa kwa kuweka wenyewe wataalamu wanasema '*subgrade*', *subgrade* hii itafuatiwa baadae na '*subbase*'.

Kwa hiyo, namuhakikishia kwamba wataalamu wa *UUB* ni wataalamu wenye uzoefu wameweza kujenga barabara nyingi tu kule Pemba kutoka Michakaeni mpaka Gombani wamejenga wale wataalamu wetu wa *UUB*. Vile vile, hapa Unguja barabara nyingi za Mjini wamejenga *UUB* na barabara ya Bambi/Umbuji yenye urefu wa kilomita 5 ya Mhe. Mohammedraza, tumejenga wenyewe sisi kwa wataalamu wetu wa ndani. Kwa hiyo, nawaambia wawakilishi wawe na imani sana na wakandarasi wetu wa ndani wana uwezo wa kujenga barabara hii.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kulipwa fidia, yeye mwenyewe ni shahidi kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshaanza kulipa fidia, tulilipa awamu ya mwanzo milioni 30,000,000 na sasa hivi tumelipa mwezi wa Aprili milioni

60,000,000, kwa hiyo, kuna pesa kama milioni 91,000,000 tumeshawalipa wananchi hasa wa Shehia ya Ole/Kianga. Yeye alinipeleka na akanionesha mwenyewe kwamba kuna nyumba nyengine hizi wamelipwa fidia ambao wenyewe wamefurahi kwa sababu walisema thamani ya zile nyumba kusema la kweli ni za udongo na nyengine zilikuwa ziko chini ya kiwango, lakini kwa fidia waliolipwa wametushukuru sana na yeye ni mmoja wapo katika wale waliolipwa fidia.

Kwa hiyo, mimi nina imani *UUB* itapojenga ile barabara haitofika katika mivungu ya nyumba nyengine ambazo hazikujenga kwenye hifadhi ya nyumba. Nataka kuwahakikishia wawakilishi wote kwamba sisi tuna nia ya dhati kutaka kuhakikisha ahadi zote tulizotoa katika Ilani ya Uchaguzi wa CCM tunazitekeleza kwa vitendo. Na vile vile ahadi alizotoa Mhe. Rais kwa wananchi nazo tumezipa umuhimu wa kipekee na tutahakikisha ahadi hizo tunazitekeleza ipasavyo.

Mhe.Naibu Spika, mimi naomba sana wawakilishi wetu waendelee kutuunga mkono, wajue kwamba awamu hii ya saba ya Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, awamu ya pili tumekusudia kabisa kuwasaidia wananchi wetu kutatua kero zao mbali mbali na nina imani kubwa kabisa baada ya muda mfupi kero hizo zitatatuka na *inshaallah* tuko tayari kuhakikisha watu wote wanatuunga mkono bila ya kujali itikadi zao za chama.

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila nisimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa bajeti aliyotuletea, ni bajeti ya vitendo ambayo nina imani kabisa kwa umahiri wake mkubwa na uzoefu wake katika kada hii ya fedha na wizara alizozipitia hapo kabla atatuvusha salama na ile ahadi ya Mhe. Rais aliyosema kwamba mwaka 2020 tuhakikishe kwamba mapato tunayokusanya ni shilingi 800 bilioni, kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu tutaifika katika kipindi hiki kabla hata kufikia muda huo.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Malindi naiunga mkono bajeti hii na kuwaomba waheshimiwa wengine nao waiunge mkono, kwani hii ni bajeti ambayo ina dira kubwa sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima. Lakini pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi nami nikaweza kutoa mchango wangu katika Bajeti hii ya Serikali ya mwaka 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nitamke kwamba, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Chwaka tunaunga mkono bajeti hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ni imani yangu kwamba maelezo yaliyotolewa awali wakati wa uwasilishaji wa kitabu hiki yamekidhi na yameelezwa kwa kina kwa kiasi gani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Awamu ya Saba kipindi cha pili ilivyojidhatiti na kuhakikisha kwamba inadhibiti, kwanza inaongeza mapato ambayo yatakuwa yanaongezea shufaa na kupunguza ugumu wa maisha kwa Mzanzibari. Lakini pili serikali imejidhatiti kutumia ama kubana mianya ya upotevu wa mapato hayo, mategemeo yangu kwamba wajumbe wote wa Baraza hili tungeweza kuiunga mkono bajeti hii na kuiunga mkono serikali ili tuweze kuipa nguvu serikali kwa ajili ya kukamilisha malengo yaliyokusudiwa yakiwemo haya ya kuongeza mapato, lakini pia kudhibiti matumizi yasiyokuwa na tija pamoja na kushirikiana na serikali katika kuzuwia mianya ya upotevu wa mapato.

Mhe. Naibu Spika, bila ya shaka yoyote, sote ni wananchi na sisi ni mashahidi na mashuhuda wa kuona baadhi ya matendo yanayofanywa na marafiki zetu, washirika wetu, ama ndugu zetu katika kupelekea upotevu wa mapato ama kuwaelekeza wao jinsi gani ya kukwepa mapato hayo. Ni imani yangu kwamba sisi kama wawakilishi wa wananchi tutaweza kutumia fursa ya kuweza kuwaelekeza wenzetu kushirikiana na serikali yetu katika kudhibiti mianya hiyo ili mapato haya yaweze kuingia serikalini yaende yakatumike vizuri kwa manufaa ya wananchi wetu wote wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine la pili limezungumzwa kwa mapana sana suala zima linalohusiana na mradi wa usalama mjini, masuala mazina ya uwekaji wa *CCTV*, taa, pamoja na vifaa vyengine vya kiulinzi. Ni kweli ukiangalia katika nadharia unaweza ukaona kama serikali imetumia fedha nyingi sana shilingi 18 bilioni katika mradi huu. Lakini ningeomba Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, likaendelea kuvuta subira ili ufike wakati sasa tutakapowasilisha bajeti Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ tuwape nafasi ya kuwasikiliza. Matarajio yangu kwamba maelezo yatakayotolewa yatakidhi na yatatosha na sote tutashawishika na kuona hoja na haja ya serikali kuweza kufanya matumizi haya katika uimarishaji wa usalama wa mji wetu.

Tunapozungumzia masuala mazima ya usalama, maana yake tunazungumzia nafasi ya uwekezaji, nafasi ya kukuza uchumi, tunazungumzia nafasi ya kulinda na kudumisha miundombinu iliyopo, kinyume ya kuweka usalama,

maana yake wewe unaruhusu yale yote ambayo umeyafanya katika harakati za maendeleo unampa mtu nafasi ya kuweza kuyavuruga. Kwa hiyo, matarajio yangu kwamba tutawapa nafasi wizara husika watatupa maelezo ya kutosha na katika hilo naamini yatatosheleza kwa kuweza kuona umuhimu na busara za serikali katika kutumia fedha kukamilisha mradi huu muhimu katika kuweka usalama wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, jengine ningeomba tu, sote tumeisifu serikali katika miundombinu ambayo imejenga, imeimarishwa, ningetoa wito kwetu sisi kama wawakilishi wa wananchi tuendelee kuwahimiza wananchi wetu, tuendelee kulinda miundombinu ambayo imejengwa kwa faida yetu sisi tuliopo leo hata kwa kesho kwa vizazi vyetu viliopo. Miradi hii ni mikubwa ina gharama kubwa, tukishirikiana katika kuibomoa tutakuwa tunarudisha nyuma taifa letu katika hatua za kimaendeleo ambazo tunaendelea nazo katika kipindi cha miaka 52.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ningeomba sana, nimesikiliza kwa utulivu sana michango ambayo walikuwa wakichangia Waheshimiwa Wajumbe. Kwa bahati mbaya sana sikuweza kusikia michango mingi ya wajumbe ambayo ingeweza kuishauri serikali katika kuongeza vyanzo vya mapato, kwani sote tumeona serikali namna ya vyanzo ambavyo imepanga. Ni imani yangu kwamba katika wajumbe hawa ambao wamo wataalamu wa fani mbali mbali basi wangeshajihisha na kushirikiana na serikali katika kubuni vyanzo na kuendeleza vyanzo viliyopo katika kuongeza mapato kwa sababu serikali haikatai maelekezo ama vyanzo vyengine vya mapato katika kuongeza mapato ya serikali kwa kutambua sote tuna madhumuni mamoja ya kumsaidia mwananchi wetu katika huduma ambazo anapewa.

Mhe. Naibu Spika, kipekee naomba niendelee kuishukuru sana serikali kwa maamuzi yaliyofanywa ya kupandisha mshahara asilimia mia moja. Haya ni maamuzi makubwa sana na lazima tujisifu wala tusione aibu, kujisifu kwa kutambua kwamba kufanya mabadiliko ya mshahara kwa asilimia mia moja ni maamuzi makubwa na maamuzi yenye tija sana kwa maslahi ya wananchi wetu na kwa maslahi ya wafanyakazi wetu. Sasa inapofika pahali kwamba sisi wawakilishi kama jambo hili hatujalisema vizuri, maana yake tutakuwa tunaivunja moyo serikali lakini pia tutakuwa tunawavunja moyo wananchi wetu na wafanyakazi wa serikali, ambapo kwa kiasi kikubwa wafanyakazi hawa wa kada ya chini dio ambao serikali imewalenga katika kuwaongezea kipato chao ili maisha yao yawe bora zaidi.

Mhe. Naibu Spika, lakini kama hilo halitoshi kwa mara ya kwanza katika ukanda huu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya maamuzi mengine mazuri na yenye maslahi makubwa sana ambapo imeweza kwenda na *Universal pension*, jambo ambalo ni lenye faida kubwa sana kwa wananchi wetu, wazee wetu ambao wameweza kulitumikia taifa hili, wameweza kuitumikia nchi hii, ambapo wamefikisha umri wa kutokuwa na nguvu kile kile kidogo ambacho serikali inacho imeona ipo haja na ipo sababu ya msingi wa kuweza kugawana nao na kuonesha *incentive* zao kwamba hazikuwa bure wala hazikuwa zimepotea katika jasho lao walilolipoteza katika kujenga nchi yetu hii.

Mhe. Naibu Spika, jengine Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya maamuzi mengine ya busara makubwa sana ambayo ni kumpunguzia mzigo wa kodi mfanyakazi wetu. Tumepunguza kodi kutoka asilima 13 hadi asilimia 9 ni jambo kubwa sana la kupigiwa mfano. Ni imani yangu kwamba mambo haya ukiyatizama matatu kwa ujumla yangetosha kutupa sifa na faraja kubwa serikali kwa wananchi wetu na jamii tunayoiongoza. Niombe tu Waheshimiwa Wawakilishi tuendelee kuipa nguvu serikali, kuiunga mkono kuona haya ambayo yamedhamiriwa na yamefanyika yanaendelea kudumishwa kwa matendo ili wananchi wetu wazidi kunufaika kwa siku za mbele zinazokuja.

Mhe. Naibu Spika, jengine hapa limezungumzwa kwa kiasi suala la barabara ya Ole - Kengeja juu ya dhana na hofu, suala zima la kulipwa fidia na suala la kwamba barabara itajengwa katika uvungu. Jambo hili Mheshimiwa, halina msingi mkubwa wa kulaumu, ni kweli kwamba serikali imeamua kujenga barabara kwa kiwango cha lami barabara yenye urefu wa kilomita 35 ya kutoka Ole hadi Kengeja. Barabara maamuzi ya serikali kwamba itajengwa kwa hatua, itajengwa kwa mujibu wa maumbile ilivyo, barabara yenyewe tunajenga kipande baada ya kipande na baadae kuunganisha tukapata hesabu ya kilomita 35. Lakini hata utaratibu husika wa ulipaji wa fidia, fidia inalipwa kwa utaratibu huo huo, kipande ambacho kimekusudiwa kutumika ndicho ambacho kitalipwa fidia, lakini maelekezo ya serikali yako wazi kwamba kulikuwa kuna hofu na utaratibu wa tathmini haukuwa mzuri sana.

Kwa hiyo, serikali inaendelea kufanya utaratibu mzuri wa kupata tathmini kwa kuona kwanza mali inayochukuliwa na serikali kwa ajili ya kubomolewa kwa ajili ya kupitisha barabara inakuwa ni mali halisi inayotambulikana, imefanyiwa tathmini inayostahiki kwa mujibu wa bei na viwango vya serikali ndio hapo baadae serikali iweze kulipa fedha kwa wale ambao watapisha maeneo ya ujenzi wa barabara.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine lililozungumzwa ni suala la gati kwa upande wa Mkokotoni. Mhe. Naibu Spika, matarajio yangu kwamba Waheshimiwa Wawakilishi, wangeendelea kuisifu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada ambazo imezichukua katika kurahisisha huduma nzima za miundimbinu ya usafiri. Ni kweli ahadi ya Mhe. Rais ya kujenga gati kwa upande wa Mkokotoni na Tumbatu aliitoa katika kampeni mwaka 2010 na katika mwaka huu 2015 ahadi ile sehemu ya asilimia 50 imeshakamilika.

Kama utakwenda Tumbatu Gomani mkabala na Ofisi ya Wilaya Ndogo ya Tumbatu utaona tayari kwamba kipande cha gati chenye urefu karibu mita mia moja kimeshajengwa. Namshukuru sana Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Tumbatu yeye alikuwa ni shahidi mwaka huu Mwezi wa Pili tulipokwenda kutembelea gati ile na Mhe. Rais akawa ameridhika na jitihada. Mipango ya serikali kwa kupitia Shirika la Bandari ni kuona kujenga gati ya upande wa pili sasa ya Mkokotoni ili kukamilisha mradi huo kuupunguza usumbufu wanaoupata wananchi wetu wanaovuka kwa ajili ya kwenda kisiwani. *(Makofi)* Mhe. Naibu Spika, pongezi za pekee ningetarajia zingekwenda kwa wakandarasi wetu wa ndani wanaosimamiwa na Shirika la Bandari kwa kuona kazi hiyo wameifanya wao wenyewe kwa kuzingatia maumbile ya bahari, kina cha maji, maumbile ya udongo, lakini vifaa na rasilimali zilizotumika zote zimesimamiwa na wao kwa utaalamu wao wa ndani.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine la mwisho ambalo ningependa kulichangia nimesikiliza hapa kwa makini suala la *DIASPORA*. Nilihakikishie tu Baraza lako tukufu kwamba serikali imefanya maamuzi ya makusudi kuona kwamba eneo hili la *DIASPORA* tuweze kuwahusisha wenzetu Watanzania na Wazanzibari walioko nje ya nchi ili na wao waweze kutoa nguvu zao au mchango wao katika harakati za maendeleo nchini kwetu. Ni kweli kwamba mwaka jana 2015 Mhe. Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya kongamano kubwa Dar-es-Salaam kwa madhumuni ya kuwashajihisha na kuwahamasisha Watanzania ili nao Watanzania wanaoishi Ughaibuni nao waone umuhimu wa kuja kwao kuja kuwekeza. Nimhakikishie Mhe. Mwakilishi na Baraza lako tukufu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imekamilisha Sera ya *DIASPORA*, hatua iliyofikiwa ni kwamba tayari Kamati ya Makatibu Wakuu wameshaipitia, tunajiandaa kwa ajili ya kufikisha serikalini kwa kukamilisha maamuzi ya serikali ili baadae tukamilishe utaratibu mzima husika ili sasa tuwape nafasi na fursa kubwa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi na wao waweze kutoa mchango wao katika maendeleo ya taifa lao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naomba nirejee tena kauli yangu ya kwanza kwa kusema kwamba naunga mkono bajeti hii kwa asilimia

mia moja, mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wenzangu wa Jimbo la Chwaka.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nikushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia Hotuba hii ya Serikali ambayo imewasilishwa na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Khalid Salum Mohamed.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa ushindi mkubwa sana aliyoupata kwenye uchaguzi mkuu uliopita na kuendelea kuiongoza nchi yetu.

Pili, nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Khamis Mussa Omar kwa maandalizi mazuri ya Hotuba hii ya Bajeti ya Serikali kuhusu Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, tatu, nataka vile vile niwashukuru kwa mara nyengine tena wananchi wa Jimbo langu la Tumbatu kwa mara nyengine tena ya tano kunipa ridhaa yao ya kuwaongoza kuwa mwakilishi wao, nawashukuru sana. *(Makofi)* Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo pia nataka niwapongeze wawakilishi wenzangu wote ndani ya Baraza hili tukufu ambao wamepata ridhaa ya wananchi katika kuwatumikia katika kipindi cha miaka mitano hii. Ni imani yangu kwamba wananchi wamewaamini ndio maana wamewachagua, lakini pia wale waliopata bahati ya kupitia Jimbo la Ikulu nao wamechaguliwa kwa sababu aliyewateuwa amechaguliwa na wananchi wote wa visiwa hivi vya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, moja kwa moja niende kwenye mchango wangu nilioukusudia, nataka nimpongeze Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uamuzi wake wa kuitekeleza kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 hadi 2020. Katika kitabu hiki au katika hotuba hii kwenye ukurasa wa 18 Waziri wa Fedha na Mipango ametueleza jinsi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Saba inavyokusudia kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili tuweze kujitegemea na kupunguza utegemezi kwa baadhi ya washirika wetu wa maendeleo na wahisani wetu.

Nadhani eneo hili ni eneo muhimu sana kwetu sisi kulisimamia na kuhakikisha kwamba dhamira ya Rais wetu na dhamira ya wenzetu wanaosimamia eneo hili

sote kwa pamoja Waheshimiwa Wawakilishi tulisimamie na tushirikiane nao ili liweze kutekelezeka kwa asilimia mia moja. Kwani tutakapofanya hivyo ndipo sote tutakaporudi kifua mbele mwaka 2020 baada ya ukusanyaji mzuri wa mapato, maana yake na utekelezaji wa Ilani ya CCM tutautekeleza kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Spika, nataka niungane na wenzangu wote walioliunga mkono eneo hili na kwa sababu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ndio ambao tutapita kukagua utekelezaji wa serikali bila shaka tutachukua nafasi hii kuwahimiza wananchi wetu ili kujenga utamaduni wa kununua na kudai risiti. Vile vile, sisi ambao tuko katika sekta mbali mbali tuliopewa majukumu ya kusimamia ofisi za serikali nasi tutazidisha kasi ili kuhakikisha kwamba serikali inaongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ili tuondokane au tupunguze utegemezi katika matumizi yetu ya serikali. Hilo limeelezwa kwa upana zaidi katika ukurasa wa 18 katika hotuba hii.

Jengine ambalo nilitaka nilisema ni suala zima la serikali kuweka mkakati katika ukurasa wa 24 wa kuhakikisha kwamba kila kwenye shilingi moja serikali inatumia senti 58.7 kwenda katika sekta tano muhimu ambazo zimebeba malengo makuu ya serikali ambazo ni ujenzi, mawasiliano na usafirishaji, elimu, mafunzo ya amali, afya, ardhi, maji, nishati na mazingira na kilimo mali ya asili, mifugo na uvuvi kwa ujumla.

Sekta hizi tano zinatarajiwa kutumia jumla ya Shilingi 494.2 bilioni, katika kipindi cha mwaka huu wa bajeti sekta hizi zinatarajiwa zitumie pesa hizi. Kwa hiyo, naipongeza sana serikali kwa maamuzi ya kuweka kiwango hichi cha fedha ambapo ukifanya hesabu kwa wale wachapa hesabu utakutia kiasi ya senti 41.3 tu ndio ambayo imeelekezwa katika sekta nyengine muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Kwa hiyo, nataka nichukuwe fursa hii kuwapongeza wachumi wetu pamoja na uongozi wa Wizara ya Fedha kutushauri serikali na serikali tukakubali na hii leo nina imani kwamba hotuba hii iko mbele yetu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tutakubaliana nayo ili serikali iweze kufanya tuliyoyakusudia.

Pengine kile kilio cha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao toka wameanza kuchangia hasa pale walipokwenda katika ukurasa wa 29 kifungu cha 68 kwenye suala zima la uwekaji wa kamera za vifaa na vifaa vya ulinzi vya Tanzania shilingi bilioni kumi na nane. Sasa mimi nadhani Waheshimiwa Wajumbe walikuwa hawakwenda zaidi wakaangalia hizi sekta muhimu hasa zile walizozipigia kelele miundombinu ya barabara, afya, elimu.

Hawakwenda kwenye ukurasa huu ambao umeeleza kinaga ubaga kwamba bajeti yetu ya mwaka huu imezingatia suala la kutumia senti hamsini na nane nukta saba kuelekea katika sekta zile nyengine ambazo wamezizungumza.

Mhe. Naibu Spika, imani yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe watapitisha mafungu yote haya wakati tutakapokwenda kwenye kamati ya matumizi. Kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Suala la uwekaji wa *CCTV* limetokana na nini. Limetokana na ushauri uliofanyika kwenye Baraza la Biashara la Taifa miaka mitatu iliyopita kwenye maabara ya utalii kutokana na matukio mbali mbali ambayo yalitokea ya kuhujumiwa wageni kutoka nje na namna Zanzibar ilivyokuwa imesakamwa na kutishiwa kwa kushawishiwa kwa nchi zinazoleta watalii ziache kuleta kutokana na kutokuwa na usalama wa kutosha.

Kwa hiyo, serikali haikukurupuka katika kulileta suala hili iliona upo umuhimu wa kuweza kujiandaa na kuweka vifaa vya ulinzi hasa *CCTV*. Sote tumeshuhudia matukio mbali mbali ya utiaji wa tindi kali kwa wageni na raia umefanyika katika nchi hii na katika dunia ya leo huwezi kubaki hivi tulivyo. Kwa hivyo, bilioni kumi na nane hizi sio zote zinakwenda kwenye *CCTV* nimesema ni *CCTV* pamoja na vifaa vyengine vya ulinzi.

Mhe. Naibu Spika, *CCTV* ni *component* moja tu katika fungu hili la bilioni kumi na nane, hakuna kitu muhimu katika dunia hii ya leo kama kujihakikishia usalama wa nchi. Kwa hivyo, hatuwezi tukasema tuna-*save* bilioni kumi na nane lakini usalama wa nchi yetu na usalama wa wananchi wetu na usalama wa wageni wanaotutembelea tukasema hakuna umuhimu wa kuweka vifaa vya ulinzi na kuweka *CCTV* kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa kutosha katika nchi yetu unapatikana.

Kwa hiyo, mimi niwaombe Waheshimiwa Wajumbe, inawezekana pengine waliangalia kwa haraka haraka, kweli ukichukuwa suala la *CCTV* kwa mfano zile ninazoweza kuweka nyumbani kwangu ni tafauti na *CCTV* hizi kabisa. Lakini hii ni sehemu tu ya *component* ya vifaa vya ulinzi ambavyo vitatumia hizi bilioni kumi na nane ndani yake kuna vifaa vingi. Sote tumekuwa tukishuhudia matukio ya kuingizwa silaha kwenye Bandari bubu, sasa hatuwezi kuelekea katika udhibiti kama hatukujihakikishia kuwa na vifaa muhimu vya ulinzi.

Lakini hata sekta yetu ya utalii ambayo inaingizia nchi mapato ziadi ya asilimia 80 za fedha za kigeni kama hatutakuwa na usalama wa kuhakikishia wageni wetu wanaotutembelea kwamba tunao usalama wa kutosha.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo naomba niende moja kwa moja kwenye suala zima la kuishukuru Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mambo mengi ambayo ndani ya jimbo langu katika kipindi kilichopita yaweza kupatikana chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Ali Mohd Shein, mambo mengi yameweza kufanyika ya maendeleo kwa wananchi wa Jimbo la Tumbatu. (*Makofi*)

Kama alivyokwisha kusema Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ahadi ya ujenzi wa gati katika maeneo ya Mkokotoni na Tumbatu zilitolewa toka wakati wa Awamu ya Tano ya Dkt. Salim Amour Juma. Lakini faraja iliyoje baada ya kuingia Awamu wa Saba ya Dkt. Ali Mohd Shein utekelezaji wa gati ndogo katika kisiwa cha Tumbatu sasa umekamilika na imani yangu kwamba Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji itakapokuja na bajeti yake kupitia Shirika la Mabandari kama alivyosema Waziri wa Nchi Afisi ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na upande wa pili wa ujenzi wa gati katika eneo la Mkokotoni nao utaelezwa na bila shaka utakamilika katika kipindi hiki cha awamu ya saba 2015/2020. *(Makofi)*

Kwa sababu ahadi zilizomo katika Ilani ya Uchaguzi hatukuahidi, yaani CCM hatuweki ahadi ya siku mbili. Ahadi zetu zote ni kwa kipindi cha miaka mitano na lazima wakati wa kuendesha serikali Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza tukufu uchague vipaumbele vya kuvifanyia kazi, huwezi katika kipindi cha mwaka mmoja ukafanya yote. Lakini ndani ya kipindi cha miaka mitano ni imani yangu kwamba na ujenzi wa gati hii ya Mkokotoni nayo itakamilika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, zimetajwa barabara kadhaa, nataka pia nichukuwen nafasi hii kuipongeza serikali kwa ujenzi wa barabara itakayoanzia Chuini kwa Nyanya hadi Mkokotoni. Ni imani yangu kwa sababu kwenye bajeti hii imo na pia kwenye mipango ya serikali imo. Vile vile, nina imani kwamba atakapokuja Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji atakuja kuieleza kwa kina zaidi. Kwa hiyo, mimi naipongeza serikali ya Dkt Ali Mohd Shein ya Awamu ya Saba kwa kuweka mipango madhubuti katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika kipindi cha miaka mitano hii. Kwa mafano barabara imetajwa itajengwa katika kipindi cha mwaka huu barabara ya Mtambile - Muwanda nayo ni imani yangu ndani ya kipindi cha miaka mitano hii nayo itapata nafasi ya kujengwa kupitia fedha za mfuko wa barabara. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya kwisha kusema hayo. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tumbatu naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii maalum ili kutoa mchango wangu juu ya bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, na mimi kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa katika hali ya uzima katika wakati huu na wasaa huu. Na mimi pia nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Rais wa Zanzibar Dkt Ali Moh'd Shein kwa ushindi wa kishindo alioupata. (*Makofi*)

Aidha, nampongeza Makamu wa Pili wa Rais Balizo Seif Ali Idd kwa ushindi wa kishindo alioupata katika jimbo lake lakini pia na kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais.

Aidha, nampongeza sana Spika wa Baraza la Wawakilishi, Naibu Spika na viongozi wengie wote.

Baada ya kusema hayo niende moja kwa moja katika kutoa maoni yangu halafu mwisho nitawashukuru wapiga kura wangu baadae na familia yangu.

Mhe. Naibu Spika, niemona nichukuwe fursa hii ili kutoa tafsiri yangu niliyoipata kwa mujibu na muelekeo wa maoni ambayo tulikuwa tunatoa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa maoni yangu baada ya kutafakari kwa kina bajeti na mpango wa maendeleo nimeona kwamba kwa mpango huu na bajeti hii imeelekezwa katika kuwakomboa masikini kwa lugha nyengine tunasema *pro-poor* budget *and pro-poor planning* na hii imefanywa kwa makusudi ikiwa ni hatua za awali za kuwaondoa wananchi wetu katika hali ya kipato cha sasa ili kwenda katika kipato cha uchumi wa kati. Kwa hivyo, suala hili limeandaliwa kwa makusudi.

Mhe. Naibu Spika, ni muhimu kuelewa kwamba ili kuwafikishia na kuwatimizia wananchi wetu malengo tuliyokusudia ni lazima mpango huu na bajeti hii tuielewe sote serikali na Wawakilishi na kwa maneno mengine mpango huu lazima tu-*own ownerships of the planning and budget.* Kwa tafsiri yangu vile vile wakati wa michango ya Waheshimiwa Wawakilishi ilionekana kama kwamba kuna kuonesheana kidole serikali, serikali, serikali. Ni kweli serikali lakini tuelewe kwamba mpango huu ni wetu sote. Kwa hivyo, sote tuhakikishe kwamba kila senti itakayotumika kwa mpango huu baada ya kupitishwa basi inalenga katika kufanisha malengo ya uchumi yaliyopangwa katika mwaka huu wa fedha na kila senti iwe na *impact* kwa ajili ya kuongeza uchumi wetu. Haitowezekana hata kidogo sote serikali pamoja na Wawakilishi kutumia fedha kinyume na mipango tuliyojiwekea.

Kwa hivyo, sisi viongozi na ninaposema viongozi na Wawakilishi wamo na watendaji wetu wamo, lakini pia na wananchi lazima mpango huu tuuelewe baada ya kuuelewa tuumiliki, tukisha umiliki tuutekeleze kwa pamoja na kwa hivyo, lengo letu litafanikiwa. (*Makofi*)

Kwa maana hiyo Mhe. Naibu Spika, fikra hii au dhana hii ndio itakayotusaidia kuifanya bajeti yetu iwe na *value for money* haitakuwa busara kutumia mabilioni ya pesa halafu athari yake ikawa ndogo busara zaidi na hekima zaidi ni kuona kwamba tunatumia fedha katika bajeti hii na matokeo yake yalingane na tukifanya hivi kwa kweli tutasonga mbele hatua kwa hatua. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, jamho jengine la jumla ambalo nataka niliseme ni suala la tabianchi.Hili hatujalisema vizuri sana, kwa kweli suala hili tunalihitaji sote serikali na Wawakilishi kulitizama katika jicho kubwa zaidi kwa sababu athari nyingi zimeshaanza kujitokeza katka jamii zetu na sote ni mashuhuda wa suala hili. Kuongezeka kwa maji ya chumvi na kuingia katika mashamba ya mipunga, hili limekuwa na athari kubwa. Hata juzi tu nilipokuwa katika ziara ya jimbo langu wananchi wamenionesha athari kubwa iliyoletwa na bahari kuingia katika mashamba ambayo watu wanalima mpunga katika kisiwa cha Makoongwe, Kisiwa panza na Mabonde mengine kama Jalani, Tondooni, Kikoma na maeneo mengine yote haya yameathirika.

Kwa hivyo, nataka suala hili sisi serikali na sisi Wawakilishi tulichukuwe kwa uzito wake na tulitafsiri kwa uzito wake kwani lina athari kwa wananchi wetu ambao ndio masikini. Kwa hivyo, jambo hili la athari za tabianchi limeshaanza kuleta athari kwa wakulima wetu na kwa maana hiyo hapa nadhdani sisi serikali itabidi tuchukuwe hatua maalum lakini pia na Wawakilishi tuchukuwe hatua maalum za kuona kwamba athari hizi tunazipunguza kadri inavyowezekana.

Mhe. Naibu Spika, ni muhimu pia kuelekwa kwamba sisi viongozi wa kisiasa tukiwemo wa serikali na Wawakilishi kwamba lazima tuwe wakweli na waadilifu katika kutimiza majuku yetu. Tusipofanya hivyo kwa kweli tutakuwa hatuwatendei haki wananchi wetu ambao wametuchagua. Kwa hivyo, lazima tuwaoneshe imani kama kweli tuko pamoja na wao.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine la mwisho ambalo nataka kulisema pengine watu walidhani labda nitazungumzia masuala ya elimu ata leo si siku yake. Wananchi wa Jimbo la Mkaoni wanatoa shukurani za dhati kabisa kwa serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa juhudi zake iliyochukuwa katika suala zima la kulifanyia ukarabati mkubwa Hospitali ya Abdalla Mzee ambayo sasa hivi

imefikia hatua za mwisho kukamilika. Kwa hivyo, wanaishukuru kwa moyo safi kabisa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupita Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo, sisi viongozi tuone fahari kueleza matunda yanayoletwa na Serikali ya Mapinduzi katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tusione haya kueleza mafanikio yaliyopatikana. (*Makofi*)

Aidha, pia wananchi wa Jimbo la Mkoani wanaishukuru tena serikali kwa kuweza kujenga skuli kubwa ya Sekondari ya Mkanyageni ambayo pia imefikia karibu asilimia 95 ya kuweza kukamilika.

Baada ya kusema hayo sasa nitoe shukurani zangu za dhati kwa wapiga kura wote wa Jimbo la Mkoani, Shehia ya Chokocho, Mkanyageni, Makombeni, Kisiwa Panza na nyenginezo. Lakini pia nitoe shukurani maalum kwa viongozi wa Chama cha Mapinduzi katika Jimbo la Mkoani kwa kusimamia vyema Ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Halkadhalika natoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa familia yangu hasa mama yangu Mwakombo Mmanga, wake zangu wote, watoto wangu wote. (*Makofi*)

Mwisho, kabisa nashukuru wananchi wote. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Sasa hivi ni zamu ya Mhe. Rashid Ali Juma na Naibu Waziri wa Afya. Kwa kuwa muda tunao ninatarajia Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo hatochukua muda wote huo, kwa kuwa wakati tunao tutampa nafasi Mhe. Harusi Said Suleiman, kuchangia kidogo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. Mimi awali ya yote nimshukuru nimshukuru *Allah Subuhana Wataalla* Muumba Mbingu na Ardhi kwa kutuwezesha hadi siku ya leo kuwa na afya bora na kukaa hapa kuweza kuchangia na kujadili mambo muhimu ambayo yanaweza kuipelekea nchi hii katika maendeleo kabisa na kuweza kutufikisha tutakaporejea kwake, tukawa watu wenye kuridhiwa. Ninamshukuru *Allah* kwa hatua aliyotupa.

Pili, nichukue fursa kuishukuru sana familia yangu. Familia ya Mzee Gudi, hususan na nitaanzia na mke wangu mpenzi aliyemmoja, wapekee, asiyetarajia mwengine pamoja na watoto wake ambao kwa muda mrefu wameweza

kuungana na mimi baada ya kipindi kizito sana cha mambo mengi yaliyopita na kuweza kunivumilia kwa yote hadi kufikia leo hii, na mimi kuwa ni mmoka katika Wawakilishi wanaoweza kuwatetea wananchi kupitia jimbo lao. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii ya pekee kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuweza kushinda kwa kishindo kikubwa kabisa ambacho hakijatokea tangu tuanzia vyama vingi kwenye uchaguzi. Na hakitarajiwi kupitwa kiwango cha asilimia 91.4. Ninamshukuru sana kwa ushindi alioupata, lakini vile vile ninamshukuru kwa imani kubwa aliyotupa kuweza kutuchagua kuwa miongoni mwa viongozi ambao tutaisimamia nchi hii na kuweza kuitetea hadi kuifikisha katika uchaguzi ujao wa 2020 bila ya kupata Wapinzani kama walivyokataa hawa waliopita. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, itakuwa ni vyema zaidi nikaendelea kuwapongeza na kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Amani kwa kuweza kuamua kwa makusudi na kwa dhati kabisa, kuweza kunipitisha mimi kama mgombea wao na hatimae kushinda kwa kishindo kikubwa katika chaguzi zote mbili; ulioharibika na wa marejeo. Lakini imani yao ilibakia pale pale kunipatia ushindi. Ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Amani na wote ambao walishiriki katika kutusaidia kwenye uchaguzi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila ikiwa sitowashukuru wafanyakazi wa vyombo vya habari ambao hii leo wapo hapa na wapo tangu tulipoanza kula kiapo kwenye Baraza hili. Na wataendeleza kulionesha Baraza hili na wananchi waweze kuelewa ukweli. Ninawashukuru sana kwa kazi zao kubwa na ninatumaini nitakuwa msimamizi wa kwanza kuhakikisha yale masuala yanayoulizwa, kupata haki zao kupitia bajeti. Basi tutawasimamia wazi tuhakikishe wanafanya kazi hii kwa ari zaidi na moyo wa ukunjufu na upendo wa kazi yao. (*Makofi*)

Mwisho kabisa nichukue fursa kuwashukuru wafanyakazi wa Wizara ya Habari, Utalii na Michezo kwa kuweza kunipokea mara tu baada ya kuchaguliwa kuwa kiongozi wao wa wizara. Na kunipa ushirikiano mkubwa ambao hadi hivi sasa unaleta mwelekeo mpya wa kuona kwamba kweli CCM imeshika madaraka. Kuwepo kwetu basi Wapinzani hawakuwa wakileta maendeleo. Maendeleo tunayo sisi.(*Makofi*)

Baada ya hayo sasa Mhe. Naibu Spika, naomba nichangie mambo machache kabisa. Kwanza nichangie suala zima la bajeti hii kwa kujali usalama.

Ninapenda nijuulishe Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wawakilishi wote pamoja na shukurani mulizozipata, tuelewe wazi kwamba bila ya usalama hakuna bajeti. Bajeti inajali sana usalama wa nchi. Usalama wa nchi yetu ni muhimu sana katika kuhakikisha kwamba yote tunayoyachangia hapa basi yatafikiwa ikiwa tumejali sana na tumetuliza sana na kusimamia usalama wa nchi hii. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ni wazi kwamba hapa tunajadili mapato na matumizi ambayo yamewasilishwa.Lakini matumizi haya yataweza kufikiwa endapo mapato yatapatikana. Mapato yatapatikana endapo usalama utakuwa wa hali ya juu. Basi nichukue fursa hii katika kuisimamia bajeti hii na kuiunga mkono bajeti hii, tumpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa muda wote huo tuliokuwa nao kuweza kuutuliza usalama, utulivu na amani ndani ya nchi hii. Hadi sasa tunaweza kujadili bajeti hii. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ni wazi kwamba tumepita katika kipindi kigumu. Kipindi hicho kilikuwa kinatarajiwa kuwa na misukosuko mengi, lakini ni wazi kwamba kama misukosuko hiyo, utulivu umepatikana, amani imepatikana basi na bajeti hii tuliyoitunga hapa na tukaiwasilisha, ikapita kwa Makatibu Wakuu, ikapita Baraza la Mapinduzi na hatimaye kuwasilishwa hapa kwenye mjadala wa Baraza la Wawakilishi. Ni wazi kwamba bajeti hii itapita na tutaisimamia vizuri na mapato yatapatikana na *inshaallah* matumizi yatakwenda kama yalivyopangwa kwenye mapato ambayo yatapatikana. (*Makofi*)

Sasa ninataka nichangie kidogo kuhusu suala la maji. Suala zima la maji Mhe. Naibu Spika, linaonekana ni kero kubwa sana. Bajeti hii nayo imeletwa kwa jumla wake. Katika suala zima la kupata bajeti hii, mapato ambayo yamepangwa, basi naomba sana tuweke kipaumbele suala zima la maji. Kwa sababu la maji ndiyo ndiyo suala la mwanzo la uhai wa binadamu. Bila ya maji, binadamu hatoweza kufanya chengine chochote. (*Makofi*)

Naomba sana bajeti hii ilitilie mkazo suala zima la maji. Tukikumbuka historia ndogo tu. Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kipindi chake chote cha miaka mitano ya Awamu hii ya Saba aliyoanza kuongoza, alitia mkazo mkubwa sana katika kuyasimamia upatikanaji wa maji. Ni vyema wananchi wakaelewa na Waheshimiwa Wawakilishi wakachukua fursa hii kuweza kuwafahamisha wananchi kwa kila jimbo lao na kwa kila eneo lao wanaloishi.

Mhe. Naibu Spika, uhaba wa maji ndani ya kisiwa chetu umeanza kutawala. Kisiwa chetu miaka ya nyuma hakikikuwa na tatizo la maji. Tulikuwa tunauza

maji kupitia kwa mameli nje ya nchi na kupitia kwa watu mbali mbali ambao wanaokuja wakaona ubora wa maji yetu. Lakini hivi sasa inaonekana wazi kwamba maji katika visiwa vyetu yamepata msukosuko wa upungufu. Kwa hivyo, ni vyema kwamba tukawafahamisha wananchi kwamba kina cha maji ambacho tulikipata wakati wa nyuma na ambacho kilikuwa kinatokana na chemuchemu mbali mbali hivi sasa kimepungua.

Lakini kwa jitihada za serikali hii, bado tumeweza kupunguza tatizo la maji kwa zaidi ya asilimia 83 kwa upande wa Unguja na asilimia 87 kwa upande wa Pemba. Ni kiasi kidogo sana ambacho hivi sasa kikafikiwa tatizo la maji linaweza likaondoka. Likiondoka tatizo la maji kupitia bajeti hii, basi matatizo mengine yatakuwa ni rahisi kuyatatua. Wapo wanaotaka kuleta viwanda, wapo wanaotaka kuleta uwekezaji, lakini hao wote tegemeo lao kubwa ni suala zima la maji. Hivyo, naomba sana katika bajeti hii ambayo tunaijadili fungu ambalo litapangiwa kwenda suala zima la maji lipelekwe kwa asilimia mia bila ya kuchelewa, ili wananchi waweze kupata suala zima la maji. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nizungumzie kidogo suala la mapato. Bajeti hii tunayoizungumza itakuwa na thamani fupi endapo mapato tunayotarajia kuyakusanya yasifikiwe. Basi ni vyema sasa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango akajipanga vizuri yeye na timu yake, kuhakikisha kwamba mapato ya ndani tuliyopanga kuyakusanya yanakusanywa kwa ukamilifu bila ya kupungua. Ikiwezekana mapato haya yakusanywe kabla ya kufikia mwisho wa mwezi wa Juni. Jambo hilo linawezekana kutokana na vianzio tulivyonavyo.

Mhe. Naibu Spika, mapato ya ndani kuna sehemu nyingi hivi sasa yanaonekana bado hayajakusanywa vizuri. Mimi labda nitoe mfano mmoja tu mdogo. Tutagundua kwamba muda mrefu tumeanza suala la uwekezaji na tumeanza kutegemea suala la utalii. Utalii hapa petu umeanza mwaka 1992 na ulianza na hoteli chache tu.

Hoteli zilizoanza hapa ilikuwa labda ni Mawimbini, Uroa *Bay*, *Bravo Club* na nyengine kama *Franco Rosso*. Lakini hoteli hizo zimekuwa zinauzwa muda kwa muda kwa thamani kubwa sana. Na pato linalouziwa hoteli hizo huwa halikusanywi kodi. Hoteli inauzwa kutoka mmiliki mmoja kwenda mmiliki mwengine. Nchi yetu hatutambui wakati gani imeuzwa, wakati gani imehaulishwa. Lakini wakati wa kuhaulishwa, kuna *management fees* ambazo zinafanyikana, kuna mapato yanayotokana na mauzaji ya hoteli zile lakini watu weu bado hawaja mahiri katika kukusanya mapato haya.

Mapato haya ni lazima yakusanywe kwa nguvu zote kupitia vyombo vyetu vyote viwili. Iwe chombo cha *TRA* kwa ile kodi ya *ten percent*, yaani kodi moja ambayo inakuwa ni ya *VAT* kwa upande wa *ZRB* na kodi ya *ten percent* ambayo inakusanywa *TRA*. Nimesahau kidogo jina lake.

Lakini vile vile ninataka kusema kwamba tatizo zima la watu ambao wanakuja kupata huduma hapa petu kupitia utalii. Utalii wetu una mfumo *package*. Mfuno wa *package* umefanyiwa *research* mara nyingi sana. Ni ule mfumo ambao mtu analipa huko aliko, mtu analipa kila kitu, hapa anakuja kwa matumizi tu. Kwa hivyo, si rahisi sana kujua kiasi ambacho anatumia na pato gani ambalo nchi imepata na kiasi gani kingeweza kukusanywa kama kodi. Ni vyema sasa tukawa wafuatiliaji wazuri tukajua matumizi halisi ambayo yalipaswa kukusanywa hapa Zanzibar na matumizi ambayo yalipaswa kukusanywa upande wa pili ambapo wageni wanatokea. Mapato haya yanaweza kuisaidia sana nchi yetu katika kukuza mapato na tunaweza tukaendeleza mapato ambayo tunayatarajia katika kuendeleza bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, nije suala zima la utamaduni na uasilia wetu. Ni wazi kwamba tuna wajasiria mali wengi sana, tuna sekta isiyo rasmi. Sekta isiyo rasmi haikusanyi kodi vizuri. Kwa vile wao tayari wamejiweka kwenye utayari wa kujiona kwamba sisi ni wakusanyaji mapato na wafanyabiashara wadogo wadogo. Hivyo, ulipaji wao unakuwa ni wa makisio. Mara nyingi hawa wanashindwa kutunza hesabu na hawawezi kabisa kukusanya ipasanyo. Ningeomba sana taasisi zetu zote mbili zikashirikiana kwa njia moja au nyengine kuhakikisha kwamba mapato katika sekta isiyo rasmi inawezwa kuwekwa katika *net* na inakusanywa vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, niende kwenye hali nzima inayotokana na masuala ya mapato kwenye asilia yetu. Tumekuwa wabunifu wa kuweza kufanya biashara mbali mbali lakini wananchi wetu hawana ubuni na utamaduni wa kulipa kodi katika hizo bidhaa tunazozilisha. Mhe. Naibu Spika, biashara za mifukoni Zanzibar ni nyingi sana. Na biashara za mifukoni huwa hazina takwimu wala rekodi na Warabu wamesema, "mali bila ya daftari inaghibu bila ya habari". Kwa hivyo, mali ikighibu bila ya habari, maana yake kodi haitoweza kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, nichangie kidogo kuhusu maendeleo ya yaliopo. Mhe. Naibu Spika, kwenye kipindi hichi tangu tuanze vyama vingi nchi yetu imeonekana imepiga hatua nyingi sana za maendeleo. Sasa ni vyema katika kupitia bajeti hii tuliyokuwa nayo ni wazi kwamba tunataka kuleta maendeleo ya ziada zaidi ya tulipofikia. Katika kufikia hilo basi ningeomba sana

Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi wetu kwa jumla na mimi nitakuwa mfano kwa Jimbo langu la Amani ambao wamenichagua kwa nguvu zote, kuhakikisha kwamba tunachokifanya na tunachokianzisha kinatunzwa ipasavyo. (*Makofi*)

Tumekuwa wengi wa kuanzisha lakini si wazuri wa kutunza. Tumekuwa wazuri wa kupewa misaada na kupewa na mambo mengi lakini si wengi wa kutunza. Hivyo basi tunaweza tukarejea kuzijenga barabara ambazo zimeshajengwa, tunaweza kuendeleza kujenga miundombinu ambayo imeshafanyika kwa kipindi kirefu. Yote yanatupasa kuyarejea kwa muda mfupi kutokana na kushindwa kutunza na kuendeleza miundombinu ambayo tunayo. Kupitia bajeti hii basi ningeomba sana wasimamizi wa bajeti zote ambazo zimejumlishwa ndani ya bajeti iliyowasilishwa, tuwe mahodari wa kutunza vitu vyetu.

Mfano mzuri ni taa za barabarani za Michenzani ambazo zimejengwa kwa *solar,* zimejengwa muda mchache lakini sasa hivi haziwaki hata kwa asilimia tatu. Ni kushindwa kutunza. Kwa hivyo, ningependa sana katika bajeti hii, mengi tunataka tufanye mazuri, maendeleo yaliopo tuyatunze na tuyakuze. Barabara ziliopo tuziendeleze na tuzikuze, ili tuhakikisha kwamba usimamizi wetu utaendeleza vizuri bajeti hii tuliyokuwa nayo.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache, sasa na mimi nitoe hoja kwamba kwa bajeti hii iliyowasilishwa, mimi sina wasi wasi nayo. Bajeti hii ni toshelezi kama ilivyoambiwa. Ni *Based Budget Programme* ambayo tunaipanga hapa. Kwa hivyo, ninataka kuiunga mkono kwa asilimia zote zinazopaswa kuungwa mkono bajeti hii. Na *inshaallah* ninawaomba wenzetu tuipitishe bila ya matatizo ili tuoneshe umadhubuti wa Chama cha Mapinduzi. Chama cha Mapinduzi kimo humu ndani. Chama cha Mapinduzi ndiyo kimeweka bajeti hii na ndiyo sasa kitaweza kuisimamia na kuipitisha bajeti hii. Kwa hivyo, sisi kwa pamoja, mimi nikiwa wa mwanzo ninasema ninaunga mkono kwa asilimia mia na zaidi kidogo ili kuipitisha bajeti hii. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Rashid Ali Juma. Anayefuata ambaye atakuwa ni mchangiaji wetu wa mwisho, atakuwa ni Mhe. Naibu Waziri wa Afya Mhe. Harusi. Karibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika. Mimi kwanza naomba nitoe shukurani za dhati kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia kidogo pamoja na kufafanua kidogo baadhi ya changamoto ziliopo katika Wizara ya Afya.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kupata ridhaa ya Wazanzibari kwa asilimia 91.4. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ninapenda pia niendelee kutoa shukurani zangu za dhati kwa kumshukuru na kumtakia dua kwa Mwenyezi Mungu jembe letu la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi. Lakini pia naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kwa kukuchagua wewe pamoja na Spika kwa kura nyingi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ninapenda pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi, waliopata uteuzi wa Mhe. Rais pamoja na Manaibu Mawaziri pamoja na Mawaziri wasiokuwa na Wizara Maalum, Wakurugenzi, pamoja na Makatibu Wakuu. Na ninawaomba watumie vizuri nafasi waliyopewa na Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, katika kuendeleza kutoa shukurani zangu za dhati naomba pia niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Wete kwa kunichagua kwa kura nyingi na kuniwezesha leo kuingia na kusimama katika Baraza hili. (*Makofi*)

Ninawashukuru wote walionichagua na hata wale ambao walionuna hawakunichagua pia ninawashukuru. Mhe. Naibu Spika, naomba pia niishukuru familia yangu. Na nikianza na mama yangu mzazi pamoja na mume wangu na ndugu zangu na wanangu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ninapenda niendelee kutoa shukurani zangu kwa kumshukuru Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja watendaji wake wote kwa kutuandalia hotuba hii ya bajeti ambayo imeletwa kwetu kwa maslahi ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, nikianza kuchangia naomba nianze kuchangia kidogo kwa kupitia yale ambayo yaliainishwa katika hotuba yetu hii. Hotuba iliyokuwa nzuri, ilijitosheleza na ina vigezo vyote vya kuletwa katika Baraza hili. Ninaamini kwamba kutokana na jinsi na ubora wa hotuba ile, basi changamoto nyingi ambazo zinaikabili serikali yetu na zinawasumbua wananchi wetu basi

zitatuka na kupatiwa *solution*. Hasa changamoto ya barabara ambayo imo kidogo katika Jimbo langu la Wete. Ninaamini itapata ufumbuzi. Hasa kwa kuanzia barabara ya Wete mpaka barabara kongwa inayoishia Meli Tano.

Mhe. Naibu Spika, pia, ninaamini kwamba kwa hotuba ile na bajeti yetu ile iliyosomwa na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, tatizo la maji pia litapata ufumbuzi, tatizo ambalo linawasumbua kidogo kwa kiasi fulani wananchi hasusan kwenye kipindi hichi kinachoelekea cha mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Mhe. Naibu Spika, ubovu na uchakavu wa nyumba za maghorofa za maendeleo, hususan katika Jimbo langu la Wete Mtemani. Ninaamini kwa mwelekeo ulivyotueleza katika hotuba ile basi zitapata ufumbuzi.

Mhe. Naibu Spika, sasa kidogo naomba niingie katika kufafanua kidogo changamoto ambazo zinaikabili Wizara yangu na zilizotajwa katika michangio mbali mbali. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya inakiri kwamba wizara hii ni wizara ambayo ina changamoto nyingi. Na changamoto ni sehemu ya maisha. Ninawaahidi Waheshimiwa wa Baraza hili pamoja na wananchi kwamba awamu hii tuliyonayo ya saba na jinsi wizara ilivyojipanga kwa maelekezo ya Serikali Kuu, basi changamoto nyingi zitatuliwa. (*Makofi*)

Naomba nigusie kidogo katika kipengele kilichotajwa na Mheshimiwa, ninakumbuka kama ni Mhe. Machano Othman Said, cha uwepo wa kambi ya kipindupindu na wasi wasi wake kwamba kitaathiri nyumba jirani ambazo zipo na kambi hiyo au vijiji ambavyo vipo jirani na kambi hizo ikiwemo kambi ya Chumbuni.

Mhe. Naibu Spika, kwanza ninataka nilieleze Baraza hili kwamba kipindupindu hakiambukizwi kwa hewa. Kipindupindu kinaambukizika kwa kutumia maji machafu ambayo yamechafuliwa pengine na kinyesi. Kwa hivyo, ninamuomba Mheshimiwa atoe wasi wasi yeye pamoja na wananchi wanaokaa katika vijiji jirani kwamba kukaa kwa kambi pale katika vijiji vile vimeizunguka kambi ile, si athari wala hawatopata maambukizo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, na kwamba ushauri wake kuwa kwa nini wizara haioni haja ya kujenga hospitali nyengine mbali kwa ajili ya kushughulikia tu wagonjwa kipindupindu. Hili nalo pia kwa upande mmoja ni tatizo. Hivyo, mtoe mgonjwa wa kipindupindu Chumbuni. Maana maeneo ambayo yanajengwa kambi za kipindupindu, mara nyingi ni yale maeneo ambayo yapo *affected* na kipindupindu. Maeneo ambayo sasa hivi ni matatizo kwa kipindupindu sana ni

hilo la Chumbuni, Shaurimoyo, Mtopepo, Daraja Bovu pamoja na maeneo mengine. (*Makofi*)

Sasa si rahisi kuweza kumtoa mgonjwa wa kipindupindu hapo ukampeleka pengine Bungi, unamkimbiza mbio haraka na magari kwenye kituo cha kipindupindu kilichotengwa nje ya mji, atakufa wakati yupo njiani na hatoweza kupata huduma. Ndiyo maana Wizara ya Afya inaweka kambi katika maeneo ambayo yapo karibu na zile sehemu zipo na tatizo hili la kipindupindu. Kwa hivyo, naomba uondoe wasi wasi kwamba tatizo hili litaambukiza majirani zako, litaambukiza wananchi wako, wala hawaambukizwi kwa hili.

Mhe. Naibu Spika, jengine lilisemwa kuhusu Kituo cha Afya cha Sinzini. Kituo cha Afya Sinzini, sijamfahamu ni Mwakilishi gani lakini itakuwa ni jimbo hili hili linalohusiana na Sinzini. Alisema kwamba kimeanguka na wananchi wanapata huduma katika nyumba ya mtu binafsi.

Ni kweli, ninakiri kwamba kituo hichi kimeanguka na hakikuanza kuanguka tu, kwanza kilipasuka. Kilileta mpasuko kituo taratibu mpaka Wizara ikaona kituo hakikidhi mahitaji ya kuwashughulikia wananchi katika kituo kile. Kwa hivyo, wizara ilikaa na jamii na kuzungumza nao ili kutafuta *solution* ya jambo hili. Na alitokea mwananchi ambaye anaitwa Bakari Hamad, alikuwa Katibu wa CCM wa Mkoa wa Kusini Pemba na sasa hivi ni Mkuu wa Utawala Ofisi Ndogo ya CCM Dar-es-Salaam. Huyu alijitolea kutoa nyumba. Ndiyo hii nyumba ambayo mpaka sasa inatumika kwa kutoa huduma za afya katika Kituo kile cha Sizini. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ninataka nimuhakikishie na ninawahakikishie wananchi wa Sizini kwamba wizara kupitia Serikali Kuu inahangaika inatafuta uwezekano wa kujenga kituo kile ili kiweze kutoa huduma na yule mwananchi arudishiwe nyumba yake. Sasa hivi tayari imeshafanya mazungumzo na wafadhili ambao wanaitwa MILELE. MILELE wao wamekubali kukijenga kituo hichi na wametuahidi kwamba kitachukua muda wa mwaka mmoja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi. Mimi naomba sasa nichukue nafasi hii kuunga mkono hotuba hii ya bajeti kwa asilimia mia moja. Na ninaitakia kila la kheri. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hapa mbele yangu sina tena wachangiaji. Na ninatarajia kwamba tukijaaliwa kesho Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango baada ya kipindi cha Maswali na Majibu atakuja kujibu hoja zenu.

Kwa hivyo, kwa maana hiyo niwashukuru sana kwa michango yenu pamoja na utulivu wenu.

Naahirisha kikao hadi kesho tarehe 25/05/2016, saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1.21 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 25/05/2016 saa 3:00 asubuhi)